

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**(Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 24 Aprili, 2008)**

*(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel John Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2007 (*The Annual Report and Accounts of the Tanzania Communication Regulatory Authority (TCRA) for the year, 2007*).

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu sheria ya mwaka 1995 ya maadili ya viongozi hairuhusu kiongozi au mtumishi yeyote wa umma kutumia Ofisi za Serikali kwa shughuli zake binafsi. Rais wa Awamu ya Tatu na mmoja kati ya Mawaziri walitumia Ofisi ya Serikali kwa kuanzisha kampuni binafsi. Je, Serikali inachukua hatua gani kwa uvunjaji huu wa sheria?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, swali lake aliloliuza sasa hivi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala hili limeibuka kwa nguvu sana hivi karibuni na baadhi yetu bado tunalifuatilia na kujaribu kuona hali halisi ikoje. Kwa hiyo, tutakapokuwa tumepata maelezo ya kutosha na ya kina juu ya nini hasa kimetokea na kwa kuzingatia taratibu za nchi yetu tutafikia uamuzi ambao tunadhani utakuwa ni kwa maslahi ya taifa letu. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, swali moja la nyongeza. Kwa kuwa taarifa hizi zimetoka muda mrefu na kwa kuwa taarifa zote hizi

ziko kwenye Ofisi za Serikali kwa mfano Ofisi ya *BRELA* ina taarifa kamili ya uanzishwaji wa kampuni hizi. Kwa nini watuhumiwa wengine mara wanapopatikana na hatia wanapelekwa mara moja mahakamani kushitakiwa. Kwa nini hili la Serikali liwe na kigugumizi mpaka leo wasichukue hatua? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, unapelekwa mahakamani kunapokuwa kumejitokeza ushahidi wa kutosha kwamba umevunja sheria fulani. Sasa haya maelezo ambayo tumekuwa tunayapata ni kweli *BRELA* wanazo taarifa cha msingi hapa ambacho tunapaswa kujiuliza katenda kosa gani la jinai. Kwa sababu ni jambo moja kuzungumzia masuala ya jinai ni jambo jingine kama unazungumza masuala ya maadili, kwa maana ya uongozi.

Ni mambo mawili ambayo yanaweza yakatazamwa kwa mtazamo tofauti kabisa na ndiyo maana nimesema ni lazima tufike mahali tujiridhishe kama lililofanyika ni kwa kuwa wewe unadhani ni *criminal* au bado tunadhani ni jambo ambalo linaweza likashughulikiwa kwa utaratibu wa kawaida wa kisiasa. (*Makofi*)

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuninpa nafasi, ningependa kumwuliza Waziri Mkuu swali lifuatalo:-

Hivi sasa dunia nzima au nchi nyingi sasa zimekumbwa na uhaba wa chakula. Je, Tanzania tunajiandaa vipi kuhakikisha kwamba nchi haipati matatizo ya chakula? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, swali lake aliloliuliza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni dhahiri kabisa kwamba ni nchi ya wakulima kwa sehemu kubwa na kazi tuliyonayo kubwa ni namna ya kuboresha kilimo ambacho hivi sasa bado hakina tija kubwa kwa lengo la kuwezesha taifa hili kuwa na chakula cha kutosha kwa maana kwamba kwanza, kuweza kujilisha wenyewe. Lakini vile vile kuweza hata kutumia chakula hicho kuuza nchi za nje kwa maana ya nchi jirani na nchi nyingine. Kwa hiyo, wakati tunakubali kabisa kwamba ni kweli liko tishio kubwa na kwa sehemu kubwa limesababishwa na mfumo mpya wa matumizi ya nafaka kutumika katika uzalishaji wa mafuta ambao sasa umekuwa ndiyo kilio kikubwa hatuna budi na sisi kujipanga vizuri na tumekwishatoa maelekezo kwa wakuu wa mikoa wote kwanza kuchukua tahadhari ya ndani kwamba kilimo sasa ni lazima kipewe nafasi kubwa na kiwe na mipango madhubuti ili kujilinda katika janga ambalo linaweza likatokea mbele ya safari. (*Makofi*)

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa pia Serikali ilishaamua kutoa pembejeo kwa ruzuku Waziri Mkuu haoni ingekuwa jambo zuri sasa Serikali kuchagua mikoa ambayo wanayo hakika ina mvua za uhakika na watu wanaweza kusaidia kutoshereza nchi huko ndiko pembejeo zipelekwe?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mzindakaya swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Nadhani raia yake ni nzuri tulianza na wazo hilo mwanzoni lakini baadaye ikaonekana pengine lilikuwa linaleta matatizo makubwa zaidi kuliko tulivyokuwa tumefikiria. Lakini wako Waheshimiwa Wabunge wengi tu na baadhi ya viongozi ambao wanadhani tukianza kuliangalia kwa mtazamo huo. Hata kwa taarifa nilizonazo mpaka sasa Mikoa mitano ambayo ipo sasa hivi ambayo ndiyo tuna uhakika itakuwa na ziada ya chakula sehemu kubwa ni ile Mikoa ambayo inatoka Nyanda za Juu Kusini. Mara nyingi ndiyo wanatoa mazao mengi.

Lakini tunayo mikoa mingine mitano ambayo ndiyo tuna hakika kabisa watakuwa na upungufu wa chakula. Kwa hiyo, pengine ni jambo zuri kwa Serikali kutazama tuone kwamba tunaweza. Maana rasilimali ni kidogo pengine tukiweka nguvu kubwa katika maeneo yale ambayo tuna uhakika yanaweza kuzalisha vizuri zaidi na tija kubwa zaidi tunaweza tukafanikiwa zaidi kuliko ku-*spread resources* ndogo tulizonazo nchi nzima na matokeo yake *impact* yake inakuwa ndogo sana. Kwa hiyo, ni rai nzuri nafikiri litaangaliwa. (*Makofi*)

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize Waziri Mkuu kwa kuwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 inajihusisha kwa nguvu zaidi na maendeleo ya Michezo na kifungu (f) kinasema yatatengwa maeneo kwa ajili ya michezo. Kwa kuwa kumekuwa na mvutano mkubwa katika Jiji la Mwanza hususan Uwanja wa Nyamagana. Waziri Mkuu unatueleza nini msimamo ukoje wa Serikali kuhusu uwanja huo? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Shibiliti swali lake zuri sana kuhusiana na Uwanja wa Nyamagana pale Mwanza kama ifuatavyo:-

Kwanza niseme kwamba Uamuzi wa matumizi ya uwanja wa Nyamagana ambao kwa kipindi kirefu si uwanja tena unaotumika kwa madhumuni ya michezo uko ndani ya mamlaka ya Jiji la Mwanza. Serikali tutakachofanya ni kusaidia pale watakapohitaji msaada wa Serikali Kuu. Nimepata nafasi ya kutembelea uwanja huo nimeona hali ilivyo kwa uhakika huwezi kusema kwamba mnachojivuna nacho pale kweli ni uwanja. Si kweli pameharibika, hapapendezi pamebanwa na majengo mazuri makubwa hakuna eneo la kuegesha magari kwa sasa kwa hiyo kwa kweli ni jambo ambalo linapaswa kutazamwa tu *objectively* kwa maana ya kuona ni kitu tunafikiri kinaweza kikaleta maslahi kwa Mwanza. Bado naamini hata ni michezo mnaweza mkatafuta aina nzuri zaidi ya kutengeneza uwanja ule kwa lengo la kuwezesha michezo ya aina fulani iweze kufanyika katika eneo lile kama mnaona inafaa. Narudia kusema, uamuzi ni wa Jiji Serikali tutatoa utalaam, tutatoa *inputs* kwa kadri itakavyokuwa imependekezwa. (*Makofi*)

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwa na kauli mbalimbali za Serikali, Waziri wa Ardhi wa kipindi kilichopita alisema uwanja huo utaendelea kuwa wa michezo. Naibu Waziri wa Michezo wakati anajibu hapa Bungeni

alisisitiza hivyo na leo hii asubuhi Mbunge wa Jimbo la Nyamagana ameelezwa kwamba hautavunjwa. Unasemaje kuhusu hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, narudia maneno niliyoyasema awali uamuzi juu ya matumizi ya uwanja ule yako ndani ya mamlaka ya Jiji la Mwanza. Wengine tunachoweza kuwasaidia ni ushauri tu. Kama mnataka kupageuza pale au kupaendeleza kwa malengo ya michezo kwa maana ya *stadium* wakati mnayo Kirumba pale kubwa kabisa *well and good*.

Lakini lazima mfanye mahesabu muone kwamba kwa kufanya hivyo itakuwa ni kwa manufaa ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza au hapana. Ndiyo nasema mnaweza mkaendeleza wazo hilo lakini pengine itabidi kurebisha muone ni aina gani ya michezo ambayo inaweza ikafanyika pale. Kwa sababu kwa mazingira ya sasa ya Mwanza mimi sioni kama mnaweza kweli mkapaleka pale mchezo wa mpira wa miguu. Hakuna eneo la kuweka magari, eneo lile limebanwa sana sasa na majengo mapya yanayolizunguka eneo hilo.

Sana sana mnaweza labda mkafikiria *in door games* ambazo pengine hazi-attract watu wengi. Kwa hiyo, nasema kaeni chini jaribuni kuona ni kipi kipo kwa maslahi ya Jiji la Mwanza. Sasa wako wanaofikiria waweke pale hoteli, waweze kuwekeza katika mambo fulani fulani ya kiuchumi. Bado maamuzi ni yenu. Sisi hatuwezi kuingilia sana hayo ambayo yanasemwa na watu mbalimbali. (*Makofi*)

**MHE. OMAR S. KWAANGW’:** Mheshimiwa Spika, Watanzania wanapenda kuwa na maisha bora. Lakini uwezo wao wa kununua, ile *purchasing power*. unaathiriwa sana na upandaji wa bei za bidhaa. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, una mtazamo gani na unawaambia nini Watanzania kuhusu hilo? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo kuhusiana na swali ambalo ameuliza Mheshimiwa Kwaangw’. Kwanza tukubaliane naye kwamba ni kweli kabisa kwamba bidhaa zinapanda bei sana na wakati mwingine kwa haraka sana.

Katika hali ya kawaida Watanzania wengi hawana uwezo wa kuweza kwenda kwa kasi ya upandaji wa bei za vitu ambao sasa unajitokeza. Sasa sababu za kupanda bei ni nyingi lakini kubwa nadhani ambalo wote tunalijua pengine itakuwa ni mafuta kwa sababu hilo ni jambo ambalo linatuathiri sana. Siyo sisi Tanzania tu lakini hata nchi nyingine, hasa zile zinazoendelea. Kwa hiyo, hilo wakati tunalikubali na tunalitambua kazi kubwa tuliyonayo hapa ndani ni kutafuta tu namna ya kupunguza kasi ya watu kuzidi kupandisha bei na gharama za mafuta hayo bila sababu za msingi.

Lakini kichocheo cha kupanda kwa bei za mafuta unazikuta zinaathiri uzalishaji viwandani na karibu katika kila mahali hata usafirishaji wa bidhaa. Kwa hiyo, ni jambo kubwa na ni lazima wote tukiri kwamba hatuna budi kuweka nguvu pamoja ili tuweze kupambana na hiyo hali.

Kwa hiyo, na mimi nadhani kama Serikali tunachoweza kuwaahidi Watanzania ni kwamba kwa upande wa Serikali tutafanya kila juhudi kwanza kuimarisha vile vyombo vinavyosimamia bei mbalimbali au udhibiti wa bei mbalimbali ili kuhakikisha kwamba hilo linabakia katika uwezo ambao tunadhani ndiyo wa haki. Lakini vile vile ni lazima tuharakishe vile vile kufikiri haraka haraka kwamba kama tunataka kwa kweli kujitahidi katika eneo hili, ni lazima tuingie sasa katika mambo ambayo tunadhani yatuwezesha kupata mazao mengine kwa kupitia viwanda na hata na kilimo. Ni lazima vile vile tujikite katika *agro industries* ili tuweze kuwawezesha Watanzania katika mazingira yao waweze kupata fedha ambazo zinaweza zikasaidia kupambana na hiyo hali ambayo inatuathiri kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, kwa kifupi niseme ni kazi kubwa lakini nia ikiwepo tunaweza wote kwa pamoja tukakabiliana na hilo tatizo. (*Makofi*)

**MHE. OMAR S. KWAANGW’:** Mheshimiwa Spika, naomba tu ufafanuzi kwamba uwezo wa Watanzania ungeweza kuongezeka kupitia ruzuku inayotolewa na Serikali kwenye mbegu na mbolea. Lakini inaonekana ile faida ya ruzuku haiwafikii wakulima pale chini. Mheshimiwa Waziri Mkuu, unasemaje kuhusu hilo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, analiseme Mheshimiwa Kwaangw’, wote ni mashahidi tunajua ni kweli lakini ni lazima tuseme kwa nini haifiki huko. Kwanza ni kwa sababu mbolea yenyewe haitoshelezi mahitaji bado. Tunahitaji kujenga uwezo wa kuweza kupata mbolea yote inayohitajika. Kwa kweli kama tungeweza tukapata yote na yote ikawa kwa bei yenye ruzuku ya Serikali hiyo ingewawezesha Watanzania pengine wengi zaidi kupata hiyo mbolea. Lakini vyombo navyo ambavyo tunavyo ambavyo tumevipa kazi ya kusambaza mbolea Mheshimiwa Kwaangw’ vingine ni vyombo vyetu wenyewe. Lakini si waaminifu hata kidogo. Wamepewa dhamana ya kufanyakazi kwa nia nzuri lakini hao hao anauza mifuko kumi anakuambia imekwisha anabaki anaiuza kwa magendo, kwa bei kubwa *and these are the people* tuliowa-trust kwamba wafanye hiyo kazi. Ndiyo maana mimi nadhani mtazamo sahihi kwa sasa, ni watu tujitahidi kutumia *SACCOS* kwa sababu ni vyombo vyetu, vyombo vya wakulima, Vile, ndivyo viwe ndiyo hasa *conduit* ya kupitisha pembejeo.

Mimi nadhani Serikali tukijipanga vizuri, tunaliweza kabisa kwa sababu tumejaribu maeneo mengine na limeonekana kufanyakazi kwa ufanisi zaidi kuliko hawa watu binafsi mnaowaita mawakala kwa kweli ni tatizo kubwa sana. *Lets go for SACCOS.*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tukiendelea na kipindi hiki cha maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda mtambue kuwepo kwa Mama Tunu Pinda, Mkewe Mheshimiwa Waziri Mkuu namwomba asimame. Ahsante sana. Kwa taarifa tu mama, uliogopa bure, mzee huyu anaweza. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa Serikali imeamua kubinafsisha mashirika ya umma na mpaka sasa mashirika 216 tayari yamekwisha binafsishwa na ni baadhi ya mashirika ndiyo yamefanya vizuri kama Sigara na *Breweries* na mengine mengi hayakufanya kazi vizuri. Nadhani haya yamekiuka mkataba. Je, utawaambia nini wananchi kuhusu hayo mashirika ambayo

hayakufanya vizuri na mengine ambayo hayakumaliza hata kulipa ulipaji wa mashirika hayo? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo kuhusiana na swali la Mheshimiwa Ndugu Lekule Laizer. Kwanza niseme tu kwamba suala hili la ubinafishaji ni sera ya Chama chetu cha Mapinduzi na imekuwa ikitekelezwa sasa kwa muda mrefu na kwa ujumla wake matokeo ya sera hiyo sisi ndani ya Serikali tunaamini na tunadhani yamefanyakazi vizuri, kwa sababu viwanda vingi ambavyo vilikuwa katika hali mbaya sana, hali duni vimeweza kufurukuta na sasa vinatoa ajira. Vinatoa vile vile mchango mkubwa kwa Serikali kupitia kodi mbalimbali. Lakini ni kweli vile vile kwamba si makampuni yote, wala mashirika yote yaliyobinafsishwa yanaendelea kutimiza majukumu yake inavyotakiwa. Yako baadhi yamelegalega. Lakini ziko sababu nyingi zinazopelekea jambo hilo kutokea. Kwa hiyo, Serikalini tulichofanya ni kuwa na utaratibu wa kufuatilia utendaji kazi wa makampuni hayo na mengine tumechukua hatua za kurekebisha kwa kadri hali inavyoruhusu. Pale inapobidi tutachukua hatua ambazo ni kali zaidi tu kwa msingi kwamba umekiuka utaratibu tuliokubaliana. Kwa hiyo, uwezo wa kuchukua kama kuna ukiukaji ni kusitisha na mtu mwingine aweze kupewa chombo hicho kukiendesha. Lakini kwa kweli kwa sasa tunaweza tukasema hali si mbaya kama ambavyo watu wengi wanafikiria. (*Makofi*)

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Serikali ilikwishatenga fedha za kujenga barabara ya Marangu – Mwika, Mkuu Rombo na Mwika Kilacha, Jimbo la Vunjo. Kwa hivi sasa mkandarasi aliyekuwa anajenga barabara hiyo amesimamisha kuendelea na ujenzi na Serikali.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi wa Vunjo kuhusu kuendelea kujenga barabara hiyo?

**WAZIRI MKUU:** Naomba kutoa maelezo kwa Mheshimiwa Kimaro kuhusiana na barabara aliyoeleza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Kimaro usishtuke sana na hatua hizo za Serikali za kumsimamisha mkandarasi huyo ni wajibu wa Serikali pale inapotokea kwamba mkandarasi hatimizi majukumu yake vizuri na tunadhani kuwepo kwake si kwa maslahi ya nchi, Serikali lazima ichukue hatua kama hiyo. Inasimamisha mkataba na tumeshafanya sehemu nyingi hata *sehemu* hii ya Manyoni kutoka pale Isuna kuelekea Singida kule tumefanya hivyo. Lakini ni baada ya kuona kwamba utendaji kazi unasuasua na anaonekana hawezi kutimiza majukumu yake vizuri. Tunachoweza kukuahidi ni kwamba hatua hiyo ni kwa nia njema na baada ya muda si mrefu utaona hatua za Serikali sasa zitakazopelekea pengine kupata mkandarasi mwenye uwezo mkubwa zaidi ili aweze kutekeleza jukumu alilokabidhiwa kwa ufanisi mkubwa zaidi. Kwa hiyo, nakuomba ufanye subira tu kidogo utaona hatua za ziada zitakazofuata.

**MHE. SIJAPATA FADHILI FADHILI NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nimwulize Waziri Mkuu swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa Mkoani Kigoma hasa Kigoma Vijijini, Serikali iliamua kuwawekea alama ya x wananchi kwenye nyumba tangu mwaka 2004. Mwaka 2007 mwezi wa 8 mwaka jana Serikali tena ilipita ikawawekea namba kwanza wakaweka namba ya L halafu wakawawekea na tarakimu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sijapata X zimewekwa Wilaya nzima hujabainisha ni wapi?

**MHE. SIJAPATA FADHILI NKAYAMBA:** Kigoma Vijijini.

**SPIKA:** Ndiyo, Wilaya nzima?

**MHE. SIJAPATA FADHILI NKAYAMBA:** *Main road.*

**SPIKA:** Inatoka wapi kwenda wapi maana tuwe wazi.

**MHE. SIJAPATA FADHILI NKAYAMBA:** Barabara ya kutoka Mwandiga mpaka Kalinzi, barabara ya kutoka Mwandiga njia panda mpaka Uvinza na barabara nyingine kutoka Mwandiga kwenda Kasulu. Swali, kwa kuwa wamewekewa tarakimu x wakawa wanahesabu, wanawaandika majina, halafu wakawaambia kuwa watalipwa. Je, wale ambao walishahamishwa kwenye nyumba zao kwa kuzibomoa na kuzijenga upya kwa kuzisogeza nyuma. Je, watalipwa?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, swali hili ningependeza sana kama lingekuwa kwa maandishi ili tuweze kuona unacholenga ni nini. Lakini niseme tu kwa ujumla tu kwamba sehemu zote zile ambazo barabara kuu au barabara zile za Mikoa zinapita na ni sera ya nchi kwamba ni vizuri wale watu ambao wako ndani ya *road reserve* wakapewa fursa ya kuondoka kwenye maeneo hayo ili kupisha barabara zile zitakapokuwa zinatengenezwa. Namna peke yake ya kumpa ujumbe mtu wa namna hiyo ni kumwekea alama ya x ajue kwamba yuko ndani ya eneo la barabara. Lakini sababu ya pili kwa wale ambao kuwepo kwao pale kuwe kwa msingi wa kisheria kwa maneno mengine alipewa hati kabla barabara hiyo haijakuwepo huyo Serikali itafikiria kumpa fidia. Lakini kama wewe ndiyo ulikuja ukaikuta barabara na bado ukajenga pale hoja kwamba hukujua kwamba kuna sheria ya namna hiyo tukienda mbele ya Mahakama tutakushinda. Kwa hiyo, mimi naomba tu nitoe rai kwa sababu ni la jumla pengine ni vizuri ukaweza ukalibainisha vizuri zaidi ili tujue nani ambaye ana haki nani hana. Utaratibu mliokubaliana kati ya Wizara husika ukoje na kwa maana hiyo nani watastahili kulipwa hata wale wa zamani, lazima kutakuwepo na vigezo fulani ambavyo vitakuwa viliwekwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu maswali kwa Waziri Mkuu yanahusu sera haya mambo ya kuuliza mara daraja, ningependa kama Spika nijiridhishe kwamba kweli mnawashirikisha Waheshimiwa Mawaziri wa wa Sekta ili

tusimhangaisha Waziri Mkuu na mambo madogo tu. Lakini kwa kuwa bado tunajifunza na mimi niendeleo kuwa mkarimu kwenu.

**MHE. SIJAPATA FADHILI NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mimi nimeuliza hivi.

**SPIKA:** Usirudie swali nadhani nimekuita ili uulize swali la nyongeza.

**MHE. SIJAPATA FADHILI NKAYAMBA:** Swali la nyongeza kwa kuwa Serikali tena imepita mara ya pili imeweka tarakimu za rangi nyeupe na wakaambiwa kuwa wale waliokuwa wamewekewa tarakimu watalipwa na kuna wale ambao walishabomoa nyumba zao kabla ya hapo. Je, watalipwa na wenyewe? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Sijapata ndiyo nimesema si rahisi kwa Waziri Mkuu kulijibu swali hilo kwa nini, kwa sababu misingi ya kuweka tarakimu hizo nyeupe sasa na zile ambazo awali ziliwekewa x mimi sina maelezo kwa sasa kwa sababu ni jambo ambalo liko kwenye ngazi ya Wilaya pale Mkoani. Unahitajimaelezo ya kina ili waweze kufafanua na tuone vile vile maana yake nini hizo alama. Maana ukisema tu waliambiwa mimi sijui kama kweli waliambiwa hilo. Kwa hiyo, nadhani likija kwa utaratibu mwingine nitakusaidia zaidi. *(Makofi)*

**MHE. JAMES DAUDI LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kumwuliza Waziri Mkuu swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe 6 mwezi wa nne mwaka huu wananchi wapatao 150 wa kijiji cha Chapulwa kata ya Mwendakulima, Wilayani Kahama walivamia mgodi wa Buzwagi na kukata uzio kwa kutumia mashoka ili kutoa njia kwa wananchi kupita baada ya mgodi kuzungusha mgodi wote uzio.

Tarehe 21 mwezi wa 4 wananchi wapatao 500 wa Kata yote ya Mwendakulima walivamia mgodi wa Buzwagi katika lango kuu na kuzuia magari yasiingie ndani ya mgodi. Mheshimiwa Waziri Mkuu panapofuka moshi pana moto na kwa kuwa dalili tayari zinaonyesha pale Mwendakulima kuna moto mkubwa unaweza kufumka wakati wowote, Serikali inatoa kauli gani kuhusu hali hiyo ya Mwendakulima? Lakini pia Serikali inatoa kauli gani kuhusu wananchi wale 14 waliokamatwa na wamenyimwa dhamana baada ya tukio hilo? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikubaliane na Mheshimiwa Lembeli kwamba ni kweli kumekuwa na matukio aliyoyaeleza kwa tarehe hizo alizozitaja. Ni kweli vile vile kwamba baadhi ya watu walikamatwa na wamepelekwa kwenye vyombo vya sheria. Jambo hili lina namna nyingi za kulitazama. Nimejiuliza sana kwamba ni kwa nini wanafanya hivyo, lakini baadaye nikaelezwa kwamba kwa bahati nzuri wananchi wa eneo lile wote walilipwa fidia zao tena walilipwa zaidi kuliko hata Serikali ilivyokuwa imekadiria. Wamejitahidi pale wakawatengenezea barabara ambayo kufuatia uzio ule imelazimika barabara kuhamishwa kupelekwa sehemu nyingine ikachongwa lakini naambiwa wananchi hawataki kwenda kuitumia barabara hiyo



wanataka wapite hapo hapo. Nikaambiwa vile vile kwamba kwa ujumla ni kama vile wananchi wanasema sisi hapa hatuondoki tunarudi hapo hapo kwenye mgodi.

Sasa mkifika hapo tatizo linakuwa ni kubwa sana na tunamshukuru Mungu tu kwamba katika hali iliyotokea hapakutokea maafa au janga kubwa ambalo lingeweza likaitia Serikali katika majaribu makubwa sana.

Kwa hiyo, nitoe wito kwa wananchi wako wote Mheshimiwa Lembeli ambao wako kwenye mgodi ule kujitahidi sana kuepuka sana matumizi ya nguvu au kitu chochote ambacho kinaweza kikaonekana ni ukiukwaji wa Sheria kwa sababu haitawasaidia sana. Lakini pili, Serikali ni lazima tukubali kwamba iko haja ya kujaribu kusogea na kuzungumza na wananchi, tuzungumze na wenye mgodi ule ili tujue hasa tatizo ni kitu gani.

Sasa tumetuma Naibu Kamishna wa Madini, amekwenda pale kutufanyia *ground work* nimewaambia Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Ngeleja pamoja na Mheshimiwa Masha tukirudi Dar es Salaam tukutane na kama hapana budi basi tufanye utaratibu wa kwenda kwenye mgodi ili tuweze hasa kubaini tatizo likoje na tuweze kuwatendea haki wote wawili, mwenye mgodi na wale wananchi endapo itaonekana kuna upande wowote ambao haukutendewa haki.

Lakini narudia kutoa wito tafadhali sana, endelea kuwasihia wananchi wasitumie sana nguvu katika kujaribu kupata haki zao. Tupo kwa ajili hiyo, tuzungumze na yanawezekana yakaisha.

**SPIKA:** Kwa kufidia Mheshimiwa Lembeli.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa vile dhamana ni haki ya msingi ya mtuhumiwa yoyote kama makosa yake siyo makubwa sana. Je, unasema nini kuhusu wananchi wale 14 ambao kwa kweli hawakuwa na jembe, panga wala mawe lakini sasa wanajikuta wamenyimwa dhamana?

**WAZIRI MKUU:** Ndiyo maana nimesema Mheshimiwa Lembeli tusaidiane. Nitawaagiza watawaachia kwa dhamana, tutashauriana vizuri tu. Lakini na wao wasitumie nguvu kubwa wakati mwingine kupambana na vyombo hivi. Matokeo yake ni hayo, maana ukishawekwa ndani kutoka tena inakuwa shida. Lakini tutawasihi sana nina hakika wataachiwa, lakini tuwaombe basi wasitumie kasi ya namna hiyo kwa siku zijazo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwa kufidia ule muda wa mambo mengine ambayo yametufanya, utambulisho na kadhalika. Swali la mwisho Mheshimiwa Salim Hemed Khamis.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa Bunge letu ni chombo kikuu cha uwakilishi wananchi ambacho kimebeba heshima na hadhi maalum katika nchi yetu. Kwa kuwa katika hizi siku za karibuni kumetokezea baadhi ya watu kwenye vyombo vya habari wanajaribu kupaka matope Bunge letu

kuchafua jina la Mheshimiwa Spika kwa kukuhusisha na matumizi mabaya ya fedha katika Ofisi yako. Je, Serikali inayo taarifa ya hali hii, habari hizi na kama inazo imechukua hatua gani? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Kwanza nakushukuru sana, umeweka jambo hili vizuri sana kwa sababu na wewe umetumia lugha ile ile ya baadhi ya vyombo, baadhi ya watu wanatumia fursa kupaka matope watu, na kumpaka matope Spika, jambo ambalo linaonyesha wewe mwenyewe *you are not convinced* kwamba hayo ni kweli. Mimi nadhani jambo hilo ni zuri sana. *(Makofi)*

Sasa wakati mwingine kuyazuia haya mambo yanayopita kwenye mtandao, yanapita kwenye vyombo wakati mwingine si rahisi sana. Lakini tuliyasikia wote hapa, nina hakika na wewe ulikuwepo siku ile na ulisikia kauli alioitoa Mheshimiwa Spika na mimi nilidhani ilikuwa ni jambo zuri sana alikuwa jasiri sana kwamba alisema jamani nitafanya kila linalowezezana kuwapeni taarifa ya hali halisi juu ya mambo yote yanayodaiwa kwamba yamefanywa na Mheshimiwa Spika. Sasa mimi nilidhani Spika kwa nafasi yake akisema jambo namna hiyo kazi ya Serikali ni kumpa fursa hiyo aweze kutayarisha utaratibu na baadaye kwa kauli yake alisema atakuja kuwaambieni hapa ukweli wa mambo haya yakoje.

Mimi nadhani tsubiri, si jambo zuri sana tunampa pole kwa hili. Lakini aah! Ndiyo uhuru wenyewe tulio nao wa vyombo vya habari na mambo mengine. Nadhani tufanye tu subra kidogo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hapo ndiyo mwisho wa Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Kuhusu utaratibu

**SPIKA:** Utaratibu, Mheshimiwa Rished.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68. Naomba mwongozo wako, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anasimama hapo na tumeona kwa sasa tumeanza kuwa nusu saa lakini kwa kauli yako tuna mategemeo kwamba muda utaongezwa. Je, unasemaje Mheshimiwa Spika kama patakuwa na kiti ambacho pengine wakati mwingine Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kuketi na ajibu maswali.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu ana afya njema, na ni heshima kwamba Kiongozi kama huyu, Kiongozi wa ngazi ya juu kama huyo, anasimama kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge kwa niaba ya wananchi. Kwa hiyo tulilitafakari toka mwanzo na ikaonekana kwamba si vema kwa sababu maswali ya

papo kwa papo yanafuatana pale pale, hata zoezi kwa mfano leo Waheshimiwa Wabunge 9 mmeuliza na wanane mmeuliza na nyongeza. Nalo lingekuwa ni zoezi ambalo halijengi hadhi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa kama anafanya kwata, anakaa anasimama, anakaa anasimama. Kwa hiyo, nadhani utaratibu uliopo unatosheleza kabisa. Ahsante. (*Makofi*)

Katibu endelea kwa hatua inayofuata!

## **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 161

### **Nafasi ya Wabunge katika Uongozi wa Wilaya**

**MHE. MBAROUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa mara nyingi Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakipenda kufafanuliwa nafasi yao ya uongozi kiitifaki katika ngazi ya Wilaya na kwa kuwa ni muda mrefu umepita tangu Serikali ilipotoa ahadi ya kutoa ufafanuzi huo:-

- (a) Je, Serikali imefikia hatua gani katika utekelezaji wa jambo hilo?
- (b) Je, ni lini Serikali inatarajia kutangaza na kutekeleza uamuzi wake kuhusu suala hilo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ufafanuzi huu unazingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kwamba nchi yetu ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano. Maeneo ya Utawala yaani Mikoa, Wilaya na maeneo mengine yamegawanywa na Rais kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria na kwa kushauriana pia na Rais wa Zanzibar. Mikoa inaongozwa na Wakuu wa Mikoa na Wilaya zinaongozwa na Wakuu wa Wilaya wanaomsaidia Mheshimiwa Rais, kutawala na kuongoza wananchi.

Kwa mantiki hiyo basi, uongozi wa kiitifaki katika ngazi ya Wilaya unaongozwa na Mkuu wa Wilaya, na kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano au wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Viongozi wa Muhimili mingine ya dola yaani Mahakama na Bunge kama wapo huwa wanapewa kipaumbele katika kujumuika au kushiriki shughuli inayohusika. Itifaki inazingatiwa mapema wakati wa

maandalizi ili kuzitambua pia taasisi nyingine kama vile vyama vya siasa, madhehebu ya dini au watu maarufu wanaoheshimika katika jamii ya eneo hilo, eneo husika. Mikutano ya hadhara kwa ajili ya maendeleo ya wananchi huwa inaandaliwa na uongozi wa Serikali, ile ya vyama vya siasa na makundi mengine mbalimbali inaandaliwa na vyama na makundi husika na ambavyo huwa na itifaki yao.

(b) Mheshimiwa Spika, Mbunge ni mwakilishi wa wananchi wa jimbo la uchaguzi, viti maalum kupitia vyama vya siasa vilivyopata viti vingi vya Ubunge, Kuteuliwa na Mheshimiwa Rais au Uwakilishi wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Viongozi hawa ni wajumbe wa mabaraza mbalimbali pale wilayani na shughuli za Serikali zinatambua majukumu yao kwa mujibu wa Sheria zilizotungwa na Bunge hili. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge hili tukufu kwamba utaratibu uliopo kwa sasa unatambua nafasi ya viongozi niliowataja na azma ya kuimarisha itifaki katika ngazi ya wilaya ili kusimamia vema utekelezaji wa shughuli za umma.

**MHE. MBAROUK K. MWANDORO:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kunipa fursa kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri nafikiri bado ufafanuzi zaidi unahitajika. Inakuwaje wakati wa shughuli maalum kama vile ufukuzaji mwenge, au anapofika mgeni wa nchi katika Wilaya, Mbunge anaachiwa nafasi ya mwisho kabisa, na hulazimika kukimbia mara kwa mara. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, mimi naamini si mara nyingi inatokea kwamba katika misafara hasa misafara ya mwenge gari la Mbunge linakuwa nyuma kabisa. Kama ndiyo hivyo basi kuna dosari. Lakini tufahamu sote kwamba kule Wilayani tunakotoka kuna matatizo ya kila aina kutegemeana na Wilaya. Mara nyingine kunakuwa na upungufu wa magari na viongozi wengine hulazimika kupanda katika gari moja. Mara nyingine meza na viti vya kukalia havitoshi. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, haya yote yanawekwa maanani, lakini kwa vile Wabunge ni viongozi kule Wilayani na wanajihusisha katika maandalizi ya ujio wa viongozi wa kitaifa au mwenge, basi watoe ushauri huo katika vikao hivyo.

**SPIKA:** Naisihi Serikali tu iliangalie vizuri swala hili. Swali Ali Said Salim nyongeza? *(Makofi)*

**MHE. ALI SAID SALIM:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Wabunge upande wa Tanzania Bara moja kwa moja ni Wajumbe katika Halmashauri zao na kwa upande wa Zanzibar, Wabunge ambao ndiyo wawakilishi wa wananchi si Wajumbe katika Halmashauri jambo ambalo ni mapungufu makubwa. Je, Serikali ya Muungano haioni ni vema kuishauri Serikali ya Zanzibar ili kubadilisha utaratibu ili Wabunge nao wawe Wajumbe wa Halmashauri wanakotoka?

**SPIKA:** Hili ningeomba liulizwe swali mahsusi kwa sababu ni jipya. Swali lililopo mbele yetu ni la itifaki na hili ni suala la uwakilishi ambalo ni tofauti. Tunaendelea.

Na. 162

### **Usumbufu wa Kufuata mishahara benki**

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA** aliuliza:-

Kwa kuwa watumishi na watendaji mbalimbali wanaofanya kazi vijijini wakiwemo walimu na wagani wa sekta mbalimbali kwenye jimbo la Songwe hupata shida sana kufuata mishahara yao umbali wa km 80 hadi 200 kwenda kwenye Tawi la *NMB* lililoko Chunya kila mwezi ambapo baadhi yao hutumia wiki kabla ya kurudi vituoni mwao.

- (a) Je, Serikali haiwezi kuzungumza na *NMB* ili kuanzisha huduma ya benki huko vijijini, kwa mtindo wa *mobile banking system services*?
- (b) Kwa kufanya hivyo. Je, Serikali haioni kuwa itawaongezea tija na morali ya kufanya kazi watumishi hao na kuongeza ufanisi kazini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Guido Gologolio Sigonda, Mbunge wa Songwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, nakubalina na Mheshimiwa Sigonda, Mbunge wa Songwe, kwamba huduma za benki zinaposogezwa karibu zaidi na wananchi na wafanyakazi zinaongeza tija na motisha kwa watumishi ya kufanya kazi na hivyo kuongeza ufanisi. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge pia kuwa kuanzishwa kwa huduma za kibenki kwa njia ya magari kutasaidia watumishi, watendaji na wananchi pale ambapo si rahisi kufungua Tawi. Ninamwomba Mbunge wa Songwe, Mheshimiwa Sigonda tushirikiane ili tuone jinsi huduma za kifedha zinavyoweza kuboreshwa kwa ajili ya wananchi wa Jimbo lake la Songwe.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kushawishi vyombo vya fedha kusogeza huduma karibu na wananchi kote nchini ili waweze kuzitumia kwa urahisi na bila kuhangaika sana. (*Makofi*)

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa tatizo hasa la kero hiyo ni ukubwa wa eneo la Wilaya ya Chunya na kwa sababu tayari mikakati imekwishaanza kufanyika ya kuiomba Serikali iipatie Wilaya hiyo Wilaya nyingine, kwa

sababu jitihada hizo tayari zinafanyika. Je Mheshimiwa Waziri utakubaliana na mimi kwamba tushirikiane kwa kuhimiza Serikali ili kusudi Wilaya hiyo igawanywe? Swali la kwanza.

Swali la pili, kwa sababu umekubali mwenyewe kwamba tutashirikiana. Je, uko tayari kuja katika Wilaya ili kusudi uthibitisha haya yote ambayo nayasema? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ungejibu lile swali la pili tu. Lile la kwanza siyo jukumu la Wizara ya Fedha kuhimiza kugawanywa Wilaya.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, ninakubali kabisa na ninaitikia wito wake na kukaribishwa kwake kutembelea Songwe itakuwa ni heshima kubwa. Kwa hiyo, tukutane tupange ni lini tutakwenda. Nitashauriana na Mheshimiwa Waziri wangu tukishamaliza tutakwenda Chunya na tutaangalia mambo yalivyo.

**MHE. MANJU S.O. MSAMBYA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mazingira ya Songwe hayana tofauti na mazingira ya Wilaya ya Kigoma Vijijini na hasa Kata ambazo ziko mwambao wa Ziwa Tanganyika. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari vile vile kushirikiana na mimi ili tuone namna ya kuwasaidia watumishi walioko maeneo hayo na hasa kama inawezekana hiyo *mobile service* iwe ya *speed boat*? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwanza nikubali mwaliko wake na yeye vile vile tutashauriana Wizarani pale na ninamwahidi kwamba itakuwa heshima kufika Kigoma.

La pili naomba nitoe maelezo ya jumla kwamba Serikali tangia ilipoamua kujiondoa kwenye kuendesha vyombo vya fedha uwezo wake wa kulazimisha vyombo hivi kufungua matawi ama ya magari ama ya *speed boat* ama matawi ya kawaida si mkubwa sana. Kwa sababu vyombo hivi vina *management* zake na zina Bodi zake na haya masuala ya kufungua matawi haya ni jambo la kiutendaji. Kwa hiyo, Serikali inachofanya ni kukaa karibu na benki hizi na kushauriana na mara nyingine kwa kweli ni kuwaomba kwa niaba ya wananchi wetu kupeleka hizi huduma za fedha kwenye karibu na wale wananchi.

Kwa hiyo, pamoja na kusema kwamba tuko tayari kwenda Chunya, tuko tayari kwenda Kigoma, tuko tayari kwenda Bumbuli na Wilaya nyingine. Naomba tukumbuke kwamba hapa hatuahidi kwamba tutakavyofanya hivyo tutakwenda kufungua matawi ya benki la hasha. Tutakachofanya ni kwenda kujiridhisha kwamba *yes* kuna uwezekano wa hapa kuwa na tawi la benki na kwa hiyo tunapozungumza na benki hizi na kushauriana tunakuwa na nguvu zaidi ya kujenga hoja.

## Mapato yatokanayo na uwindaji

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Iringa ina hifadhi ya Ruaha na Vitalu vya uwindaji na kwa kuwa mara kwa mara *TANAPA* hutoa misaada kusaidia maendeleo ya huduma za kijamii kama shule, zahanati na kadhalika. Katika Wilaya yenye hifadhi hizo kwa mujibu wa programu ya Serikali ya ujirani mwema:-

- (a) Je, Serikali inaweza kutoa taarifa ya kwamba ni kiasi gani cha misaada kilichotolewa kwa maeneo yanayozunguka hifadhi hizo katika Wilaya ya Iringa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita?
- (b) Je, Wilaya inafaidika vipi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma, Mbunge wa Kalenga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Jumla ya miradi nane (8) iliyogharimu shilingi milioni 100,594,300.00 imetekelezwa kati ya wananchi wa Wilaya ya Iringa na Hifadhi ya Taifa ya Ruada katika kipindi cha miaka mitatu (2005/2006 hadi 2007/2008). Miradi hiyo ni pamoja na uwekaji wa samani bweni la wavulana katika shule ya sekondari Idodi. Ujenzi wa madarasa mawili na Ofisi, Shule ya Msingi Kitisi na ujenzi wa joshu la mifugo kijiji cha Malinzanga. Miradi mingine ni ya ujenzi wa nyumba ya mwalimu shule ya msingi Kinyika, ujenzi wa zahanati ya kijiji cha Nyamakuyu, ujenzi wa nyumba ya muuguzi kijiji cha Mafuluto, ununuzi wa samani na ujenzi wa bwalo la chakula na jiko shule ya sekondari Pawaga.

(b) Mheshimiwa Spika, mpango wa ujirani mwema wa *TANAPA* huzipunguzia Halmashauri za Wilaya gharama zinazohitajika kutekeleza miradi ya maendeleo vijijini. Aidha, Halmashauri hubakia na kazi ya kuhakikisha miradi hiyo inapatiwa wafanyakazi na vifaa vinavyohitajika kama vile madawa ili yaweze kutumika ipasavyo. Aidha, Wilaya ya Iringa ni mojawapo ya Wilaya 42 zinazonufaika na mgawo wa asilimia 25 kutokana na uwindaji wa kitalii, ambapo katika kipindi cha miaka mitatu Wilaya hiyo ilipata kiasi cha shilingi milioni 11,848,260.00.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Spika kuniruhusu niulize maswali ya nyongeza. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake hata hivyo napenda kuuliza maswali ya nyongeza mawili. Kuhusu miradi inayotekelezwa ya shilingi milioni mia moja na nusu napenda kusema kwamba yote hii imetekelezwa mpakani au pembezoni lakini mbuga na hifadhi ni mali ya wananchi wote kwa ujumla

wao. Sasa inakuwaje wanaofaidika ni watu wachache wa mipakani. Je, Waziri atakubaliana nami kwamba wananchi wa Iringa hawatendewi haki?

Swali la pili, juu ya mgao wa ile asilimia 25 katika miaka mitatu tumelipwa milioni 11.8 au milioni 3.9 kila mwaka. Kiwango hiki ni kidogo sana ni kama utani tu. Je, ni kigezo gani kinatumika kwa nini kusiwe na kigezo kinacholeta haki zaidi kwa wananchi wa Wilaya ya Iringa? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya TANAPA kutekelezwa pembezoni mwa hifadhi, kama nilivyosema mpango huu ni wa ujirani mwema ambao unashirikisha wananchi wa vijiji ambavyo vinakuwa jirani na hifadhi. Kwa maana hiyo lengo hasa ni kuangalia ni namna gani vijiji hivyo ambavyo viko jirani na hifadhi vinashiriki katika shughuli za uhifadhi. Lakini pia matarajio ni kwamba vijiji hivyo ndiyo vinakuwa vinaathirika na *inter face* kati ya binadamu na wanyama. Wao ndiyo wanyamapori wanakotoka kwenye hifadhi, wanakwenda kushambulia kwenye maeneo yao, kwa maana hiyo ilionekana pengine ni vizuri kushirikiana na watu hawa ili waweze kuona umuhimu wa uhifadhi, umuhimu wa kutunza wanyama hao. Mantiki hiyo inaonyesha kwamba pengine kwa mtu mwingine ambaye yuko mbali zaidi hawezi akaona madhara yanayojitokeza kutokana na wanyama hao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili kwamba kiwango kinachotolewa ni kidogo cha asilimia 25 kuna sababu nyingi au vigezo vingi vinavyotumika kupata kiwango hiki. Kwanza kiwango hiki hutegemeana na shughuli zenyewe zilizofanyika katika mwaka husika. Lakini pia mapato haya si kwamba ni mapato yenyewe tu yote yanakwenda kwenye Halmashauri hiyo kama tulivyosema ni asilimia 25. Na hiyo asilimia 25 ni baada ya kuwa asilimia 25 nyingine imetolewa kwa ajili ya uendelezaji wa uhifadhi kwenye ule mfuko unaoitwa *TWDF*. Kwa hiyo, kinachobaki ndiyo asilimia 25 yake inakwenda kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, kiwango hiki kinakuwa ni kidogo lakini kinategemea na shughuli zilizofanyika na mgao wake pia unahusishwa na *balance* inayokuwa imebaki baada ya kuwa tumetoa kiasi kinachokuwa kinatakiwa kwa ajili ya ule mfuko unaohusika na uendelezaji wa uhifadhi. (*Makofi*)

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa suala la msingi la hifadhi ya Ruaha linafanana kabisa na hifadhi ya Mlima Kilimanjaro. Ningependa kujua kwamba wale wananchi wanaoishi kuzunguka Mlima Kilimanjaro wanafaidikaje na *park fees* zinazolipwa kutokana na Mlima ule? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Kilimanjaro kuna *National Park* inayoitwa *TANAPA*. Kama ilivyo kwenye hifadhi zingine mpango huu wa ujirani mwema unaotekelezwa na *TANAPA* na kwenyewe pia unatekelezwa. Kwa sasa siwezi nikataja miradi ambayo imetekelezwa na *TANAPA* kwenye maeneo yanayozunguka hifadhi hiyo. Lakini naamini mpango huu pia upo na takwimu zikihitajika kama ilivyoonyesha sasa hivi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nini kimefanywa na *TANAPA* kwenye maeneo ya hifadhi hiyo, naweza



kumwonyesha baada ya kuwa tumecheke na Takwimu zetu Ofisini. Lakini huu mradi wa ujirani mwema unahusu hifadhi zote ambazo ni za Taifa zinaendeshwa na TANAPA. (Makofi)

Na. 164

### ***Menopause* kwa akina mama**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Kwa kuwa zaidi ya asilimia sabini na tano (75%) ya wanawake duniani wakifikisha umri wa miaka 40 na kuendelea wanapitia kipindi kigumu sana cha mpito kitiwacho *Menopause* na kwa kuwa kipindi hiki kinabadilisha sana tabia za wanawake hao na kusababisha matatizo mengi yanayogusa hata familia husika. Je, Serikali inafanya jitihada gani kuelimisha jamii yote iweze kuelewa kikamilifu mabadiliko hayo ili iweze kuwavumilia kina mama wanapokuwa katika kipindi hicho kama inavyofanywa katika nchi zilizoendelea?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anne Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa *menopause* siyo ugonjwa. Katika hali ya kawaida, mwanamke yeyote mkamilifu baada ya kuvunja ungo huendelea kupata hedhi kila mwezi hadi kufikia umri wa miaka kati ya 40 hadi 52 ambapo mwanamke huacha kabisa kupata hedhi. Hali inayotokea kwa mwanamke katika kipindi hicho ambacho hedhi imekoma kabisa kitaalam ndiyo inaitwa *menopause*. Mabadiliko yanayotokea baada ya mwanamke kufunga hedhi ambayo yanatokana na kupungua kwa kichocheo (homoni) ya istrojini. Mabadiliko haya hupokelewa kitofauti kati ya mwanamke na mwanamke. Baadhi ya mabadiliko ni kama kupata joto hasa wakati wa usiku au *hot flash* kuwa mkali kuliko kawaida. Kupungua hamu ya tendo la ndoa au kuongezeka kwa hamu ya tendo la ndoa. Kukosa usingizi, kuongezeka uzito na kadhalika. Aidha, wanawake wengine hawapati mabadiliko yoyote katika kipindi chote cha *menopause*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Wizara yangu haina mkakati wowote kuelimisha jamii yote kwa ujumla wake kuhusu suala hili. Hata hivyo, elimu kwa mtu mmoja mmoja hutolewa kliniki na hospitali. Mheshimiwa Spika kupitia Bunge lako tukufu naomba kutoa wito kwa akina mama wote wanapojikuta katika hali hii wafike mara moja hospitali ili kupata ushauri wa kitaalam.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kutuelimisha Taifa zima kuhusu *menopause*.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa, utafiti uliofanyika kwa nchi yetu ya Tanzania imeonekana kwamba wanaume zaidi ya asilimia 35 wanapigwa na wake zao japo huwa hawasemi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sisi wanawake wengi tumefanya utafiti tukagundua kwamba ile asilimia ya wanawake wanawapiga waume zao ni wale wanawake ambao wanakuwa wako kwenye kile kipindi cha mpito cha *menopause* ambacho hawafanyi hivyo kwa makusudi. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kutoa japo vipeperushi Tanzania nzima kuwaelimisha kina baba ili waweze kuwavumilia wake zao wanapokuwa kwenye kipindi hiki cha mpito ambacho ni kigumu kuliko ambavyo ikiachiwa hivyo inaweza ikasababisha ndoa nyingi sana kuvunjika wakati wa kipindi hiki ambacho kina mama hawafanyi hivyo kwa makusudi? (*Makofi/Kicheko*).

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, haya matatizo ya *menopause* yanazo dawa ambazo zinapunguza makali ya *menopause*. Na dawa hizi zinasaidia sana wanawake wengi kutokana na matatizo haya na si kwamba ni matatizo madogo, ni matatizo makubwa sana kwa wanawake wengi. Je, Serikali haioni kwamba ni vyema pia na sisi Tanzania tukatafuta madawa haya ili tuweze kuwapunguzia kinamama adha ya kukutana na matatizo mengi ya kipindi cha *menopause*?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Ni kweli katika tafiti zinaonesha asilimia 35 ya wanaume huwa wanapigwa na wake zao. Ni ukweli kabisa kwamba elimu ya kutosha inahitaji kutolewa kwa wana familia hawa ambao wanaleta mzozo katika nyumba zao. Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu suala la *menopause* ni kwamba mama anakuwa mkali na hivyo baba anashindwa kuelewa ni kitu gani kinaendelea. Kwa hiyo, yeye anapata hisia nyingine ambazo zinasababisha labda kuleta ugomvi katika nyumba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nachukua ushauri wake kwamba Wizara ya Afya, itajaribu kuandaa vipeperushi na kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kufahamu kwamba inapofikia kipindi cha *menopause* mama anahitaji msaada mkubwa sana ili aweze kupita kile kipindi cha mpito. (*Makofi/Kicheko*).

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili. Ni ukweli kabisa kwamba kunahitaji kuwe na dawa, lakini katika tafiti ambazo zimefanywa zinaonesha kwamba tatizo la *menopause* kunakuwa na *imbalance* ya *hormones* kati ya *oestrogen* na *progestron* na kwamba hiki kipindi ni kipindi cha mpito ndani ya mwaka mmoja inakuwa imeisha. Lakini tafiti zimeonesha kwamba kwa sasa hivi hakuna dawa *specific* ambayo tutasema tumpe mwanamama ili aweze kupunguza haya makali ya dalili za *menopause*. Ziko *hormones* ambazo anaweza kupewa, saa nyingine anaweza akapewa dawa za uzazi wa mpango ili aweze kuzuiya lakini *so far research* imeonesha kwamba haiwezi kumsaidia.

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kusema, tuweze kuwasaidia kina mama hawa wanapokuwa katika hali hii ili tuwape *support*. Ni kipindi kifupi cha mwaka mmoja na baadaye matatizo haya yataisha na atarudia maisha yake kama kawaida. Asante sana. (*Makofi*).

**MHE. FATMA ABDULHABIB FERREJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, pamoja na matatizo ambayo yanatukabili sisi wanawake kuanzia umri wa miaka 40 na kuendelea yanayotokana na *menopause*, lakini wana saikolojia wame *prove* kwamba wanawake na wanaume wote wanapofika umri wa miaka 40 na kuendelea, wanapita katika kipindi kigumu kinachoitwa *middle age crisis*.

Je, Wizara yako ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba inaisaidia jamii kusaidia matatizo ya kupunguza ndoa kuvunjika na kupigwa kwa wanaume na wake zao na wanaume kuacha kwa wingi wake zao. Vile vile kuwa makini katika kipindi hicho cha *middle age crisis* ili jamii ibakie kuwa moja? Kwasababu katika kipindi hicho ndoa nyingi huvunjika? (*Makofi*).

**SPIKA:** Majibu, naibu Waziri wa Afya. Nadhani suala hili linavyoonesha litahitaji semina wakati wa mkutano wa Bunge. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Fereji, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa inapofikia miaka miaka ya 40 wanaume na wanawake huwa kunakuwa na mabadiliko mengi sana katika makuzi yao na hali ambayo wanavyojisikia. Nakubaliana kabisa kwamba inahitajika uelewa mkubwa watu wafahamishwe katika hii *middle age crisis* ili watu waweze kudumisha ndoa zao. Lakini kwa ushauri wako Mheshimiwa, nitawasiliana na Waziri na Wizara yangu ili tuweze kuona kwamba ni jinsi gani tutatoa elimu kwa Waheshimiwa Wabunge, ili kuweza kuona mabadiliko kuanzia miaka 40 na kuendelea ni jinsi gani mabadiliko mwanadamu anayapata na jinsi gani ambayo tunaweza tukasaidia ili kuweza kuishi maisha mazuri na hatimaye kulinda ndoa za waume na wake zao. Ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 165

**Kupeleka Vifaa vya Kisasa na Wataalamu Kwenye  
Zahanati na Vituo vya Afya**

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O K.n.y. PINDI H. CHANA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM imepewa jukumu la kuzipatia vifaa vya kisasa na wataalamu hospitali, vituo vya afya na zahanati za Serikali katika kipindi cha 2005 – 2010:-

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa kuna upungufu mkubwa wa wataalamu wa afya katika hospitali, vituo vya afya na zahanati za Serikali nchini kama Lupanga (Ludewa) Kisanga, Mtambile (Mufindi) na hospitali ya Mkoa wa Iringa kwenye Wadi ya Wazazi?

(b) Je, ni sababu zipi zilizosababisha upungufu wa wataalamu kama ilivyoelezwa kwenye swali (a)?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na tatizo la upungufu wa wataalamu wa afya nchini?

(d)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu na kutambua upungufu mkubwa wa watumishi uliopo ndani ya Sekta ya Afya zikiwemo hospitali za Ludewa, Kisanga, Mufindi na Hospitali ya Mkoa wa Iringa. Kulingana na tathmini iliyofanyika Juni, 2006 kulikuwa na watumishi wa afya wapatao 15,060. Hii ni sawa na asilimia 32 ya watumishi wote wanaohitajika.

(b) Sababu za upungufu wa watumishi wa afya kama ilivyoeleza katika kipengele (a) hapo juu ni kama ifuatavyo:-

1. Kiwango cha ajira zinazoidhinishwa ni kidogo ukilinganisha na kiwango cha watumishi wanaohitajika katika sekta husika.

2. Ikama ya watumishi katika sehemu za kutolea huduma imepitwa na wakati ikilinganishwa na ongezeko la idadi ya watu na maradhi.

3. Kiwango cha wahitimu wa taaluma za afya ni kidogo kuliko mahitaji halisi ya rasilimali watu. Mfano, katika kipindi cha miaka 9 iliyopita kumekuwa na jumla ya wahitimu 20,943 kiwango hiki ni kidogo kuliko rasilimali watu inayohitajika kwa sasa ambao ni 31,808.

4. Maslahi na mishahara isiyolingana na hali halisi ya mahitaji muhimu na hivyo kuwafanya watumishi waondoke katika ajira za Serikali na hasa katika sehemu zenye mazingira magumu.

5. Na pia kufariki au kustaafu kwa baadhi ya watumishi.

(c) Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na tatizo la upungufu wa watumishi wa afya nchini, Wizara imechukua na kutekeleza hatua zifuatazo:-

1. Kulegezwa kwa masharti na taratibu za ajira za Serikali kwa watumishi wa kada ya afya kwa kupangiwa vituo vya kazi moja kwa moja toka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii mara baada ya kuhitimu mafunzo yao.

2. Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya afya.

3. Utekelezaji wa mikakati ya kuwafanya watumishi kudumu katika utumishi wa umma kwa kuboresha mazingira ya kazi.

4. Wizara kwa msaada wa *Global Fund* inatarajia kutoa ajira za mkataba kwa watumishi wa afya ili kuongeza idadi ya watumishi katika sehemu za kutolea huduma za afya hususani katika vituo vinavyotoa huduma ya dawa za kupunguza makali ya UKIMWI.

5. Kuanzishwa kwa Taasisi Maalum (*Mkapa Foundation*) kushughulikia ajira za mkataba kwa watumishi wa kada za afya kwenda kufanya kazi sehemu za mazingira magumu.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake ni mazuri. Nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, hospitali ya Mafinga, Wilayani Mufindi ni hospitalui ambayo ipo kwenye barabara kuu na ajali nyingi zinatokea na pia inahudumia wagonjwa kutoka Wilaya nyingine ikiwemo Wilaya ya Iringa Vijijini na Wilaya ya Mbarali. Je, Serikali itakuwa tayari kuwaongezea watumishi pamoja na vifaa ili kukidhi mahitaji makubwa ambayo hospitali hii inakutana nayo?

Swali la pili. Kwa vile kuna upungufu wa dawa kwenye vituo vya *CTC* hasa dawa za kupunguza magonjwa nyemelezi kama septrin. Je, Serikali itakuwa tayari kuhakikisha kwamba vituo vyote vya *CTC* nchini vinapewa dawa za kutosha za magonjwa nyemelezi ukizingatia kwamba wagonjwa wengi wanatoka vijijini na wanapokwenda pale hospitali wanakuta hizo dawa hazipo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ledian Mng'ong'o, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Kweli kabisa hospitali ya Mafinga inahudumia wagonjwa wengi kuliko kawaida yakena ina uhaba wa vifaa na watumishi kama nilivyokuwa nimesema katika jibu langu la msingi kwamba tunafanya utaratibu wa kuhakikisha kwamba watumishi wanakwenda kule. Ninachotaka kumwambia Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba suala la vifaa, hospitali ya Wilaya iangalie jinsi gani itaweza kununua vifaa kutoka katika zile pesa za *Basket Fund*, ili kuweza kupata na pesa ambazo zinatoka katika Wizara ili kununua vifaa.

Lakini suala la watumishi, tunaomba walete maombi yale ambayo yameruhusiwa yako *budgeted* na sisi tutaangalia kuweza kuona kwamba tunawapelekea watumishi wengine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa dawa za kutibu magonjwa nyemelezi katika vituo vya *CTC*, tutafuatilia jambo hili ili tuweze kuona kwamba upungufu ni kiasi gani. Lakini nitawashauri vilevile wale madaktari husika katika vituo vyote vya hospitali iwapo kunatokea upungufu wa dawa za kutibu magonjwa nyemelezi basi maramoja walete taarifa ili waweze kupatiwa hizi dawa kwasababu ni muhimu sana kwa wale wagonjwa ambao wanapata dawa za kurefusha maisha. (*Makofi*).

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika sehemu ambayo wananchi wake wanaadhibika kwa kiwango kikubwa kabisa ni wananchi wa Wilaya ya Mafia haswa wanaokaa vijijini, kwa tatizo la upungufu mkubwa wa watumishi wa zahanati au wa Idara ya Afya kwa ujumla.

Je, Serikali inaweza ikatupa kipaumbele kwa vijana wetu wanaomaliza kidato cha nne waweze kuwachukua na kwenda kuwapeleka katika vyuo hivi vya utabibu au wa unesi, na baadaye waweze kurudi kuja kuwahudumia wananchi wa wilaya ile ya Mafia, kwasababu hata tunapopata ikama za watumishi hakuna mtu anayetaka kuja Mafia?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shah, Mbunge wa Mafia, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kumwambia Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba kama kuna wanafunzi ambao wamemaliza sekondari na amefaulu vizuri masomo ya sayansi, atuletee majina ili tuweze kuhakikisha kwamba tunaipa kipaumbele Wilaya ya Mafia. (*Makofi*)

Lakini vilevile ninaomba pia Waheshimiwa Wabunge, tujaribu kuwa *convince* watoto wetu wanaposoma na kama mtaona kuna watoto wamefaulu vizuri, tuleteeni majina ili tuweze kuona kwamba tunawapangia vyuo na hatimaye tuwarudishe katika Wilaya husika. (*Makofi*)

Na. 166

### **Ujio wa Rais wa Marekani Nchini Tanzania**

**MHE. SALIM HEMEDI KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa tarehe 16/2/2008 Tanzania ilipata ugeni wa kiongozi mkubwa duniani Rais George W. Bush wa Marekani:-

Je, Tanzania ilifaidika vipi kisiasa na kiuchumi kutokana na ujio wa kiongozi huyo maarufu duniani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemedi Khamis, Mbunge wa Chambani, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza kisiasa ziara ya Rais George W. Bush nchini Tanzania ni ishara kwamba sera zetu za ndani na nje zinakubalika kimataifa. Aidha, kwa kuwa Rais George W. Bush ni Rais wa Taifa kubwa duniani, ziara yake ilitangazwa kote duniani moja kwa moja na vyombo vingi vikubwa vya habari duniani. Hivyo, kupitia ziara hiyo Tanzania imepata fursa ya kujulikana zaidi duniani.

Mheshimiwa Spika, kiuchumi Tanzania ilifaidika na ziara hiyo kwa Rais Bush na Rais Kikwete kusaini mkataba wa *Millennium Challenge Compact* au *MCC* ambapo Tanzania itapata msaada wa dola za Kimarekani milioni 698 kwa miaka mitano kusaidia ujenzi na uimarishaji wa miundombinu ya barabara, nishati na maji katika maeneo mbalimbali ya Jamhuri yetu ya Muungano.

(b) Mheshimiwa Spika, pili misaada mikubwa ya fedha katika kupambana na malaria na ukimwi imeendelea kutolewa kwa kupitia mpango wa Rais wa kudhibiti maambukizi ya *UKIMWI* au *President's Emergency Plan for HIV/AIDS Relief* na mpango wa Rais kudhibiti malaria, *President's Malaria Initiative*, kama sehemu ya kupambana na malaria. Rais George W. Bush aliagiza vyandarua milioni 5.2 kutoka katika kiwanda cha *A to Z* cha Tanzania kilichopo Arusha. Vyandarua hivyo, vitanunuliwa na Serikali ya Marekani na vitasambazwa hapa Tanzania katika mradi wa kupambana na malaria.

(c) Tatu, kutokana na Tanzania kutangazwa sana katika ziara hii, tunaamini nchi yetu imejitangaza kwa wawekezaji na watalii zaidi kutoka nje.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, ujio wa Rais Bush, hapa nchini ulitoa neema nyingi kama alivyosema Mheshimiwa Waziri. Miongoni mwao Barabara zetu ziliparwa, kwa mfano barabara ya Uhuru, kwenda hospitali ya Amana iliparwa ikawekewa lami japo ni robo kilometa. Haspitali zetu vilevile zilikarabatiwa. Je, Serikali ilipata wapi fedha hizo wakati kabla ilidai kwamba haina fedha?

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, Je, serikali sasa itakuwa tayari kuwakaribisha wageni kama Bush, kutembelea nchi yetu? Maana inaonekana kwamba kuja kwao ni neema na kutatua matatizo sugu ya nchi hii? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ningependa kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli wakati Rais Bush alipokuja kutembelea Tanzania sehemu mbalimbali zilifanyiwa marekebisho. Lakini hili ni jambo la kawaida, hata wewe ukipokea mgeni nyumbani kwako chumba utakachomweka lazima utakikarabati, utakiweka kizuri. Kwa hiyo, kwa hili ni jambo la kawaida. (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, fedha zilikuwepo kwaajili ya matumizi ya kukarabati barabara hizi. Lakini tumepata kichocheo kwa ugeni huu ndio maana zikatumika kwaajili ya ukarabati.

**MHE. MWANAWETU S. SARAFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi nina swali dogo la nyongeza. Kwa jinsi ninavyomfahamu Mmarekani, tunaweza tukaeleza nini kilichomvutia kiongozi huyu mkubwa hadi akasifia nchi yetu ya Tanzania licha ya amani na utulivu ambao yeye hakuwa ameuona kwasababu alikuwa amekuja na ulinzi mkubwa katika nchi hii? (*Makofi*).

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania na Marekani zimekuwa na uhusiano wa muda mrefu. Na katika kupitia uhusiano huo na Tanzania kujulikana kimataifa kutokana na sera zetu ndio maana hata rais wa Marekani amevutiwa kutembelea nchi yetu. (*Makofi*).

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa muda umetutupa mkono. Aah, Mheshimiwa Waziri, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, majibu ya ziada.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ningependa kuongezea majibu yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Rais Bush wa Marekani, pamoja na serikali nzima ya Wamarekani, ilivutiwa na sera yetu nzuri ya uongozi bora, utawala bora, mchakato wa demokrasia na matumizi ya fedha zinazotoka kwa Wafadhili, matumizi mazuri ya fedha hizo katika miradi ya maendeleo. Rais Bush, baada ya kuridhika kwamba katika bara zima la Afrika, nchi ambayo ina *invest in the people*, nchi ambayo inajishughulisha na uhuru wa wananchi wake, nchi ambayo inajali demokrasia, nchi ambayo inathamini utu, akaamua kuichagua nchi hii kuja na tukapata faida kubwa sana na ningependa kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba pesa, shilingi milioni 698, dola za Marekani tulizopata zinaifanya Tanzania kuongoza katika nchi 15 zilizosaidiwa na mpango huu. (*Makofi*)



**Barabara Iendayo Kwenye Kituo cha Utafiti wa Kilimo Naliendele**

**MHE. MOHAMED S. SINANI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Kituo cha Utafiti wa Kilimo kilichopo Naliendele – Mtwara, kina umuhimu mkubwa katika kuboresha kilimo hapa nchini na nchi za jirani hususan kilimo cha korosho lakini kipande kidogo cha barabara inayoelekea kwenye kituo hicho ni mbaya sana:-

Je, ni lini Serikali itaweka lami kwenye kipande cha barabara chenye urefu wa kilometa saba (7) kinachoelekea kituoni hapo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Meshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Meshimiwa Spika, barabara ya Mtwara hadi Naliendele, kilometa 7, ni sehemu ya barabara ya Mkoa wa Mtwara hadi Newala, yenye jumla ya urefu wa kilometa 140. Barabara hii ambayo ni ya changarawe na udongo imekuwa ikifanyiwa matengenezo ya aina mbalimbali ili iweze kupitika wakati wote. (*Makofi*)

Meshimiwa Spika, kuanzia mwaka wa fedha 2004/2005 Serikali kupitia msaada wa Serikali ya Norway, imekuwa ikitenga fedha za kuifanyia ukarabati kwa kiwango cha changarawe kwa awamu barabara hiyo. Hadi sasa jumla ya kilometa 96 zimekwisha karabatiwa kuanzia njiapanda ya uwanja wa ndege hadi kijiji cha Miule, Tandahimba, zikijumuisha kilometa 7 anazozungumzia Mheshimiwa Mbunge, kwa jumla ya gharama ya shilingi bilioni 2.19. Kwa sasa barabara hiyo inapitika vizuri wakati wote.

Meshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa barabara hiyo inakuwa katika hali nzuri na kupitika wakati wote kwa kuitengea fedha za matengenezo kila mwaka. Hali ya fedha itakaporuhusu Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara hiyo kwa kuanzia na kipande hicho cha kilometa 7 hadi Chuo cha Kilimo Naliendele.

**MHE. REYNALD A. MROPE:** Meshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri aliyoyatoa katika swali hili.

Meshimiwa Spika, ningepomba kuuliza. Kwa kuwa, katika eneo la *Mnazi Bay*, Msimbati, hivi sasa kumegunduliwa gesi, kuna fununu za mafuta na kadhalika. Lakini barabara ya kutoka Mtwara mpaka Msimbati, kilometa 40 ni mbaya sana sana.

Je, Waziri anafikiriaje kuweka barabara hii kwa kiwango cha lami ili wawekezaji na watu wengine wanaotaka kuja kuwekeza Mtwara, waweze kupita kwa urahisi katika eneo hili ambalo ni lulu ya Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Meshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, kama ifuatavyo:-

Meshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kila wakati pale ambapo kuna uwekezaji na kuna faida za kiuchumi kwa nchi ambazo zinajitokeza, basi Serikali ama yenyewe kwa kushirikiana na wafadhili au hao Wawekezaji, tuweze kuboresha miundombinu ya kufikia maeneo yale ili kuweza ku-*tap* ule uchumi ambao umetokea pale, kwa mfano uwezekano huo wa gesi na mafuta.

Kwahiyo, barabara hii ya kutoka kati ya Mtwara na Msimbati ni moja ya maeneo haya. Katika Bajeti zetu zijazo tutaendelea kuangalia uwezekano wa kuiboresha barabara hiyo kwa kiwango cha lami kama itakuwa imewezekana kutegemea na fedha za Bajeti. (*Makofi*).

Na. 168

### **Ndege za Shirika la Ndege la Tanzania**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilichukua hatua ya kusitisha Mkataba wa *ATCL* na *SAA* ambao ulikuwa unalitia Taifa hasara kubwa:-

- (a) Je, mpaka sasa shirika jipya la Ndege la Tanzania, *ATCL* lina ndege ngapi?
- (b) Je, kati ya hizo ni ngapi ambazo zimekodishwa au kununuliwa kwa kutaja aina na idadi ya ndege?
- (c)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Meshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa ufafanuzi ufuatao:-

Baada ya kuingia mkataba na *South African Airways*, Shirika la ndege la Tanzania, *Air Tanzania Cooperation (ATC)*, lilibadilishwa jina na kuitwa Kampuni ya Ndege ya Tanzania, yaani *Air Tanzania Company Ltd-ATCL*. Na baada ya kusitisha mkataba na *SAA* shirika letu la Ndege linaendelea kujulikana kama kampuni ya Ndege ya Tanzania, *ATCL*.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi huo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kampuni ya ndege ya Tanzania kwa sasa inamiliki jumla ya ndege sita.

(b) Mheshimiwa Spika, Ndege tatu zinamilikiwa na *ATCL* na ndege tatu zimekodiwa. Ndege zinazomilikiwa na *ATCL* ni ndege moja aina ya *Boeing 737-200* na zingine mbili za aina hiyo zilizokodishwa. Na ndege moja ni ya kwetu katika hizo *Boeing* na mbili zimekodishwa. Na ndege mbili zilizounuliwa za *Dash 8Q300*. Aidha ndege moja ya *Airbus 320-200* na yenyewe imekodishwa na hii inategemea kuwasili siku nne kuanzia leo.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Meshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Meshimiwa Spika, katika vyombo vya habari tumeona kwamba wameelezea *ATCL* imekodisha ndege ya *Airbus* ambayo ni mbovu inahitaji matengenezo makubwa sana. Na inabidi itengenezwe ili iweze kukidhi mahitaji ya hapa nchini.

Swali, ni sababu gani ilipelekea *ATCL* kwenda kukodisha ndege ambayo inahitaji matengenezo makubwa na vilevile ukizingatia ma *pilot* wetu wamezoea *Boeing*, kwa nini walienda kukodisha *Airbus*?

Meshimiwa Spika, swali la pili. Je, katika mkataba wa kukodisha ndege hii. Je, walizingatia taratibu za *Public Procurement Act*?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kulitokea na taarifa kwenye vyombo vya habari ambavyo hasa hasa inatokana na taarifa kwenye *internet* kwamba ndege iliyokodishwa kutoka Elisalvado ilikuwa ndege mbovu, nataka niwahakikishie Bunge hili Tukufu kwamba haya maneno hayakuwa ni kweli kilichotokea na hii ni kawaida ya ndege ya zote unapokodisha ndege inafanyiwa *see check*. *See check* inajumuisha vilevile kwamba ile ndege *stripped off* unaivua kabisa kule kule kuweza kuiweka katika hali ya kuweza kusafirishwa. Na gharama za kufanya hii kazi ni za yule mwenye ndege. Sasa nadhani hawa walipata taarifa hizo na wakaona wakati *see check* inafanyika kule wakachukulia kwamba ni ndege mbovu.

Lakini ni utaratibu tu kwamba ukikodisha ndege huwezi ukachukulia kwamba ni ndege mbovu, lakini utaratibu ni kwamba ukikodisha ndege huwezi ukaja ukaileta nchini kabla ya *see check* kufanyika.

Sasa ukikuta wakati huo ndiyo wame-*stripped off* wanaifanyia yale matengenezo ambayo ni kuiweka katika hali nzuri mtu unaweza ukaanza kusema kwamba ndege ni mbovu. Haikuwa hivyo ilikuwa ni maneno ya ndani. Mengine kwa kweli pale *Air Tanzania* mimi niseme kuna matatizo. Hata umbeya ndani ya shirika lile umo ndiyo maana wengine wameanza kutoa hayo. Mimi nilikuwa mhasibu Mwandamizi *Air*

*Tanzania*, mwaka 1980 hadi 1985, wakati Mheshimiwa Bakari Mwapachu akiwa *General Manager*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo lilikuwa ni shirika lenye heshima ukifanya kazi *Air Tanzania* unaonekana kwamba ni mtu wa heshima. Uwongo uwongo huu na umbeya huu haukuwepo. Sasa hii imeniletea kwa kweli hali hii kuonyesha kwamba hali sio hivyo. Lakini siyo kweli na baada ya hapo baada ya *see check* wenzetu wa TCAA ambao kwa kweli ni *Regulatory Authority* inayoheshimika sana duniani ilikwenda kule na ikathibitisha kwamba ile ndege iko sawa sawa.

Lakini zaidi ya hapo *FAA* ambayo ni mamlaka ya anga kule Marekani ambao wanafahamika vilevile wakatoa *Certificate of Export* baada ya kuona iko sawa sawa.

Kwa hiyo, nilitaka nilihakikishie Bunge hili kwamba ile ndege iko sawa sawa siku nne kuanzia leo itafika na itaweza kuanza kufanya kazi kama kawaida.

Na. 169

### **Ukarabati wa Bwawa la Setched**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA (K.n.y. MHE. DAMAS P. NAKEI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwa na ahadi ya Serikali ya muda mrefu tangu mwaka 2001 ya ukarabati wa Bwawa la Setched katika Kata ya Ufana Wilayani Babati; na kwa kuwa, Serikali imewahi kukumbushwa juu ya ahadi hiyo:-

Je, kwa nini hakuna hatua zozote zinazoonekana kuchukuliwa kuhusu ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Setched lipo katika kijiji cha Setched, Kata ya Ufana Wilaya ya Babati. Bwawa hili, lilikuwa na mita za ujazo 58,800, lilipojengwa mwaka 1954 na kwa sasa limejaa tope na uwezo wake wa kuhifadhi maji umepungua kwa kiasi kikubwa. Inakadiriwa kuwa hivi sasa Bwawa uhifadhi maji wake umepungua kwa kiasi kikubwa.

Inakadiriwa kuwa hivi sasa Bwawa linahifadhi maji kwa kiwango cha asilimia 30 pungufu ya uwezo wake. Hata hivyo, pamoja na hali hiyo, tuta la Bwawa na utoro wa maji bado vipo katika hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ilivyo hivi sasa, ni wazi kuwa kazi ya kukarabati Bwawa la Setched inaweza kugharimu kiasi kikubwa cha fedha kinachokadiriwa kuwa

shilingi bilioni 2.4, ikilinganishwa na shilingi milioni 411 zinazokadiriwa kuhitajika kujenga Bwawa jipya lenye ukubwa huo huo.

Aidha, uondoaji wa tope kwenye Bwawa unaweza hata kuhatarisha usalama wa mitambo ya kufanya kazi. Kwa kutambua hali hii, mwezi Juni, 2006 Halmashauri ya Wilaya ya Babati Vijijini ilianisha maeneo ya kujenga mabwawa mapya na kufanya upimaji katika vijiji mbalimbali ikiwa ni pamoja na kijiji cha Setched.

Aidha, chini ya programu ya maendeleo ya sekta ya maji ambayo inatekelezwa katika wilaya zote kuanzia mwaka wa fedha 2007/2008, Halmashauri za Miji, Manispaa na wilaya hupewa fedha na kuzitumia kulingana na miradi waliyopanga. Utaratibu ni kwamba miradi ya maji inaibuliwa na wananchi na uamuzi wa mradi upi uanze kutekelezwa na upi ufuata, upo mikononi mwa Halmashauri ya Wilaya husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, gharama ya kukarabati Bwawa la Setched kwa kutoa udongo ni kubwa kuliko gharama ya kujenga Bwawa jipya, Wizara yangu sasa kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kupitia mradi wa *PADEP* inafanya uchunguzi wa kujenga Bwawa jipya baada ya kukarabati lile la Setched.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa pia sababu zinazowafanya wafugaji kuhama hama ni pamoja na kutafuta maji kwa ajili ya mifugo yao na kwa kuwa ni azma ya Serikali kuboresha sekta ya ufugaji nchini. Ni kwa nini basi Serikali isichukue hatua na mikakati ya makusudi ili kukarabati au hata kuchimba mabwawa mapya ili kuruhusu wafugaji wasihame hame na hivyo sambamba na kuboresha ufugaji katika sekta hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango wa kujenga mabwawa chini ya programu yetu ya kuendeleza sekta ya maji na programu ile kuendeleza sekta ya kilimo. Programu zote hizo zinao utaratibu wa kujenga mabwawa jambo la kusisitiza tu katika hili ni kwamba mabwawa haya ni ya ghali sana yanahitaji gharama kubwa na yanachukuwa eneo kubwa maji yale yanapozagaa kila mahali.

Kwa hivyo tunachokifanya sasa ni kuangalia mabwawa yanayojengwa isiwe kwamba kila sekta ijenge Bwawa lake mifugo wajege la kwao, kilimo wajege la kwao na wengine wajenge mabwawa yao kwa sababu haitawezekana hata ardhi itakuwa finyu.

Kwa hiyo, tunachofanya sasa ni kutumia intergrated development approach kusudi bwawa likijengwa liweze kushirikisha matumizi yote ya maji ya kunywa, kilimo, ufugaji na matumizi mengine. Hilo liko katika utaratibu wa Serikali.

Na. 170

### **Tatizo la Maji – Kijiji cha Ifunda**

**MHE. LEDIANA MAFURU MNG'ONG'O** aliuliza:-

Kwa kuwa, tatizo la maji katika kijiji cha Ifunda wilayani Iringa limekuwa Sugu na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wanawake, watoto na hata wanafunzi wa sekondari zilizoko kwenye kijiji hicho:-

Je, ni lini Serikali itaboresha hali ya upatikanaji maji ili kuwaondolea usumbufu mkubwa wanaopata wanawake na watoto?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o, Mbunge wa Viti maalumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kijiji cha Ifunda kina wakazi 4,944 kwa takwimu za sensa ya mwaka 2002, inawezekana sasa wameongezeka. Mahitaji ya maji kwa ajili ya kijiji cha Ifunda ni mita za ujazo 1,036 kwa siku. Mwaka 1992, kijiji hiki kilipata huduma ya maji ya visima vifupi 26 vyenye pampu za mkono kupitia msaada wa fedha kutoka Serikali ya Denmark. Mwaka 2006, pampu za mkono 5 kati ya 26 hapo kijijini zilibiwa. Aidha, visima 20 kati ya visima 21 vilivyobaki vilikauka. Hadi hivi sasa ni kisima kimoja tu kina maji na ndicho kinaendelea kufanya kazi. Visima vilivyobaki bado havitoi maji.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa Vijijini ililiona tatizo hilo la ukosefu wa maji katika kijiji cha Ifunda na kuanza kulishughulikia kama ifuatavyo:-

Mwaka 2006/2007 Wizara yangu ilitenga shilingi milioni 10 kwa ajili ya kununua pampu ambazo zilifungwa kwenye visima vine. Kwa bahati mbaya visima hivyo navyo vimekauka. Katika mwaka 2007/2008, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ilitengewa shilingi milioni 76 kupitia Ruzuku ya Maendeleo kwa Serikali za mitaa (*Local Government Capital Development Grant*) kwa ajili ya huduma za maji.

Kwa kutumia fedha hizo, Halmashauri ilibuni mradi kwa ajili ya kijiji cha Ifunda utakaotumia chanzo cha maji cha chemchem ya Kalenga kapya iliyoko Ifunda. Mradi utatumia mitambo ya umeme yenye uwezo wa kutoa maji mita za ujazo 1,350 kwa siku. Hivi sasa Halmashauri ya Wilaya inaendelea na mchakato wa kumpata Mkandarasi wa kujenga mradi huu na kazi inatarajiwa kuanza mwezi wa tano 2008. Mradi huu utatekelezwa kwa awamu mbili kama ifuatavyo:-

Awamu ya kwanza itahusisha ujenzi wa “*intake*” na nyumba ya mashine na kulaza bomba kuu lenye urefu wa kilomita 3.5. Utekelezaji wa awamu ya kwanza unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Juni, 2008.

Awamu ya pili ya mradi imependekezwa kutekelezwa kwa gharama ya shilingi milioni 85.5 katika mwaka 2008/2009. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na ujenzi wa tanki

la maji lenye meta za ujazo 100, kulaza mabomba ya kusambaza maji, kujenga vituo 20 vya kuchotea maji, kununua na kufunga mitambo ya kusukuma maji.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Halmashauri za wilaya ndio watekelezaji wa miradi yote inayoibuliwa na wananchi kwenye wilaya zao. Hivyo, ninamshauri Mheshimiwa Mbunge aendelee kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa Vijijini ili kuhakikisha kuwa mradi wa maji katika kijiji cha Ifunda unapewa kipaumbele kwenye mipango ya Halmashauri na kutekelezwa.

Aidha, inasikitisha pia kuona kwamba pamoja na juhudi za Serikali kuwapatia maji wananchi wake, bado suala la wizi wa pampu, mabomba na hata injini za mitambo ya kusukuma maji linaendelea hasa kutokana na biashara ya vyuma chakavu. Wizi huu unarudisha maendeleo nyuma kwa kuwa, tunafanya kazi ya kurudia. Naishauri Halmashauri ya Wilaya ya Iringa na Halmashauri nyingine pamoja na viongozi wote katika ngazi za Kijiji, Kata na Tarafa kuweka utaratibu wa ulinzi katika miradi ya maji.

**MHE. LEDIANA MAFURU MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake ya kina na mazuri na yenye kuridhisha na kutia matumaini. Naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa nimezungumzia taasisi zikiwemo na shule, na shule hizi ziko sehemu nyingi hazina maji.

Je, Serikali itakuwa tayari kukubaliana nami sasa kwamba ni wakati muafaka shule zinapojengwa zijegewe pia visima vya maji ambayo yanaweza kuvunwa wakati wa mvua kwa sababu mvua inakuwa ni nyingi, lakini maji hayo hayatumiki na watoto wanahangaika?

Je, Serikali itakuwa tayari kujenga visima virefu vya chini ambavyo vitatumika kuvuna maji ya mvua?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimsahihishe kidogo tu kwamba visima virefu si teknolojia ya uvunaji maji katika utaratibu wetu wa kitaalam. Lakini ni jambo ambalo ni muhimu. Labda niseme tu kwamba katika programu yetu ya kuendeleza sekta ya maji mtaalam ambaye ataanza kazi hivi karibuni mwezi wa Julai, mojawapo ya hadidu za rejea alizopata ni kuangalia taasisi kama anazosema Mheshimiwa Mng'ong'o, Zahanati, hospitali au vituo vya afya ambavyo vipo huko vijijini. Kitakachofanyika ni kuangalia uwezekano wa kuvuna maji ya mvua kwa kutumia paa za nyumba na kuwajengea matanki ya bei nafuu, ili hatimaye wananchi na jamii inayozunguka iweze kuiga teknolojia hii. Hata hivyo, nataka nikubaliane na Mheshimiwa Mng'ong'o kwamba kuchimba visima kwa ajili ya maji ya kunywa pamoja na njia zingine ni muhimu sana hususan kwa taasisi zetu hizi ambazo zinaanzishwa kwa *speed* kubwa sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali mawili yaliyosalia pengine yatapata nafasi kesho, sasa ni wakati wa matangazo kwa heshima na taadhima napenda tutambue uwepo pale *Speakers Gallery* Waheshimiwa Wabunge kutoka Bunge la Afrika Mashariki kama ifuatavyo na nitawaita mmoja mmoja ili wasimame tuwatambue. Wa kwanza Dr.

Didas Masamburi, Mheshimiwa Kate Kamba, Mheshimiwa Dr. Fotunatus Masha, Mheshimiwa Abdallah Mwinyi, Mheshimiwa Dr. Amani Walid Kaborou na Mheshimiwa Dr. George Nangale karibuni sana Waheshimiwa tunafuatilia kwa karibu kazi zenu mnazozifanya kwa niaba ya nchi yetu tunawatakia afya njema na muendeleo kuiwakilisha vizuri nchi yetu kwenye Bunge la Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, anao wageni wake wa Chama kinaitwa *SOBER* Tanzania, *SOBER* ni kwa kiingereza *SOBER* na kama unavyoweza kutabili hapo *NGO* hiyo inashughulikia kupiga vita matumizi ya dawa za kulevya na matumizi yaliyokithiri ya pombe, ndiyo kazi ya *SOBER* Tanzania.

Sasa waliokuja hapa ambao wanatoka chama cha kimataifa hicho ni Bwana Guna Lunstrom, mwakilishi wa Afrika Mashariki, Bwana Masudi Mvuma Afisa mipango kwa Afrika Mashariki, Bwana Adam Ngimba, Katibu Mkuu nadhani kwa Tanzania, Bibi Judith Fue Makamu Mwenyekiti Tanzania na Bibi Prisila Manyinda mjumbe wa bodi ya kitaifa. (*Makofi*)

Ameniomba Mheshimiwa Paul niwasihii Waheshimiwa Wabunge mjiunge na tawi la Dodoma la chama hiki kizuri tu kinachopambana na madawa ya kulevya na unywaji wa pombe uliokithiri. Wageni wengine kwa leo ni wa Mheshimiwa Aggrey Mwanri kutoka Wilaya ya Siha, ni Bwana Daniel Sandewa, na Bwana Lalashoi Kweka huyu sio Bwana huyu ni Mheshimiwa kumbe ndiyo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, Bwana Daniel tunaomba usimame tena, nilikuika Bwana lakini wewe ni Mheshimiwa, na Bwana Kweka huyu ni Bwana maana yake ni Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Lucy Mayenga, ni mmoja tu mgeni wake ni Eng. Bura Ngega ambaye ni mshauri wa wilaya yaani *grasker* nchi Marekani, sijui ni Mtanzania huyu anaishi Marekani sasa haikufafanuliwa hapa ni Mtanzania kwa sababu Mheshimiwa Lucy Mayenga anasema huyu ni mmoja wa wapambe wake mashuhuri katika jumuiya ya vijana ya CCM sasa sijui atarudi maana yake vijana wa sikuhizi kwa kuzamia loh! (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Shaly Raymond kama ifuatavyo: Ndugu Kundaeli Masawe, Katibu Msaidizi wa Moshi Mjini karibu sana na Ndugu Lucy Isidori, Katibu wa Jumuiya ya Wazazi Moshi Mjini karibu sana. (*Makofi*)

Wapo pia wanachuo 30 na viongozi wao wakiwa na walimu watatu wa Chuo Kikuu wa St. John University, Chuo cha Anglicana Tanzania ningeomba tuwatambue wao wasimame naomba niwatambue maalum walimu wao Neema Mwamoto, Veronica Nyanda na Gladness George, karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo pia wajumbe Muheda ambao ni wageni wa Mheshimiwa Mbunge wa Mvomero ambao wanatoka hawa ni wanafunzi wa mwaka wa tatu kutoka chuo kikuu cha Mzumbe, Mheshimiwa Murady ameomba watambuliwe karibuni sana. (*Makofi*)



Halafu wapo wageni wa Mheshimiwa Mporogomyi ambao ni wanachuo wa Chuo kikuu cha Dodoma ambao wanatoka mkoa wa Kigoma wako 14 ningomba wasimame pale walipo karibu sana. (*Makofi*)

Vikao Mheshimiwa Wilbrod Peter Slaa, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa ameniomba nitangaze kwamba leo kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo ukumbi Na. 428 saa tano asubuhi, kwa hiyo Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa ukumbi na 428.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii anaomba wajumbe wote wa Kamati hiyo ya Maendeleo ya Jamii wakutane saa saba mchana ukumbi na 227 kwa mazungumzo na viongozi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto. Hiki ni kikao cha pamoja kwa hiyo viongozi wa Wizara watakutana na Kamati ya Maendeleo ya Jamii saa saba mchana ukumbi Na. 227.

Mheshimiwa Abisalam Issa Khatib, Mwenyekiti Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara, anaomba wajumbe wote wa Kamati ya Viwanda na Biashara, mkutane ukumbi namba 133 gorofa ya kwanza jengo la utawala, saa tano asubuhi hii.

Mheshimiwa Abdallah Kigoda ameniomba nitangaze kwamba wajumbe wa Kamati zifuatazo *PAC, POC, LAAC* na Kamati ya Fedha na Uchumi leo watakuwa na semina ya pamoja na mradi wa *Depening Democracy*. Semina hii itahusu uchambuzi wa Miswada *Bills scrutiny* na itafanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa saba hadi saa kumi na moja jioni. Kwa hiyo wajumbe wa *PAC, POC, LAAC* na Kamati ya Fedha na Uchumi kwa pamoja semina kuhusu *depening democracy* ambayo itazingatia *bills scrutiny* itafanyika leo saa saba ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Lucy Mayenga ameomba yeye ni Katibu wa Wabunge wa Mkoa wa Shinyanga, Wabunge wote wa Mkoa wa Shinyanga mkutane leo saa saba mchana katika ukumbi 430 naona ukumbi 432 lakini umeshachukuliwa kwa hiyo nadhani mkikutana pale nje mtaweza kupanga ukumbi ambao utafaa, Wabunge wote wa Mkoa wa Shinyanga saa saba mchana.

Waheshimiwa Wabunge huo ndiyo mwisho wa matangazo. Sasa, kabla sijamwita Katibu atuelekeze shughuli zinazofuata. Jana Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, wakati shughuli zikiendelea na mara baada ya tangazo lililotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi alisimama na kuomba kwamba taarifa hiyo ijadiliwe. Mwenyekiti Mheshimiwa Mhagama alimwomba kwamba mwongozo wa Spika utatoka baadaye ili waendeleo na shughuli. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa jana alitumia Kanuni ya 2 kwa sababu lililotokea jana Kanuni ya 2 ndiyo ile inayomruhusu Spika kulipangia utaratibu jambo ambalo hadi wakati ule lilikuwa halina utaratibu bayana ndani ya Kanuni zetu.

Lililotukuta ni hivi Mheshimiwa Waziri au tuseme Serikali ilikuwa inataka kutoa taarifa kuhusu mgomo na vurugu zilizokuwa zikiendelea pale Chuo Kikuu cha Dar es

Salaam, *Mlimani Campus*. Lakini ilikuwa taarifa hiyo itolewe tu ili tujue sasa tumeona kuna mapungufu katika Kanuni zetu taarifa ya jambo la dharura ambalo Serikali inalitaka tu kulitoa bila kuruhusu mjadala wowote haikupangwa katika Kanuni zetu. Tutarekebisha kwa siku za usoni. Kwa hiyo, ndiyo maana kwa uhakika na usahihi kabisa Mwenyekiti Jenista aliona ahairishe tupate ushauriano lakini alipitia Kanuni iliyo sahihi. (*Makofi*)

Kwa hiyo taarifa iliyotolewa jana ni aina ya taarifa ambayo haihitaji mjadala ni kama vile mathalani ukitoa nchi tumevamiwa ama yametokea maafa mengine makubwa kabisa ya ghafula na wajibu wa Serikali ni kulieleza Bunge, lipo palepale. Kwa hiyo, tuwawezeshe Serikali wakati hadi wakati kuweza kutoa taarifa za namna hiyo.

Kwa hiyo tutazingatia mabadiliko hayo, na usahihi wa uamuzi wa Mheshimiwa Jenista unajitokeza pale kwamba leo asubuhi wale vijana wamepelekwa mahakamani. Kwa hiyo, sasa kwa vyovyote vile tusingeweza hata kuwa na mjadala kwa sababu ni suala sasa liko mahakamani. Huo ndiyo mwongozo nautoa tutaendelea kwa wakati huu ambao hatujabadili Kanuni, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali mkiwa na jambo la dharura ambalo mnahitaji kulitoa na wala halihitaji mjadala basi kwa mwongozo mwarifu Spika au *presiding officer* na mtaweza kutoa hiyo taarifa ili kupitia Bunge na Wabunge wenyewe nchi ijue nini kinaendelea.

**MHE. ANNA MARGARETH ABDALLAH:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Kanuni?

**MHE. ANNA MARGARETH ABDALLAH:** Natumia Kanuni ya 68 sehemu ya 7. Leo asubuhi tulipokuwa tunaingia wakati tumegawiwa karatasi orodha ya shughuli za leo tumegawiwa pia taarifa fupi ya utendaji ya Tanzania *International Container Terminal Services*. Katika *Order Paper* hii kuna hoja binafsi ya Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi. Sasa mimi nilitaka tu kufahamu kwamba je taarifa inakusudia kujibu hayo atakayosema Mheshimiwa Zambi. Taarifa hii inakusudia hasa nini na humu ndani kuna pia majadiliano kati ya *TICTS* na Kamati ya Miundombinu, yako humu.

Sasa huyu aliyegawa hii ni ofisi yako na maana yake ni taarifa tu ya utendaji sasa sina hakika inahusiana vipi na hii hoja binafsi ya Mheshimiwa Zambi wala aliyeleta hii hatujui ni nani pamoja na tu na kwamba karatasi hii inataja hiyo kampuni sijui ni kampuni au shirika hizo *services*. Kwa hiyo, mimi nilitaka kujua hasa kwanini limetokea wakati huyu Mheshimiwa Zambi anataka kusema ni utendaji usioridhisha na hawa wanatoa taarifa yao ndiyo sahihi. Utaratibu sahihi namna hii je, kama ndiyo sahihi mbona *RITES* hawakuleta taarifa yao. Ningependa tu kupata mwongozo wako juu ya jambo hili. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana nakushukuru sana Mheshimiwa Anna Abdallah kwa hilo taarifa mimi nilizozipata na hadi ikafikia kwamba taarifa hiyo ya *TICTS* ikasambazwa ni

kwamba waraka huo ndiyo huo huo ambao ulijadiliwa kwenye Kamati ya Miundombinu. Uliwasilishwa kwenye Kamati ya Miundombinu kuonyesha namna *TICTS* ambavyo imekuwa ikifanya kazi. Ilipoarifiwa na Sekretarieti kwamba wahusika wa *TICTS* walisikilizwa na Kamati ya Miundombinu na kuwasilisha taarifa hiyo hiyo, niliruhusu kma ni hivyo basi, kwa sababu wana Kamati wamekwishayaona si vibaya kwenye mjadala taarifa hiyo ikaweza kugawiwa. Ni kwa nia njema tu, kwamba Kamati ya Miundombinu imeliona hilo na nadhani itarutubisha mjadala kama hatuwanyimi Waheshimiwa Wabunge taarifa nyingine za upande wa pili. Mimi nadhani ndiyo njia nzuri ya kuweza kuja kupata ukweli wa suala hilo. (*Makofi*)

### **HOJA BINAFSI ZA WABUNGE**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge leo tuna hoja binafsi nne. Kwa sababu tu ya muda umefinywa, kwa kawaida shughuli za hoja binafsi au hata Miswada binafsi huwa zinapewa siku mbili. Lakini sasa kama mnavyojua kesho kutwa ni sikukuu ya Muungano na viongozi wengi itawabidi kusafiri kesho kwa ajili ya siku hiyo muhimu. Kwa hiyo, tulibakiza siku moja na nusu tu. (*Makofi*)

Sasa, mimi napendekeza kwamba tujitahidi kwenda hoja moja baada ya nyingine. Watoa hoja wazungumze kwa kifupi kwa sababu hoja zenyewe zimeshagawiwa na si ndefu sana. Nitawaita wachangiaji na kwa hili, ninaomba kwamba hakuna haja ya kurudiarudia, halafu tutaona tunavyokwenda. Utaratibu utakuwa ni kwamba, nitamuita Mtoa Hoja, atatoa hoja yake, wale ambao watakuwa wamekwishaniomba kuchangia hapa, nitawaita wachache lakini ni dhahiri kabisa kwamba ili tuweze kuzifikia hoja zote, haitawezekana wote walioomba kwa mfano kwenye hoja ya Mheshimiwa Mzindakaya kuhusu vitalu vya uwindaji ambayo ndiyo tunaanza nayo, wapo zaidi ya 10 kuchangia. Sasa wakiongea wote hao ndiyo kusema tutabaki na hoja hiyo hiyo tu kwa asubuhi nzima. Kwa hiyo, mtaniwia radhi, itanibidi nikiona mambo kama yanajirudiarudia, tuachie hapo ili tufikie hitimisho la hoja hiyo. Nadhani hili tunaafikiana, vinginevyo tutashughulikia hoja moja au mbili halafu basi. Kwa hiyo, tutajaribu kwenda kwa utaratibu huo.

Halafu, la pili ni kwamba katika ule mpangilio wa hoja, inayoanza ni hoja ya Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, inayofuata ni ya Mheshimiwa Said Amour Arfi, ya *RITES*, halafu inafuata ya *TICTS* na mwisho ya Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro ambayo ilikuwa bado inafanyiwa marekebisho, Katibu ameniambia, kwa hiyo sasa yenyewe ndiyo itakuwa ya mwisho, ya uuzwaji wa nyumba za Serikali.

Kwa hiyo sasa Katibu tuendeleo na shughuli inayofuata.

### **HOJA BINAFSI**

#### **UGAWAJI WA VITALU VYA UWINDAJI NA BEI ZAKE AMBAVYO MUDA WAKE KISHERIA UNAISHAI MWAKA 2009**

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninapenda kukushukuru wewe mwenyewe binafsi na uongozi kwa ujumla, kwa kunikubalia ili niweze kuleta hoja yangu hii.

Mheshimiwa Spika, naileta hoja hii chini ya Kanuni ya 51(1), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu hoja binafsi kuhusu ugawaji vitalu vya uwandaji wa kitalii na bei zake ambavyo muda wake kisheria utaisha mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, maudhui ya hoja hii, ina mambo makubwa mawili. La kwanza, mapendekezo yanayowasilishwa hapa mbele ya Bunge lako Tukufu yanaisaidia Serikali kuongeza mapato. Pili, inahusu uwezesaji wa wananchi katika sekta hii ya uwindaji.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa sekta hii ambayo ni muhimu sana, ingeweza kweli kulipatia Taifa letu mapato ya kutosha na kwa utafiti tulioufanya, inaonekana kwamba, tunapoteza zaidi ya dola milioni 60 kwa mwaka sawa na hela za Kitanzania bilioni 76.8 kwa mwaka ambapo kama mapendekezo yanayowasilishwa hapa mbele ya Bunge lako Tukufu yakikubaliwa, uwezekano wa Tanzania kupata zaidi ya dola milioni 80 upo, tukizingatia sekta yote kwa maana ya uwindaji pamoja na upigaji picha .

Mheshimiwa Spika, katika Kiambatanisho A, yapo mambo matatu. Kwanza, kuna mambo yenyewe halafu kuna utafiti yaani *findings* na mapendekezo. Mambo makubwa yaliyo katika hoja hii kwenye kiambatanisho hiki ni mfumo au muundo wake kwa sasa, usimamizi wa sekta hii kisheria, umiliki wa vitabu, utaratibu unaotumika kugawa vitalu, upangaji wa bei za vitalu, uwiano na usawa katika kugawa vitalu, uuzaji wa vitalu yaani *marketing*, mchango wa sekta hii kwa uchumi wa nchi yaani *GDP*, ada za vitalu na nyara zake pamoja na uwezesaji wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, labda nianze na jambo moja la kwanza. Sekta hii kwa kiwango kikubwa inamilikiwa zaidi na wawindaji wageni. Katika ule ukurasa wa nne wa kiambatanisho, nimewafanyia uchambuzi kuonyesha vitalu viko vingapi, wamiliki wako wangapi na kuonyesha jinsi idadi ya wamiliki kutoka nje ilivyo kubwa. Kwa mfano, vitalu vilivyopo kwa sasa ni 149, makampuni ya wageni yapo 12 na yanamiliki vitalu 17 sawa na vitalu vitano kwa kila kampuni moja. Wazalendo wana kampuni 29 zinamiliki vitalu 61 sawa na vitalu viwili kwa kila kampuni. Sasa hii haileti uwiano mzuri.

Mheshimiwa Spika, labda pia nieleze kwamba, uchunguzi tulioufanya, unaonyesha vilevile kwamba baadhi ya makampuni binafsi na mengi ni ya wageni, yanamiliki zaidi ya vitalu 15. Sera yetu inatoa nafasi ya kuweza kuwa na kampuni za namna hii kwa asilimia 51 kwa Mtanzania au kwa asilimia 49 kwa mgeni. Hapa nyumbani tumeweka sera nzuri ambazo zinawezesha na zinawapa nafasi Watanzania kushiriki katika mambo ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, labda niseme vilevile kwamba mimi nilikuwa kwenye Kamati ya Serikali iliyoteuliwa kusaidia mawazo na tulipeleka taarifa lakini imekuwa vigumu sana kwa taarifa yetu kutekelezwa hata ya Mheshimiwa Philip S. Marmo, zinakuwa ngumu kutekelezwa kwa sababu sekta hii, wawindaji binafsi na hasa wanaotoka nje, wanaleta usumbufu mkubwa sana na mara nyingi imekuwa vigumu mno kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, labda niseme kwamba, mimi naleta hoja hii wakati Waziri wa Wizara hii na Naibu wake ni wapya. Kwa hiyo, hoja hii ikikubaliwa, tutakuwa tumewasaidia kuondoa usumbufu unaotokea katika Wizara ile wa mgawanyiko wa maslahi kwa sababu kuna mgawanyiko mkubwa sana wa maslahi.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine mambo mengine ni ya aibu, kuna wakati wawindaji wakubwa wa kigeni wamekuwa wakiwatisha watendaji katika Wizara ambao ni waaminifu. Kwa mfano, kila Waziri aliyeondolewa katika Wizara ile, wageni wamejigamba kwamba wao ndiyo wamemtoa na mara nyingine huenda hata kumtisha Katibu Mkuu wa sasa kwamba asipofuata wanavyotaka, watahakikisha ameondoka. Sasa hatuwezi kuwa na wageni wanaotisha wananchi katika nchi yao, hili si jambo zuri.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mmoja. Sisi tulikwenda Zimbabwe tukakuta wenzetu wa Zimbabwe na hata South Afrika wao haiwezekani mgeni kupewa kitalu au kumiliki kitalu. Wageni ni wawindaji tu, wanakuja kuwinda na siyo kumiliki vitalu. Sisi haya mapendekezo ninayowasilisha hayasemi tusiwe na wageni, yanasema tuwe na wageni lakini kwa ubia, wasimiliki peke yao vitalu yaani kuwe na ubia kati yao na Watanzania.

Mheshimiwa Spika, juzi nilikuwa Arabuni kwa mfano kule Dubai, nashangaa wakubwa wanatupigia kelele sana tunapoanza kuzungumza habari ya kusaidia kutekeleza sera zetu za uwezesaji wa uzalendo, kule United Bahrain Emirate, hakuna mwekezaji yeyote anayeweza kuwekeza bila kuwa na mtu wa nchi ile. Kuna maeneo mengine nimekwenda kuyatembelea, kujenga nyumba tu, Sheria imewekwa kwamba mgeni hawezi kupewa kiwanja kwa ajili ya kujenga nyumba katika eneo hilo, anayejenga ni mwananchi na huyu mwananchi kwa sababu hana uwezo, ziko benki zinatoa mikopo kwa ajili ya kujenga, wageni wanaotoka nje, wanaokuja kufanya kazi Arabuni, wanapanga katika nyumba yake kwa fedha nyingi, niliona nilieleze hili.

Mheshimiwa Spika, vilevile wawindishaji wa Kitaliano, *Professional Hunters (PH)*, wanaofanya kazi hii ya uwindaji hapa Tanzania pia ni wageni, wenye makampuni haya kwa kuwa ni wageni, hawataki *PH* wa Tanzania kufanya kazi hiyo ambapo wenzetu wa Zimbabwe wanajitegemea kwa *PH*. Kwa hiyo, yapo mapendekezo katika ukurasa wa 13 wa kuiomba Serikali itengeneze *program* maalumu ya kuweza kufundisha hawa watu kuhusu *PH*.

Mheshimiwa Spika, vilevile ningependa niseme na Wabunge wote ni mashahidi, mwaka huu wakati wa bajeti ya Serikali, Waziri wetu wa Maliasili wakati huo Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, alikuwa hapa ndani na Wabunge wote tulipanga mstari kumpongeza baada ya kuleta zile bei.

Mheshimiwa Spika, lakini ninapenda niwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali kutokana na wawindaji wanaomiliki vitalu vingi kufanya sekta hii ni kama mali yao, mwaka jana Serikali haikutekeleza vile ilivyopitisha Bungeni kwa kutoza 50,000 kwa kila kitalu na badala yake wamepunguza na hata hiyo iliyopunguzwa haijulikani ni kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu Serikali imeweka kiwango cha kulipia kitalu kimoja dola 27,000, ndiyo itatozwa mwaka huu, mimi sina tatizo na hiyo kwa sababu lengo la hoja hii ni kwa siku zijazo kwamba hayo yanayopendekezwa hapa yatekelezwe katika kipindi cha uwindaji kuisha muda wake mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, labda nieleze kidogo jambo ambalo ni vizuri mkaliona. Vitalu hivi vinazidiana ukubwa kwa mfano kuna vitalu ambavyo nimewafanyia hesabu Waheshimiwa Wabunge, katika kile kiambatanisho, kuna GN ya Serikali, mtaiona pale katika kiambatanisho cha kwanza. Ie GN ya Serikali, namba 159 inaonyesha vitalu vimepangwa kwa *grade* yaani *grade A* na *grade B*. *Grade A* ni vitalu ambavyo viko katika maeneo *prime* ambayo vina wanyama wengi kwa mfano *Selou* na maeneo mengine ya *reserve*. Kuna vitalu ambavyo vina ukubwa wa kilomita 367, hivi viliwekwa kiwango cha 50,000 lakini kuna vitalu katika eneo hilohilo la *Selou* ambavyo vina ukubwa wa Sq. Km 2000, 3000 mpaka 4000 lakini vyote vinatozwa bei sawa, sasa hii inafanya Serikali tupoteze mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika mapendekezo haya ambayo nayawasilisha mbele yako, nimeona pia nisije tu nikasema Serikali mkagawe vitalu, nimeisaidia Serikali kupipunguza kwa *criteria* kila kitalu kuwa na kilomita 800 ambazo zinatajwa katika kile kiambatanisho cha Serikali yenyewe ambapo wanasema kitalu kimoja *on average* kiwe na *area* ya ukubwa wa kilomita 800. Kwa hiyo, ukichukua vitalu vikubwa katika A na B ukavigawa kwa msingi wa kilomita 800, vimepatikana vitalu vipya 87 ambavyo kwa wingi wake vinaisaidia Serikali kuongeza pato la Taifa. Hiyo, mtaiona katika mapendekezo katika ukurasa wa 6.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei, Serikali imeweka bei ya dola 27,000. Mimi nilikuwa kwenye Kamati iliyoundwa na Wizara, tulitembea South Africa, tulikwenda Botswana na pia Mozambique, kote huko tulikwenda kujifunza jinsi wenzetu wanavyofanya. Sasa ubishi wa bei Waheshimiwa Wabunge, mimi nimeleta, mtaona pale kwenye kiambatanisho kinachonyesha mifano ya nchi za wenzetu kwa mfano ule ukurasa wa 8, nimeweka mfano wa bei ambazo wenzetu wanatoza ili kuondoa ubishi.

Kwa mfano, tukianza na Zimbabwe. Zimbabwe kitalu kimoja kinatozwa ada ya dola milioni 2 kwa miaka mitano ambayo ukiizidisha au ukiigawa utaona kwamba ni sawasawa na dola 400,000 kwa mwaka mmoja sisi tunaweza dola 27,000. Tofauti ni kubwa mno, tena kubwa mno.

Botswana kwa mfano wao wana namna tatu. Ya kwanza, ni kwamba mtu akitaka kitalu ni lazima aombe na akiomba kwa sababu wanavitoa kwa *tender*, anatoa dola 8,335

ambazo ni *non refundable* yaani harudishiwi, akishatoa ametoa. Kwa hiyo, baada ya hapo kitalu kile watampa kwa miaka mitano, mitano ikifika miaka 15 mwisho. Kwa hiyo, kwa mwaka mmoja kwa kipindi chote cha miaka mitano atalipa dola milioni 3,333,305 sawa na dola 222,777 kwa mwaka, lakini sisi kwetu ni dola 27, sasa hii haisaidii.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mwingine, mtaona katika ukurasa ule pale, mwaka jana, Zimbabwe wao wananadi vitalu, wakinadi kitalu kimoja kwa dola milioni 2 ambayo ni sawasawa na 400,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika hoja hii, mapendekezo ni kuwa vitalu hivi vipangwe kwa *grade* kwa sababu kitalu kilicho *Selou* na kitalu kilicho kwenye eneo lingine ambalo si sawa na *Selou* vinatozwa sawa ambapo hii haiisaidii Serikali kupata mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yanayowasilishwa katika hoja hii ni kwamba *Selou Game Reserve* ambayo ndiyo *reserve* yenye wanyama wengi na wa aina nyingi na ya kwanza duniani, napendekeza kwamba itangazwe kuwa ni eneo maalum la uwindaji kitaifa na watu waingie pale kwa kushindania yaani kwa *tender*. Hii itaiwezesha Serikali kupata zaidi ya 400,000 kwa kitalu kimoja, inawezekana. Vitalu vyote ambavyo viko katika *Game Reserve* na vinapakana na hifadhi za Taifa, vilevile ziwekwe katika kiwango kisichozidi 400,000 dola. Halafu vile vitalu ambavyo ni *open areas* na havina wanyama wengi, napendekeza kwamba viwe ndiyo vya dola 27,000 kwa mwaka. Hiyo itaisaidia Serikali kuweza kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, *GDP* ya wenzetu kule Zimbabwe na Botswana katika sekta hii ya uwindaji, ukichukua maana ya uwindaji pamoja na kupiga picha, wamefikia asilimia 20 lakini sisi tupo asilimia 7 na 10 lakini kwa Tanzania sisi tuna vitalu vingi na maeneo mazuri kuliko hizo nchi zote za jirani.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo tumeliona katika utafiti huu ni kuwa Serikali tunapata pesa kutokana na *trophies* na vitalu, lakini hatupati fedha zenyewe za kigeni kutokana na uwindaji, kwa nini? Wawindishaji wote hao ambao wanamiliki vitalu pamoja na wageni, wana akaunti zao nje ya Tanzania. Kwa hiyo, ikifika wakati wa kutangaza safari, wanawalipia kwenye akaunti zao hukohuko nje, hela haziingii Tanzania, sisi tunapokea vipande kama shanga, mtu anakuja gharama zote ambazo watalii wangelipia hapa wanawalipa kwa Tshs. kupitia kwenye akaunti zao *local* hapa. Kwa hiyo, biashara kwa maana ya Serikali kupata fedha za kigeni kutokana na sekta hii, hatupati ambapo wenzetu Zimbabwe na Botswana wameshirikisha Benki Kuu yao na TRA, wawindaji wote ni *registered*.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tutakapokuwa tumeshaaza lakini tutakapokuwa tunafanya zaidi biashara yetu ya kuuza nyama nje, mimi sikufungua akaunti nje, iko hapahapa, *foreign* akaunti yangu iko hapahapa, ya dola, siku hizi tunaruhusiwa, napendekeza kwa kuwa Serikali haizuii mtu kuwa na akaunti yake ya dola, zije hapa

Tanzania, kwa nini zinakwenda nje? Hii inasababisha hasara kwa Serikali kwa sababu inakosa mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ulituomba tufupishe muda, ingawa Waheshimiwa Wabunge mmechelewa kupata maelezo ya hoja hii, nataka tu niseme kitu kimoja kikubwa kwamba mapendekezo yote yanayoletwa hapa na nikiwa Mbunge wa CCM, ninafurahi kuwajulisha kwamba Wizara inayohusika tumekuwa karibu sana, tunashirikiana, sikutaka jambo hili lije bila wao kujua hoja hii inataka nini.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ninapenda kusema kwamba baadhi ya mapendekezo hapa nimeona bora yaje kwa hoja hii kwa sababu yalishapelekwa Wizarani lakini kutokana na watu wachache kung'ang'ania maslahi yao hawatekelezi maamuzi ya Serikali, hawatekelezi kwa sababu ya maslahi binafsi na hii sekta ina matatizo makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano mmoja mtaona kwenye kile kiambatanisho, wanasema *consensus agreement*, hii kitu imekuwa inatumiwa na wawindaji wa nje, wamejiwekea mle ndani kwamba *minimum blocks* za kupewa kampuni moja ziwe nne, katika pendekezo hili nasema *maximum* zisizidi tatu, mtu asipewe zaidi ya *blocks* tatu, ndiyo kiwe kiwango cha mwisho.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo sasa naomba nisome Azimio kama ifuatavyo:-

**KWA KUWA** inafahamika kuwa, wamiliki wa vitalu vya uwindaji siyo wawekezaji bali ni wavunaji wa maliasili ya wanyamapori ambayo ni zawadi ya Mwenyezi Mungu kwa Tanzania na kwamba Sekta hii ya maliasili ya wanyamapori ina fursa kubwa ya kulipatia Taifa mapato makubwa kuliko ilivyo sasa;

**KWA KUWA** utalii wa kina unaofanywa, umeonyesha kuwa makampuni machache ya wageni ndiyo yanayomiliki vitalu vingi na bora wakati kampuni nyingi za wazalendo zinamiliki maeneo yenye vitalu vidogo na visivyo bora kwa uwindaji kama ilivyo katika kiambatanisho A ;

**KWA KUWA** kisheria inafahamika kuwa mwaka 2009 ndiyo mwisho wa umiliki wa vitalu vyote vya kuwindisha na kwamba vitalu hivyo vitakuwa wazi kwa ajili ya kugawiwa upya na muda uliobakia ni mwaka mmoja ambapo hatua zote zinazotakiwa kwa ajili ya kugawa upya vitalu vinapaswa kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na wamiliki wavya kuanza kutangaza vitalu vyao kwa uwindishaji wa mwaka 2010.

**KWA KUWA** wataalamu wa Kamati Maalum ya uboreshaji wa shughuli za uwindaji, walipendekeza kuwa ili Taifa lifaidike zaidi kutokana na shughuli za uwindaji wa wanyamapori, vitalu vikubwa vyote vigawanywe upya ili kuongeza wingi wa vitalu baada ya kugundua kwamba baadhi ya vitalu ni vikubwa mno na kwamba tangazo la Serikali Na.156 la tarehe 29 Juni, 2009 linaonyesha ukubwa wa ubora wa vitalu na kwamba Serikali imeweka ada inayofanana kwa vitalu vyote, Kundi A na kundi B bila



kuzingatia ukubwa na ubora wa vitalu jambo linaloisababishia Serikali kutokupata mapato.

**KWA KUWA** masharti yanayotumiwa na Idara ya Wanyamapori kugawa vitalu, yanawanyima fursa waombaji wapya kwa kutoa fursa zaidi kwa makampuni yenye uwezo zaidi kifedha na pia ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa wanyamapori nchini umekuwa siri ya Mkurugenzi wa Wanyamapori na kwamba ugawaji wa vitalu hivyo huwa hautangazwi na hivyo kuendelea kutokuwepo na uwazi.

**KWA KUWA** mwaka 1994, Serikali iliingia mkataba au maelewano na *TAHOA* ambapo wameendelea kuutumia vibaya kwa maslahi ya wamiliki wachache wa vitalu hivyo vya uwindaji.

**KWA HIYO BASI**, ili kuondoa kasoro zote zilizojitokeza na kuiwezesha Serikali kuongeza mapato na kuweka uwiano, uwazi na usawa katika ugawaji wa vitalu vya uwindaji na uwindishaji wa kitalii, Bunge liazimie kama ifuatavyo:-

Kwanza, kwamba Serikali ianze sasa mchakato wa kugawa upya vitalu vyote vya uwindaji nchini kwa kuzingatia mapendekezo yaliyomo kwenye kiambatanisho A cha hoja hii.

Pili na mwisho, kwa kuzingatia kuwa muda wa kumiliki vitalu vya uwindaji utaisha mwaka 2009 na kwa kuzingatia umuhimu wa Sekta ya Maliasili ya Wanyamapori kwa pato la Taifa, Serikali iweke mikakati maalum ya kukamilisha utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo kwenye aya ya 1 - 5 ya kiambatanisho A cha hoja hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa mtoa hoja.

Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono na nitaomba muamue. Ninao wachangiaji hapa, idadi yao ni saba lakini nadhani kwa kutenda haki kwa zile hoja nyingine, sidhani kama nitazidisha zaidi ya wanne lakini hebu tuanze.

Nilionao kwa mpangilio ni Mheshimiwa Mgana I. Msindai na mzingatie kwamba Waziri wa Sekta anaweza kuwa na neno la kusema kwa hiyo inakuwa siyo wanne na Waziri anaweza kuwa wa tano. Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi, Mheshimiwa Aziza S. Ally na Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa. Hao wana uhakika wa dakika zao 15 au pungufu. Lakini Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mheshimiwa Boniface Simbachawene na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, sina hakika.

Kwa hiyo, tunaanza na Mheshimiwa Mgana I. Msindai, kisha ajiandae Mheshimiwa Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii ya uwindaji.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza ndugu yetu, Mheshimiwa Mzindakaya, kwa kuileta hoja hii ambayo kwa kweli imekuja kwa kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, mimi niseme wazi, nimefanya kazi Idara hii miaka 25 mpaka mwaka 1995 nilipoingia Bungeni ndipo nikaachana nayo na sizarudi tena porini na bunduki zangu zote kwa miaka yote, ziko Polisi, niliamua kuachana nayo kabisa.

Mheshimiwa Spika, suala la uwindaji, Tanzania tunalichukulia kama jambo la mzaha. Hapa Tanzania huu uwindaji wa kitalii umechukuliwa na watu binafsi ambao wapo hapa ndani ya nchi hii na wageni. Ukweli ni kwamba, Serikali yetu haipati mapato kwenye uwindaji, mapato inayopata ni kidogo sana, *Blocks* zimetaifishwa na watu, kwa miaka yote zimekuwa za watu fulani fulani.

Hata viongozi wengi wa Idara hii na wengine wapo Serikalini, wana vitalu kupitia kampuni nyingine, uchunguzi ukifanyika, hayo yatatabainika na hawa ndio wanaotuharibia sekta hii ya uwindaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mpaka leo hii, Sheria ya Uhifadhi ya Wanyamapori ambayo ilikuwa iletwe zaidi ya miaka minne iliyopita, inapigwa danadana kwa sababu wahusika hawajataka kuileta.

Mheshimiwa Spika, kwenye miaka 1974, Serikali iliona tunamaliza wanyama wetu bila kupata faida, ikafunga uwindaji wa kitalii na kweli wanyama wetu walikuwa wamepona lakini sasa mapori yote yameingiliwa. Zamani tulikuwa na *Game Reserves*, *Partial Game Reserves*, *Controlled Areas*, *Open Areas*, *hunting blocks* zilikuwa zinatolewa kwenye *Game Reserves* na *Controlled Areas*, lakini sasa hivi na ile *Open Areas* yaliyokuwa maeneo ya wananchi ili nao wawinde, wapate kitoweo, hizi *Hunting Blocks* siku hizi zimechukua mapori yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba uwindaji unaofanyika humo siyo wa kwetu ni wa wageni wakishirikiana na watu wachache waliopo humo ndani ya nchi lakini fedha tunayopata ni kidogo mno. Wawindaji wanapita South Africa, wanapita Botswana, wanapita Zimbabwe huku wanakuja kama *Blocks* za watu walioko South Africa. Wenye Makampuni ya Uwindaji, wageni wana zaidi ya *Hunting Blocks* nane na ukienda kugusa unaambiwa na watu wa Serikali, zina watu.

Mheshimiwa Spika, mwaka juzi wakati ninachangia hapa, nilisema jamani eeh, Idara ya Wanyamapori, ifanyiwe uchunguzi. Nilitwa *chamber*, nikaambiwa, unajua hivi vitalu ni vya fulani na tukimnyang'anya huyo, nchi yetu itakosa misaada kutoka Ufaransa na hiyo danadana inaendelea mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, mimi ingekuwa amri yangu, ni kufunga kabisa uwindaji hapa Tanzania kwa muda kwa sababu tunapoteza. Wawindaji wanatakiwa waende porini na Askari wetu, kwanza, tuna uhaba wa Askari, pili, Askari wetu wana njaa, akienda porini akipewa *dollar* 100, hafuatani na wale wageni anabaki kambini, wale wanakwenda kuwinda, anawinda yule nyati na akikutana na nyati mkubwa huyo anamtupa anapiga mwingine, hatupati faida.

Mheshimiwa Spika, fanya idadi ya Askari waliopo na *Hunting Blocks* zilizopo, utakuta Askari wetu ni wachache tena wengi ni wazee, wanasubiri kustaafu. Sasa Askari anayesubiri kustaafu akipata maslahi atayaacha!

Mheshimiwa Spika, halafu lingine ambalo nataka kulizungumzia, hao wenye Kampuni za uwindaji wanaleta *professional hunters* wao kutoka nje, sisi tunakosa *control* wakati tuna vijana wetu wamemaliza Mweka, kama tulivyofanya kwenye mahoteli, tuzuie ajira za watu kutoka nje, ili vijana wetu ndiyo wafanye kazi ya uwindishaji lakini mpaka kesho hakuna. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *Hunting Blocks* zetu sasa hivi kwa kweli niwaambie kabisa hakuna wale wanyama wakubwa wa *record*, wameshawindwa mno na tunachezewa. Bajeti iliyopita Waziri alileta bei za wanyama hapa na akasema hizo ndizo zitafuatwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa mtoa hoja amesema ukilinganisha bei za hapa na majirani zetu, za kwetu ni takataka lakini hata hizo walizotangaza hapa Bungeni wale wenye makampuni wamezikataa, makampuni mengi hawajalipa, sasa Tanzania tutaendelea kuchezewa hivi mpaka lini? Tuchezewe kwenye madini, tuchezewe hata huku kwa wanyamapori? Maeneo yote sisi tuendelea kuchezewa tu.

Mheshimiwa Spika, hebu Serikali ibadilishe mtindo uliopo wa uwindaji na ikishindikana wafungiwe, wasiendele. Nirudie kusema kwamba Watanzania hatujashirikishwa, ni Watanzania wachache sana wanapewa yale maeneo ambayo hayana wanyama. Kama ndivyo hivyo, tuazimie hapa Bungeni hakuna mgeni kupata kitalu, ni lazima awe Mtanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kusema kwamba pale Idara ya Wanyamapori hapajasafishwa bado, wapo watu ambao wamewekwa na wakubwa, bado wapo watu ambao wanashirikiana na hayo makampuni kuhujumu nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sisi tuliokaa mle, kwa kweli tunaona uchungu sana, tumefanya kazi kwa uaminifu mpaka tumetoka lakini sasa hivi nchi yetu inaliwa na wenye makampuni ya uwindaji, inatia uchungu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi niseme kwamba ninaiunga mkono hoja hii lakini hebu Serikali kama ilivyofanya upande wa madini iingie na huku ichambue kwa sababu nchi yetu inaliwa. Serikali inasema inapata fedha nyingi kutoka kwenye Makampuni ya Uwindaji lakini hakuna kitu robo tatu ya fedha zinakwenda nje na ndiyo maana hawataki kufungua akaunti hapa nchini na ndiyo maana vimewekwa vipengele,

ukienda kusema hivi, wanakwenda Mahakamani kwa kufuata vipengele walivyoweka wao, TAHOA, haitusaidii sana.

Mheshimiwa Spika, sisi tunaomba Serikali itulie, iingilie kati ili madhambi yanayoendelea kufanyika, yasiendeleo na mapato ambayo tunakosa tusiendeleo kuyakosa.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mgana Msindai ahsante.

Naomba nitoe rai tu kwamba itakuwa vyema kama mkijitahidi kuwa na mchango mfupi kama dakika 10 hivi ili tupate mchango wa wengi zaidi kwa sababu mkitumia dakika 15, nitaishia wasemaji wanne tu, halafu itabidi nimwite mtoa hoja. Kwa hiyo, natumaini Prof. Raphael Mwalyosi na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally na Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa mtaokoa muda badala ya kurudiarudia baadhi ya mambo, basi mlenge kwenye *point* chache na muhimu, hii itatoa fursa kwa wengine.

Sasa namwita Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, nianze na mimi kwa kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya kwa kuleta hoja hii binafsi kwa sababu ni muhimu na ni ya msingi na kama alivyosema Mheshimiwa Mgana Msindai, imekuja kwa kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, niseme tu kwamba, ninachangia hapa kwa sababu ninaielewa sekta hii. Taaluma zangu ambazo ninajivunia kwa kweli nimezipata kutoka upande wa wanyamapori na upande wa uhifadhi. Kwa hiyo, naelewa na ndiyo maana nasema nashukuru hoja hii imekuja kwa wakati huu ingawaje kwa kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, niungane na Mheshimiwa Mgana Msindai kusema kwamba uwindaji unaondelea sasa hivi na uvunaji huo, siyo endelevu. Sio endelevu kwa sababu takwimu zinazotumika kujua na kupanga wanyama kiasi gani kwa mfano wawindwe kwenye kitalu, siyo za ukweli kwa sababu hakuna utaratibu wa kuhesabu wanyama kila wakati au kabla ya kugawa kitalu. Kwa kawaida hatujui, kama huwa wana *estimate*, hawafanyi hesabu ya uhakika ya kujua kuna wanyama wa aina gani na kuna wanyama wangapi kwa kila aina, hawafanyi hivyo. Kwa hiyo, wanaanza na *benchmark* ambayo hatujui ni kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwindaji wa miaka mingi, mioto kichaa na kadhalika, *habitat* yaani mazingira wanayoishi wanyama hao ambao wanaenda kuwindwa yameharibiwa sana. Kwa hiyo, thamani ya mazingira yale na vilevile ubora wa wanyama hao ambao ni *trophy*, umepungua sana, kwa hiyo, wanyama wetu na mzingira yao, ni ya hali ya uduni sana.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mazingira ya namna hiyo, huwezi ukazungumzia kitu unachokuiza ni cha thamani. Kwa hiyo, thamani ya vitalu hivi na *product* tunazouza ni duni kwa sababu tumekuwa hatuna *benchmark* inayoeleweka, bila kujua tuna *resources* kiasi gani kwenye maeneo hayo, tunaendelea kuji-*exploit*, kwa hiyo, ndiyo maana tunapata fedha kidogo.

Mheshimiwa Spika, ukiacha maelezo aliyotoa Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya na kwenye ripoti hii na sababu nyingine zilizotajwa lakini linahusisha pia kwa kweli suala la mazingira na *quality ya resources* zilizopo kwenye vitalu.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nichangie kifupi kwenye mapendekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya kwenye *paper* yake. Nilitaka tuboreshe suala moja lifuatalo na ni hilo tu nitalizungumzia.

Mheshimiwa Spika, kwa vile thamani ya mazingira yale ya vitalu ni duni na *trophy quality* ya wanyama wanaowindwa ni *very poor*, ndiyo maana huwezi ukapata simba wale wenye manyoya makubwa yaliyokuwa yanaonekana zamani, siku hizi wanawinda simba wadogo tu, hakuna *quality trophies*. Hata tembo kulikuwa na wale wenye meno makubwa ambayo yanaburuzwa chini, siku hizi huwapati. Kwa hiyo, kwa sababu ya *quality* hiyo. Kuna makampuni yamekuja na kuwekeza kwa kuanzia kuboresha hali hiyo kwanza.

Mheshimiwa Spika, ninajua hata Mheshimiwa Waziri anajua kuna makampuni ambayo sitaki kuyataja, ambayo wamepeva vitalu lakini wameamua hawatawinda ila wanalipa kodi zote zinazostahili. Serikali inapata mapato yake yote, lakini hawawindi. Wameamua kwamba wanataka wazingatie suala la kupandisha *quality* ya vitalu na *quality* ya wanyama ili iwe bora na wingi wa wanyama uongezeke kwenye vitalu hivyo. Baada ya hapo, *quality* iki-*improve* ndipo waangalie utaratibu wa kuwa na *sustainable hunting*.

Mheshimiwa Spika, kwenye mapendekezo ninayoyaona ambapo tunataka uwindaji uwe kwa vipindi, nadhani ni miaka mitano au kitu kama hicho halafu iwe inatangazwa wa-*compete*. Ninapenda makampuni ya namna niliyoyataja hapo juu, yapewe fursa zaidi ya kuwepo kwenye vitalu hivyo kama *demonstration blocks* za kuonyesha wawindaji wengine namna ya kuboresha vitalu vya uwindaji hata kwa kusimama kuwinda kwa muda mpaka hali ya mazingira ya vitalu yaboreshwe ndipo wafikirie *hunting* kwa wale wanaonyesha *commitment* na *interest* kwenye *resources* za nchi pengine hata kuliko sisi wenyewe Watanzania tunavyofanya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mchango wangu ulikuwa ni huo kwamba tuwape fursa makampuni ya namna hiyo na tujifunze kutoka kwenye makampuni hayo na tutumie *knowledge* tunayoipata kwenye makampuni hayo kuyaelimisha makampuni mengine ili tuwe na *interest* na *commitment* ya kuhifadhi rasilimali tulizonazo ili tuendelee kuzitumia na kupata mapato kwa miaka mingi ijayo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Prof. Mwalyosi ahsante sana na pia nakushukuru kwa mchango wako lakini pia umetuokolea muda. Sasa msemaji anayefuata ni Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally halafu ajiandae Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii. Pia naomba na mimi nimpongeze Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya kwa kutuletea hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nitachangia haraka haraka, sitopenda kurudia kama ulivyotuelekeza.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichangie kwanza katika sehemu ya ugawaji wa vitalu. Hakuna uwazi ambao unaonyesha kuna vigezo gani vya ugawaji vitalu mtu akiomba aweze kuvifuata. Naomba tufafanuliwe kuna vigezo gani ambavyo vinatumika?

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, tuweze kufafanuliwa ni watu gani ambao wanapitisha mtu anapoomba kitalu. Wanaweza kusema kuna Kamati ndogo lakini kwenye ile Kamati ndogo, nina wasiwasi Mkurugenzi wa Wanyamapori ana nguvu zaidi kuliko watu wengine waliopo kwenye Kamati ile.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwepo na utaratibu ambao utaonyesha ni watu au Bodi gani watakaokaa kupitisha ni makampuni gani yatakayopata vitalu hivyo. Kwa sababu suala hili kwanza wala halitangazwi muda unapofika au hao wengine wanaosema baada ya miaka miwili hujui wao ni wahangaikaji wa kutafuta habari hizo ndiyo maana wamejua la sivyo huwezi ukajua utasikia tu muda umepita vitalu watu wamekwishapata. Kwa hiyo, hilo ni suala mojawapo linalotutia wasiwasi sana, kwa nini isiwe wazi kama sehemu zingine zinavyokuwa wazi. Kwa hiyo, naomba sehemu hiyo iweze kuangaliwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Tabora na sisi pia tuna sehemu ambayo ni ya uwindaji. Mheshimiwa Mbunge wa Urambo Mashariki ambaye ni Mheshimiwa Samuel Sitta, kwake vitu hivyo vipo lakini katika Jimbo lake kwa kweli tangu mwaka jana kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge wa Urambo Mashariki tuliomba hata kupata *dispensary* kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Wanyamapori, lakini wapi. Mheshimiwa Mbunge huyo alihangaika muda mrefu mpaka sasa mwaka mzima zile fedha hazijapatikana. Sasa wananchi wale wa Mheshimiwa Samuel Sitta, wananufaika vipi na uhifadhi ule ambapo wanawahifadhi wanyama wale? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Said Nkumba, sehemu ya Sikonge, tumejenga *dispensary* lakini bado hatujapata mtu wa kuweza kutusaidia. Wananchi wananufaika vipi?

Maskini Mheshimiwa Samuel Sitta, yeye akiwepo pale kwenye kiti anashindwa kusimama na kujieleza lakini nachukua nafasi hii kumwomba au kusema ya kwamba

anapata shida, wananchi wake wanamsumbua. Kwa hiyo, naomba muweze kumwangualia aweze kupata na yeye kama wanavyopata watu wengine ambao wamezungukwa na Hifadhi za Wanyama. (*Makofi*)

**SPIKA:** Sijui Mheshimiwa Waziri anaandika mambo mazuri kama hayo? (*Kicheko*)

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la WMCA. Mwekezaji anapokwenda kuwekeza pale, wananchi wanakwenda kuongea naye na wana uwezo wa kukubaliana naye ili aweze kuwekeza pale. Tatizo linakuja, Wizara wanahitaji wao wawapeleke watu wanaowahitaji wao badala ya Wizara kupata ushauri kutoka kwa hao wananchi ambao wanafanya nao kazi na ambao wana *deal* nao kila wakati na ambao wanaishi nao lakini wao wanamtafuta mtu kutokana na wao wanavyoona kuwa anafaa kuweza kukaa pale.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara izingatie Kamati hizo za wananchi ambazo zinakaa na wale watu kuweza kuteua yule mwekezaji wanayemwona wao anafaa na wanayemwona kwamba anasaidiana nao ambapo itaweza kuwasaidia na kuwapa moyo wale wananchi kuweza kushirikiana na yule mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna suala la ushirikishwaji lakini suala la ushirikishwaji wao wakishaleta mtu wanaomjua wao, wananchi kushirikiana na yule mtu ambaye wamemleta wao, inakuwa siyo rahisi zaidi kuliko yule wanayemtaka wao wenyewe. Lazima tukubali kuwapa na wao uhuru wa kuweza kuchagua mtu ambaye ana uwezo wa kuweza kushirikiana na wale wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine kuhusu upandishwaji wa bei. Hili linachekesha na linasikitisha na linatia aibu sana na kichefuchefu juu yake. Mwaka jana tumepitisha hapa bei za uwindaji, matokeo yake kulikuwa na kikao Marekani, waliondoka watendaji wetu wakaenda kuandaa kitabu hiki ambacho kina bei tofauti na zile ambazo tulizipitisha hapa Bungeni. Sasa nina swali moja la kuuliza, katika nchi hii kuna Serikali ngapi? Kwa sababu kitabu hiki kina nembo ya Serikali na kila kitu kimeenda kama Serikali lakini Bunge na mimi nikiwa ni mjumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, najua bei ambazo tulizipitisha hapa na ninazo. Kwa hiyo, naangalia hizi bei na bei zilizoandikwa katika kitabu hiki, bahati mbaya, sisi Wajumbe wa Kamati wala hatuna na hata Wizara naona hana, labda anacho Mkurugenzi na watu wake wachache...

**MBUNGE FULANI:** Wewe umepata wapi?

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mimi nimetafuta kwa mtandao wangu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hivi ni vitu ambavyo vinafurahisha, vinasikitisha na vinachekesha. Naomba Wizara itufahamishe kuna Serikali ngapi? Kuna Serikali ya Maliasili na kuna Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? Kama lipo hilo, tuweze kulielewa kusudi haya masuala ya wanyamapori na masuala ya Wizara, sisi

Bunge tusiwe tunayapitisha hapa, tuwe tunaiachia Wizara yenyewe inaendelea kufanya kuliko kuwa wanatashirikisha vitu ambavyo vinakuwa hewa, tunapoteza muda wetu na tunapoteza fedha za wananchi kwa sababu vinaenda kufanyika vitu tofauti na tulivyopitisha hapa ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, nataka kuja moja, ni nani aliwapa idhini ya kufanya hayo? La pili, walienda kutangaza bei hizo wakiamrisha na nani na nani ambaye atazitekeleza?

Je, wale watu watakaokuja kuwinda na bei hizi ambazo zilipitishwa hapa, ni kwa namna gani watakaopitia mahesabu ya Serikali wataelewa kwamba bei zimepungua au zimeongezwa? Bei tulizopitisha sisi hapa ni kubwa lakini bei zilizokuwa humu kwenye kitabu ni mdogo, je, zitaingizwa katika mfuko upi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa naomba pia nimpongeza Mheshimiwa Rais, nimeona kwenye magazeti leo, wanasema Mheshimiwa Rais anahitaji kujua akaunti zile ambazo ziko nje. Mimi pia hiyo inanifanya kuwa na wasiwasi na suala hili pia, je, hizo fedha huwa zinapita wapi? Kama zinapitia huko basi zinaingia kule wao wanakuja kuwinda kwa bei ambayo ni tofauti au wanawinda wakiwa hewa? Hiyo yote na mimi nimekwishaitilia mashaka.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka la mwisho. Naomba nishauri katika Bunge hili au Serikali, Kamati ya Maliasili na Mazingira, tulikuwa tunaomba tuletewe utaratibu huu au tuletewe hoja hii haraka ili tuweze na sisi Kamati yetu kuichambua na kuweza kushauriana na kuijadili pamoja na Wizara kwa sababu tutawaita tukae nao watueleze haya mambo ambayo ameyaleta Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya na hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, tunaomba haraka sana tuletewe kabla ya Bunge la bajeti ili tuweze kulijadili angalau tukija katika Bunge la bajeti, tuwe tumejua wapi tumefikia ili tusiwe tunayafanya haya mambo ya kuleta hoja na kuzipitisha lakini bila kufanyiwa kazi. Tunahitaji hoja zinazoletwa hapa Bungeni ziweze kupitishwa na matokeo yake yaonekane.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally ahsante sana.

Msemaji wangu wa mwisho kwa maana ya upande usio wa Serikali, ni Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na baada ya hapo nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, hatimaye mtoa hoja mwenyewe. Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, endelea.

**MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii kuzungumzia hoja ya Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, juu ya ugawaji wa vitalu vya uwindaji na bei zake ambavyo muda wake kisheria unaishia mwaka 2009.



Mheshimiwa Spika, ndio nimesimama maana kuna watu wanasema siwezi kusimama, nimesimama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, nakuona, usiwajali hao. (*Kicheko*)

**MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Spika, msingi wa hoja ya Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, ni hoja mbili. Kwanza, anataka tuongeze mapato ya Serikali kutokana na maliasili hususani uwindaji wa wanyamapori na hili jambo haliwezi kuwa na ubishi, maana tunahitaji fedha. Kwa hiyo, hili liko wazi. Mheshimiwa mtoa hoja, amelieleza vizuri na wenzangu walionitangulia kuzungumza hapa wamelisemea vizuri. Kwa hiyo, hili sitaki tena kulisemea.

Mheshimiwa Spika, ninataka kuzungumzia sehemu ya pili ya hoja yake ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Hili la kuwawezesha wananchi kiuchumi, ninadhani ni kubwa sana na ni muhimu sana na tusilipuuze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza, simwoni pale *comrade*, Mheshimiwa Philip Marmo, suala hili la malalamiko kuhusu vitalu siyo jipya, lilifanyika katika miaka 1992, 1993 na 1994 ikafanya mpaka wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Utalii, Maliasili na Mazingira wakati huo alikuwa anaitwa Waziri wa Utalii, Maliasilia na Mazingira hoja yake ya bajeti hapa mwezi Julai, 1994 nusu ikwame na ikaokolewa kwa hoja ya kwamba iundwe Kamati Teule. Kamati Teule ile iliongozwa na ndugu yangu Philip Marmo na wajumbe wake wapo na waliandika ripoti nzuri tu, kubwa, hii hapa na ipo maktaba pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilipopata fursa ya kusema leo, basi nikamwomba mfanyakazi wa maktaba anitafutie ilikuwa imewekwa kwenye *shelf* kule chini kabisa haionekani mpaka uitafute kweli ndiyo unaipata. Sasa nina-*recommend* ripoti hii itazamwe *first for reference* kwa *Minister of Natural Resources and Tourism, Madam Shamsa Mwangunga*, maana itamsaidia kweli kujua hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kuna ripoti ya pili, ambayo inatokana na majibu ya Serikali Bungeni, nayo ni kubwa namna hii na hivi vyote vipo kwenye Maktaba pale Wizarani kwa sababu baada ya ile ripoti ya Mheshimiwa Philip Marmo, mimi ndiye niliyeteuliwa kuwa Waziri wa Maliasili na baadhi ya mapendekezo tulianza kuyatekeleza kwa sababu wajumbe wa Kamati hiyo walitoa mapendekezo mazuri.

Mheshimiwa Spika, moja ni la kuundwa kwa Kamati ya Ushauri ya Ugawaji wa Vitalu na mimi nilikuwa wa kwanza kuunda hiyo Kamati, nikamweka *Chairman Retired Judge of the High Court* kwa madhumuni ya kwamba hilo jambo ni la kisheria. Maana Sheria ile ya *Wildlife Conservation Act of 1974*, ni *very technical law*. Kuna wakati fulani wakubwa fulani walisema Juma Ngasongwa amegawa vitalu, kumbe ni vile vitalu vya *Presidential licences*, wakasema hii *Presidential licences* anagawa Rais. Mimi nikasema, siyo bwana, *Presidential licences* anagawa *the Director of Wildlife with the consent of the Minister of Natural Resources and Tourism*, ndivyo Sheria inavyosema, sasa watu huwa

wanachanganya changanya mambo sana. Kwa hiyo, mimi ninaomba hili jambo litazamwe vizuri kwa sababu ni la Kisheria na litazamwe sawasawa.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, walipendekeza kupunguza Makampuni yanayowinda wakasema Makampuni yapungue kutoka 43 wakati huo mpaka Makampuni 20. Lakini pendekezo zuri zaidi ni lile la tatu sasa, wakasema Makampuni haya yote yawe ya Watanzania, yasiwe ya wageni.

Mheshimiwa Spika, mimi ninataka kulisemea hili la kuwa na Makampuni ya Watanzania kwa sababu hili ndilo la uwezeshaji wananchi kiuchumi na hili halikufanyika wakati ule kwa sababu gani? Halikufanyika kwa sababu mwaka 1994 hata ndani ya Chama chenyewe, *clarity* ya Sera ya Uwezeshaji ilikuwa bado ile *clarity* imeanza mwaka 2000 ambapo ndipo tukatoa mwongozo unaitwa Mwelekeo wa Sera za CCM miaka ya 2000 mpaka 2010 na mle *key element* ndiyo ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Kama mabadiliko ya sera ya nchi yetu, tena bahati nzuri Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru yupo pale, sikumwona, maana ndiye alikuwa *Chairman* wa uandaaji wa Sera za miaka 2000 -2010 na hilo suala la uwezeshaji ndipo likajitokeza pale

Mheshimiwa Spika, mimi bahati nzuri ndiyo nikawa *Chairman* wa Kamati ya Ilani ya CCM mwaka 2000, suala la uwezeshaji tukalileta hapa kama *critical issue* katika nchi yetu. Kwa hiyo, kazi nzuri imefanywa mwaka 2003 na Kamati ya Baraza la Mawaziri iliyoandaa Sera za Uwezeshaji Kiserikali na Rasimu ya Sheria ya Uwezeshaji ya Mwaka 2004, sasa mle ndio mkaweka mambo mazuri zaidi. Mlitaja *very clearly* kwamba kuna sekta fulani lazima wapendelewe Watanzania na mojawapo ni ya maliasili. Kama alivyosema mtoa hoja pale, maliasili hakuna uwekezaji katika *real-estate* pana uvunaji tu, unaweza kuvuna sio mpaka wavune Wazungu, mna matatizo gani nyie, wapo hao Waarabu na Wahindi, *why?*

**MBUNGE FULANI:** Hatuna mahali.

**MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA:** Hamna mahali, sawa.

Mheshimiwa Spika, halafu hawa watu wa Awamu ya Nne wamefanya mambo mazuri sana, wame-*establish even a Ministry* ya Uwezeshaji. *Of course* iko *combined* na *Ministry* ya *Finance and Economic Affairs* lakini Idara ile iko pale bado. Kitu kizuri pale ni kutokana na utekelezaji wa ile Sheria Na. 14 ya mwaka 2004, ambapo tumeanzisha Baraza la Taifa la Uwezeshaji wananchi kiuchumi (*The National Economic Empowerment Council*). Lakini vile vile tumeanzisha ingawa kwa fedha kidogo *The National Economic Empowerment Fund* kwa ajili ya kuwawezesha Watanzania. Lakini vile vile tumeanzisha lile jambo kubwa la mabilioni ya JK kama sehemu ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Lakini nadhani hili la *Economic Empowerment Fund* ndio *more sustainable*, kwa hiyo lazima tulishughulikie. Katika mapato yale ya maliasili Mheshimiwa Waziri, unaweza kupeleka pale katika *Economic Empowerment Fund* ili iweze kutumiwa zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, hata juzi nilikuwa nazungumza hapa na Waziri wa Nishati na Madini, sasa hivi hayupo, nikamwambia lile suala la wachimbaji wadogo wadogo tumeliweka vizuri katika Ilani ya mwaka 2005/2010. Hoja yake ya msingi ni kuwawezesha hawa wananchi wadogo wadogo kiuchumi na lazima tuwe na *deliberate policy* ya kuwasaidia hawa.

Mheshimiwa Spika, lingine *infrastructure* zilizopo pale, *contracts* ndogo ndogo kwa nini wapewe Wazungu, Wachina na watu wengine wakati ndio za kwenda kwa wananchi wetu, hiyo ndiyo sera yetu ya kuwezesha wananchi. Nyinyi wa Awamu ya Nne, mna *commitment* kubwa sana mimi nataka kuwapongezeni pamoja na matatizo mengine lakini hili mmefanya vizuri la kuchangamkia uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na lazima tulifanye.

Mheshimiwa Spika, nataka kumalizia na mimi nataka ku-*save time* kwa ajili ya wenzangu ni kwamba kwanza tukubaliane na hoja ya Mheshimiwa Mzindakaya kwa sababu ni nzuri sana kwa *level* zote za *income generation* kwa ajili ya nchi lakini vile vile kwa ajili ya *economic empowerment*, tukifanya hivyo tunaweza kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, mimi ngoja niseme la mwisho, mimi natoka Mkoa wa Morogoro ambao unazungukwa na Selous lakini pia natoka katika Wilaya ya Ulanga ambayo inazungukwa na Kilombero *Game Controlled Area*. Kwa kweli tumejifikisha mahali pabaya mpaka hata maeneo ya wananchi tumewagawia vitalu watu wa nje na tuna sera nzuri ya *Wildlife Management Areas* ambapo wananchi watawinda kwa ajili ya kitoweo, sasa hivi tumewabana kabisa hawana tena maeneo ya kuwinda. Sasa, naomba hili nalo litazamwe vizuri wakati Mheshimiwa Waziri unapolitazama suala hili na hili nalo ulifanyie uchambuzi mzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana na naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kwanza nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kwa hoja yake binafsi kwa kuwa hoja hii ni mchango unaolenga kuboresha tasnia yetu ya uwindaji wa kitalii nchini. Lakini pia napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao na wenyewe wamechangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, umenipa dakika 15 lakini maelezo ni mengi, nitajitahidi. Kwanza napenda kwa haraka tu nianze na michango waliyochangia Waheshimiwa Wabunge na baada ya hapo kwa kifupi nitachangia hoja nzima kama jinsi Mheshimiwa mtoa hoja alivyoielezea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Msindai ameongelea kuhusu mambo mbalimbali kuhusu uwindaji unavyoendelea na jinsi ambavyo nchi yetu inafikia hatua ambayo baadhi ya mambo yaliyokuwa yanategemewa hayaendi jinsi ambavyo

Mheshimiwa mchangiaji alivyoona. Napenda kusema tu kwamba Serikali imeyapokea mambo ambayo Mheshimiwa Msindai ameyaongelea.

Mheshimiwa Spika, pia ameshauri kuwa Serikali ibadilishe mtindo wa uwindaji, hili ni jambo ambalo ni mojawapo ambalo tunalishughulikia. Lakini pia ameongelea kuhusu TAHOA kwamba haisaidii sana na ni Chama cha Wawindaji wa Kitalii lakini chama hiki kilianzishwa kwa madhumuni ya kuweza kusaidia wakati ule ambapo hatuna utaratibu maalum. Lakini kwa sasa hivi utaratibu mzima unaendeshwa kwa kufuatana na Sheria ya Mwaka 2002 lakini pia na sheria mpya ambayo tumeshaiandaa inasubiri kuingia Bungeni kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge kutoa baraka zao.

Mheshimiwa Spika, tumepokea mchango wa Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, kuhusu uwindaji na uvunaji usio endelevu. Lakini napenda kumfahamisha kwamba kwa hivi sasa Wizara yangu tulichokifanya ni kwamba tumeweka wataalam ambao wakishirikiana na Shirika letu la TAWIRI waweze kupima sehemu mbalimbali kujua ramani za vitalu, kujua vitalu viko wapi na vitalu vina maeneo gani na hali kadhalika kila kitalu kina wanyama kiasi gani na baada ya hapo ndipo tutakuwa na uwezo sasa wa kujua kiasi gani cha wanyama wako sehemu gani na vitalu vinaendeleaje. Ni jambo ambalo tumeanza kulishughulikia na hivi karibuni wataalam wataanza kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, yeye ameongelea kuhusu vigezo vya uombaji wa vitalu na pia utaratibu mzima kwamba hauna uwazi wa kutosha. Lakini napenda kumfahamisha kwamba vigezo vipo na utaratibu upo. Kuna Kamati ambayo huwa inapendekezwa halafu Mheshimiwa Waziri mhusika ndiyo anaipa ruhusa iweze kushughulikia ugawaji wa vitalu.

Mheshimiwa Spika, muda wa kugawa vitalu, ni jambo ambalo kwa kweli napenda kusema kwamba huwa linafanyika lakini jambo ambalo labda halikuweza kutiliwa maanani ni kwamba inabidi na wananchi waweze kufahamishwa. Naomba niseme kwamba Wizara yangu itahakikisha kwamba wananchi watapewa taarifa zote kwamba vitalu viko wapi na lini mgao utafanyika na ni lini watu waanze kuomba vitalu hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Mheshimiwa Aziza, ameongelea kuhusu mambo ya Mfuko wa Wanyamapori kunufaisha wananchi ikiwemo Wilaya ya Urambo na Jimbo la Mheshimiwa Spika. Napenda kumfahamisha kwamba kweli mfuko huu upo na kuna baadhi wananufaika nao lakini hata hivyo kwa suala hili, naomba niahidi kwamba nitalishughulikia ofisini ili niweze kujua kwa upande wa Urambo kama hawajapata na ni njia gani tutumie kuhakikisha na wenyewe wanapata manufaa kama wenzao wanavyopata maana kuna njia nyingi za kupata manufaa hayo ikiwemo kama pia wana sehemu ya kuweka wawekezaji na kuna ujirani mwema na hali kadhalika kuna Mfuko wa Wanyamapori, hilo naahidi nitaishughulikia.

Hiyo sio kwa Jimbo hilo tu pia napenda kusema kwamba Majimbo yale yote ambayo yamepakana na hizi hifadhi na kama yapo ambayo hayajapata na yenyewe tutahakikisha kwamba wanapata kwa sababu sasa hivi najua kuna Wilaya kama 42 ambazo zinanufaika na hifadhi hizo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Alhaj Dr. Juma Ngasongwa, mambo aliyozungumzia, napenda niyapokee kwa furaha kabisa. Ni mambo ya msingi na ripoti alizozielekeza, nitakaa na mimi nizatazame kwa makini na pia napenda kuunga mkono kwamba kwa kweli Watanzania lazima wawezeshwe kwa sababu nchini pao ndio mahali pao pa kunufaika.

Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nichangie kwa haraka haraka kuhusu mtoa hoja alichooonga. Tunajua muda ni mdogo, nitajitahidi mengine ambayo yatashindikana pia nitaweza kuyaweka hata katika maandishi. Lakini la kwanza aliongelea kuhusu muundo akatoa mapendekezo mbalimbali kuhusu ushiriki zaidi wa Watanzania na uwazi katika tasnia ya uwindaji. Hali kadhalika na ushiriki zaidi kwa Kampuni za Kitanzania katika maamuzi hayo.

Napenda kusema kwamba Serikali imeanza kulifanyia kazi suala hili ambapo kuanzia mwaka 2000 hakuna kampuni ya kigeni iliopewa kitalu badala yake kampuni za Watanzania 15 na 2 za ubia ndizo ziligawiwa vitalu. Mwaka 2000 kampuni za wageni zilikuwa 16 na sasa zipo 13. Wakati kampuni za ubia zilikuwa 7 na sasa zipo 9, kampuni za Tanzania zimeongezeka kutoka 17 hadi 32.

Mheshimiwa Spika, lakini hapo napenda nikiri kwamba ni kweli kampuni za Kitanzania zimechelewa kuingia katika fani hii ambapo kampuni za wageni zilianza siku za nyuma sana na ndiyo sababu wenyewe walinufaika wakachukua maeneo yale ambayo tunaita *Prime Areas* na Watanzania kwa bahati mbaya wengi hawakuweza kunufaika na huko lakini napenda niwahakikishie kwamba kwenye mgao wa 2009, hayo yote yatazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, la pili napenda kusema kwamba Wizara inatambua kuna haja ya kuufahamisha umma jinsi ya kuendesha shughuli mbalimbali tunazofanya. Nimeahidi kwamba tutaufahamisha umma mambo yote ya kuhusu vitalu, ugawaji hali kadhalika kwamba viko wapi na lini kikao kitakaa cha kupitisha maombi na baada ya maombi tutataja majina akina nani waliopewa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TAHOA*, nimeshaliongelea kwamba kwa sasa hivi tuna Sheria yetu ya wanyamapori ndiyo inayotawala. Zamani tuliweza kushirikiana nao kwa sababu kulikuwa hakuna wengine na tulitaka kuwe angalau na utaratibu fulani wa kuhakikisha kuwa haya mambo yaanze kufanyika kwa sababu huwa kuna vurugu nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, lingine aliongelea kuhusu mambo ya Sheria. Napenda kukufahamisha kwamba mapitio ya Sheria ya Wanyamapori, Sura ya 283 ya mwaka 2002, sasa hivi tumeirejea na ndiyo hiyo ambayo sasa hivi tumeshairekebisha. Tutaomba ushirikiano wa Waheshimiwa Wabunge tutakapoleta Bungeni, Mwenyezi Mungu akijalia, Bunge lijalo, muweze kutusaidia kutuelekeza ili tuweze kuipitisha. Mambo mengi ambayo yamezungumziwa sasa hivi yakiwemo maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya

Wanyamapori kwa ajili ya wananchi yameingizwa humo na mapendekezo mbalimbali jinsi ya kufanya kazi hizo zote yamewekwa.

Mheshimiwa Spika, pia ameongelea kuhusu Kampuni za Uwindaji kwamba ziweze kuongeza michango yao katika shughuli za uwindaji ili kupunguza umaskini. Ni kweli hiyo naafiki na nakubali na tutaitekeleza.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo amelizungumzia ni kuhusu wawindaji kwamba pesa wanalipa kule huku wanakuja tu, sisi tunapata ada za *trophies*. Nimekubaliana na wazo hilo na tutawashirikisha TRA na wahusika wote kuhakikisha kwamba hilo nalo linabadilika ili hawa wawekezaji wafungue akaunti hapa Tanzania na sisi tuweze kufahamu kila kitu na mapato mbalimbali ili yaweze kuwanufaisha Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lililoongelewa kuhusu mfumo na umiliki wa vitalu kwamba uwe na ukomo na ikapendekezwa pia muda. Napenda kusema kwamba mapendekezo haya ya ukomo wa vitalu kwa kampuni ni mazuri sana. Wizara itayafanyia mapitio ya kisayansi ili kupata uwiano wa idadi ya vitalu vitakavyowezesha kampuni moja kujiendesha kibiashara bila kuathiri, kuhifadhi na kuwa na matumizi endelevu. Tumepokea na tutayafanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia katika ugawaji wa vitalu, napenda kusema kwamba Wizara itaanza kutumia mfumo uliopendekezwa mara baada ya kupata matokeo ya tathmini ya ubora wa vitalu ambapo mchakato wake umeanza. Kama nilivyosema Shirika letu la TAWIRI wakishirikiana na Wizara ya Ardhi na wataalamu mbalimbali, wanafanya kazi hiyo ili tuweze kutathmini mambo ya vitalu na kila kitu na ikishajulikana, tutaanza kutumia mfumo huu mara moja na kuacha huu mfumo wa zamani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mambo yaku-*grade* vitalu, kuvipa thamani, hilo ni jambo zuri, tumelikubali na kazi ya kutathmini ubora wa vitalu katika kuviweka katika madaraja, ni muhimu na hiyo yote itakuja baada *exercise* tunayoifanya ya upimaji ili kujua ukubwa wa vitalu na mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kusema kwamba katika kutekeleza kanuni za uwindaji na kuzuia uwepo holela wa makampuni unaosababisha mabadiliko ya umiliki wa vitalu usiotambulika, hilo pia Wizara yangu itashirikiana na BRELA ili kuweka mikakati itakayosaidia kusimamia kanuni zote ili mambo yaende kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba mambo yote ambayo mtoa hoja ameongelea na mengine ambayo sisi pia katika utafiti yasiyo na ufanisi katika nchi yetu, sisi tunaahidi kwamba tutayaondoa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, naomba nirukeruke mengine, niongelee tu yale ya mwisho kwa haraka haraka, najua muda unanitupa mkono, ni kuhusu ada ya vitalu kwa

mwaka 2008. Ni kweli sisi tunafahamu ada tulizotoza zamani zilikuwa ndogo lakini napenda kusema kwamba mapendekezo yaliyotolewa na mtoa hoja ni ya msingi na ni mazuri na sisi tunaona kwamba iko haja ya bei zetu kuongezeka. Lakini naomba kusema kwamba kwa sababu sasa hivi ni ushindani wa soko na ni soko la dunia nzima na mambo kama tunavyofahamu ya *globalization*, kwa hali hii tumekubali kwamba mapato yetu yaongezeke, bei zetu ziongezeke lakini tutachukua kwa kufuatana na nguvu ya soko la dunia linaendaje na sisi tutakwenda sambamba na wenzetu duniani kote.

Mheshimiwa Spika, pia pendekezo la *Game Reserve* ikiwemo Selous kwamba utaratibu wake uwe tofauti, ni jambo ambalo tulishalifikiria kufuatana na mapendekezo yao waliyotoa mwanzoni na hiyo ndiyo hali ambayo tunaitegemea mwaka 2009, tuweze kubadilisha. Tulikuwa tuna aina mbili ambayo tulipendekeza na nashukuru mtoa hoja ameziongelea ni kwamba kuna baadhi ya vitalu ambavyo tunajua ni *prime* kwamba kutakuwa na kunadi yaani tutatumia minada lakini pia kuna vitalu vile vidogo vya *open area*, tutakuwa tunatumia zabuni za aina mbalimbali na pia tutaweka bei ambazo zitakuwa *fixed* na vile vikubwa nguvu ya soko ndiyo itakayoamua.

Mheshimiwa Spika, muda umeniishia, napenda tu kwa kifupi niseme kwamba kuna mengine mtoa hoja aliyoyaongelea, tumeyapokea na tutayafanyia kazi. Napenda tena nimshukuru kwa mchango wake huu, ni mchango mzuri sana, ni mchango ambao kwa kweli na nina uhakika kwamba utasaidia Wizara yangu ipige hatua na pato la nchi liongezeke.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba na mimi naunga mkono hoja hii. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema, nakubaliana mia kwa mia na wewe kwamba kwanza hoja nyingi walizosema Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri amekwishazijibu, kwa hiyo ningependa kwanza kabla sijasema kwa kifupi kabisa, niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia ambao ni Mheshimiwa Msindai, Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii na Waheshimiwa Wabunge wawili wamechangia kwa maandishi ambao ni Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Lembeli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimefarijika sana na michango ya Waheshimiwa Wabunge wote katika kuunga mkono hoja hii na vile vile nataka nitoe shukrani zangu maalum kwa Mheshimiwa Waziri kwa sababu yeye ni Waziri ambaye ameingia katika Wizara hii si muda mrefu, ndio ameanza kazi kwa kweli. Yeye kukubali mapendekezo haya, ni ishara ya moja kwa moja kwamba ni Mwanamapinduzi atakayesaidia kuiweka Wizara hii katika mstari.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka kumthibitishia Mheshimiwa Waziri kwamba sisi tutashirikiana na yeye kuhakikisha kwamba unafanya kazi kwa usahihi kwa sababu sisi tunajua matatizo ya Wizara yako. Tunajua hata ulipokuwa Naibu Waziri katika Wizara nyingine ulifanya kazi zako vizuri na huko pia tunakutakia kheri ufanye kazi zako vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninapenda niseme neno moja kubwa la msingi, nalo ni kwamba, mapendekezo yote haya niliyoyaleta katika hoja hii yanazingatia kuipa muda Serikali ijiandae vizuri mwaka 2010, wataona wenyewe si za sasa ni mpaka mwaka 2009. Mapendekezo haya, zaidi yanahusu uwindaji kuanzia mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, labda jambo moja ambalo ni muhimu sana hapa ambalo napenda kulizungumzia ni namna ya kugawa vitalu. Kama alivyosema Waziri, mimi namshauri iwe Sheria kwa sababu gani wenye vitalu na anayegawa vitalu wala sio Kamati ile, ile Kamati ilipendekezwa na Kamati ya Mheshimiwa Marmo, hajjawahi kuingizwa kwenye Sheria, ni Kamati tu iko inafanya kazi ikitaka, kwa maana wakitaka. Lakini wanaofanya kazi hapa kwamba vitalu vigawiwe kwa nani, sio Kamati hiyo, ni Serikali, haitambui Mwenyekiti ni Mkurugenzi wa Wanyamapori na Sheria ya kugawa vitalu inamtaja Mkurugenzi wa Wanyamapori, haitaji Kamati hiyo. Kwa hiyo, tunapendekeza Sheria iweke utaratibu ambao si Idara au mtu mmoja kama tunafikiria juu ya Kamati basi Kamati hii iingizwe ndani ya Sheria kuhalalisha madaraka yake.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu uwezeshaji. Hili naomba nilielezee kidogo. Ni hivi, kwanza vitalu kama nilivyosema, ni siri, mtu akiomba kitalu ataomba tu kwa kuomba hajui kitalu gani anachokiomba, hajui. Sasa wale wataalamu wa Idara ile wanapopokea maombi ya mtu huyu, wanamfuata wanamwambia, tutakutembelea siku fulani, tunataka tukukute. Wakifika, wanataka aonyeshe kama, je, ana mahema atakayotumia kwa wawindaji, ana magari mawili yatakayotumika kwa ajili ya uwindaji, ana friji au ma-*deep freezer*?

Ni vitu vingi sana wanataka huyu awe navyo. Sasa swali linakuja je, mtu huyu hajapewa kitalu anatakiwa awe na vitu hivi si lazima awe na pesa, ni tajiri je, akinyimwa kitalu hivi vitu avipeleke wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi katika *empowerment program*, tulipata nafasi ya kuzungumza na Mheshimiwa Waziri Dr. Ngasongwa na wataalam wake wakasema utaratibu ukibadilishwa inawezekana hivi vigezo visiwe vitu hivi kwa maana ya vifaa, vigezo viwe ni utalam. Sasa anapopewa barua ya *allocation* ya kitalu, barua ile ndiyo ataitumia kwenda Benki kuomba mkopo na apewe muda wa miezi sita, wanamwambia tangu tunakupa *allocation* hii baada ya miezi sita kama hujaonyesha vitu hivi utanyang'anywa *allocation*. Hivi ndivyo tunavyofikiri inawezekana lakini wakiendelea na huo utaratibu, watu wadogo hawawezi kupata vitalu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwa kumalizia ni kuwa kama alivyosema Mheshimiwa Profesa, nafurahi Waziri ameliona na amesema na mimi nataka niisitizie hilo moja. Ni hivi, mimi namfahamu mtu mmoja ambaye amepewa kitalu kule Arusha, yeye analipa kodi zote lakini pesa zake anazopata anazipata kwa kupigisha picha na anaingia gharama ya kuhakikisha kwamba wanyama wanaongezeka na wanakuwa bora. Kwa hiyo, nafikiri tutakapokuwa tunatunga Sheria, tungeweza tukatizama jambo hili nalo liwe wazi kwa maana ya hawa wanaopenda kusaidia. Lakini wenzetu pia hasa Afrika ya Kusini walikwisharuhusu *game launching* yaani mtu anaweza akaruhusiwa akafuga wanyama wa porini, shamba kubwa anafuga na inawezekana.



Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niseme nimefarijika sana kwanza na uongozi wako mwenyewe na Kamati husika na nimefarijika na maelezo ya Waheshimiwa Wabunge na hususan Waziri mwenyewe kwa maelezo aliyoyatoa. Nataka niombe kwamba ile dhana ya kusema wageni ndio wanafanya nchi ipate fedha, tuiondoe kwa sababu ninao ushahidi hapa kwamba wawindaji hawa hawa wanaojisifu wataongeza pato, kwa miaka 5 iliyopita, hatujawahi kupata zaidi ya dola milioni 9 kwa mwaka, ninazo rekodi zinazoonyesha hatujawahi kuvuka hapo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana mtoa hoja Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya.

Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyo mbele yetu inahitimishwa pale ukurasa wa 3 na wa 4 wa hoja yenyewe. Kwa kifupi ni kuweka utaratibu mpya wenye manufaa zaidi kwa nchi kuhusu ugawaji wa vitalu vya uwindaji.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja Binafsi ya Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji na Bei  
Zake ambavyo muda wake Kisheria unaishia  
mwaka 2009 ilipitishwa na Bunge)*

## **UENDESHAJI USIORIDHISHA WA SHIRIKA LA RELI TANZANIA UNAOFANYWA NA KAMPUNI YA RITES YA INDIA**

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Aidha nitazingatia kutumia muda mfupi kutokana na ulivyoshauri lakini nitapenda hoja yangu inukuliwe kama jinsi ilivyo na nitakwenda katika maeneo yale ambayo nadhani ndiyo ya msingi.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa reli ni moja ya njia nyeti sana ya usafiri duniani kote. Hapa Tanzania, usafiri wa reli ulianza toka wakati wa utawala wa kikoloni wa Ujerumani. Uwekezaji katika miundombinu ya Reli umekuwa ukiaendelea toka wakati huo na mpaka baada ya nchi yetu kupata uhuru. Usafiri wa reli ya Kati unaunganisha mikoa kadhaa hapa nchini na inaunganisha Mashariki na Magharibi ya nchi. Vile vile Kaskazini mwa nchi na upande wa Ziwa.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa reli hapa nchini katika miaka ya karibuni umekuwa na matatizo makubwa sana na hivyo kuleta malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi. Uwezo wa Reli ya Kati kupitia Shirika la Reli Tanzania na sasa Kampuni ya Reli, umepungua mwaka hadi mwaka na hivyo kupunguzia Taifa mapato makubwa. Kwa Mfano, wakati Reli ya Kati ilibeba mizigo ya tani 1,169,000 na kupata mapato ya zaidi ya Tshs. 62 bilioni mwaka 2005, ndani ya mwaka mmoja uwezo wa reli kubeba mizigo

ilipungua kwa asilimia 33 kwa kusafirisha tani 775,281 na kupata Tshs. 46.2 bilioni tu. Takwimu hizi ni kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Uchumi nchini mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, kufuatilia hali hiyo hapo juu, kwa muda mrefu sana kumekuwapo na malalamiko ya wananchi juu ya huduma za usafiri wa reli na malalamiko hayo yamezidi kuongezeka siku hadi siku hata baada ya Shirika la Reli (*TRC*) kukodishwa mwaka 2007 na kuanzisha Kampuni ya *TRL*. Ukodishaji hauonekani kuleta ufanisi na malalamiko yameendelea kuwapo kila siku kutoka kwa watumiaji wa huduma ya Reli. Usumbufu na adha kwa wananchi na hata wafanyakazi umeongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bunge ndio chombo kilichopewa madaraka kwa niaba ya wananchi kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kifungu 63(2) nanukuu:-

*“Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii.”*

Kwa mujibu wa kifungu hiki cha Katiba, Bunge lako Tukufu, kwa niaba ya wananchi linahitaji kufahamu mambo yafuatayo:-

(a) Taarifa kamili kuhusu mchakato mzima wa upatikanaji wa mzabuni uliopelekea Kampuni ya *RITES* kushinda Zabuni ya kukodishiwa *TRC*. Bunge linahitaji pia kujua nani alitoa ushauri wa kukodishwa kwa *TRC*, kwa sababu kuna taarifa isiyo rasmi kwamba Kampuni ya *RITES* ndiyo iliyopewa kazi ya ushauri (*consultancy*) na kuangalia mali za *TRC*, mafanikio au matatizo kama yapo na njia bora ya kuendesha Shirika la Reli.

Baada ya ushauri kutoka kwa Kampuni ya Ushauri, ndipo kampuni zaidi ya nne (4) zilijitokeza na kuomba zabuni ikiwemo kampuni ya *RITES* yenyewe. Kuna Taarifa kuwa kampuni moja ilikwenda Mahakamani na baadaye kuondoa kesi katika mazingira yasiyoeleweka.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, kama msimamizi wa shughuli zote za Serikali, ni vema sasa likapewa taarifa kamili kuhusu mchakato huu ili kuondoa manung'uniko na malalamiko kabla hatujaliingiza Taifa katika mgogoro mkubwa zaidi.

(b) Kwa kuwa Serikali sasa ina asilimia 49 ya hisa, Watanzania wanataka kufahamu Serikali imelipa kiasi gani kwa hisa zake 49 yaani *“paid up capital”* na *RITES* nao wamelipa kiasi gani? *RITES* imeingiza nchini fedha kiasi gani za kwake, kama fedha taslimu au kwa njia ya vifaa na mali ghafi? Je, *initial capital* au mtaji wa kuanzisha kampuni hii, ni kiasi gani na kila mmoja wa wabia yaani Serikali na *RITES* amelipa kiasi gani? Kama fedha zimelipwa kutoka vianzio vya ndani ya nchi, je, fedha hizo ziliidhinishwa na Bunge na kama ziliidhinishwa, ni kutoka kasma gani?

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu wa kawaida, anayekodishiwa ni lazima pia alipie kiwango fulani kama tozo. Ni vyema basi wananchi wakafahamu tozo ya ukodishwaji wa miundo mbinu na vifaa vya Shirika la Reli kwa mwaka ni kiasi gani na inalipwa vipi na inaingizwa katika akaunti gani ya Serikali kwani *TRC* ni mali ya Watanzania na wanastahili kufahamu na kujua mapato yanayotokana na ukodishwaji wa rasilimali na mali zao.

Mheshimiwa Spika, malalamiko haya, kimsingi yanatokana na taarifa iliyotolewa kwenye Kamati ya Miundombinu na Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, kwamba Kampuni ya *TRL* imepewa msamaha wa tozo kwa mwaka mmoja au muda huo umesogezwa mbele kutokana na kilichoitwa hali mbaya ya kifedha katika kampuni hiyo. Iwapo taarifa hii ni ya kweli, je, Serikali inaeleza nini kuhusu suala hili ambalo ni dhahiri linaonekana kwenda kinyume na misingi ya Sera ya Ubinafsishaji na Uwekezaji yaani mwekezaji kuingiza nchini mtaji; vifaa; na teknolojia kama nilivyosema hapo juu?

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ndiyo iliyosaidia kulipa mishahara ya wafanyakazi baada ya wafanyakazi kugoma kama ilivyoripotiwa katika vyombo vya habari. Ni kwa nini mzigo huu unarudi tena kwa Serikali kwa fedha za wananchi wakati sababu za msingi za ubinafsishaji au ukodishaji ni kupunguza mzigo kwa walipa kodi? Hata Fedha za Mdhamana yaani '*Performance Bond*' ambazo walitakiwa kuzilipa kabla ya kuanza kazi, nazo zinasemekana zimesamehewa.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inapelekwa wapi? Hata pamoja na kilio cha Wabunge na Watanzania kuhusu mikataba mibovu, bado Serikali inaelekea imeziba masikio na kuendelea na utaratibu wake wa mikataba isiyojali maslahi ya nchi!

Mheshimiwa Spika, ipo hofu pia kwamba Wakurugenzi wote wa kampuni hii wametoka India na hakuna hata Mtanzania mmoja ambaye amepewa kuongoza Kitengo wakati Serikali ya Tanzania inamiliki asilimia 49 ya Kampuni ya *TRL*. Busara ya kawaida, inataka Serikali ya Tanzania iwe na haki ya kuteua Wakurugenzi katika Managementi ya *TRL*. Watanzania tulio wengi, tukiwemo Wabunge, tuna hofu kuwa, kwa muda wote, kampuni hii itakapokuwa inaendesha *TRL*, itaendelea kupata misamaha ya tozo, haki zetu zitaminywa na wala hatutafaidika na chochote kwani hayuko Mtanzania hata mmoja ndani ya menejmenti mwenye kufahamu mapato na matumizi halisi ya *TRL* wala kinachoendelea ndani ya kampuni hiyo. Jambo ambalo ni hatari kwa mstakabali wa nchi yetu, kiuchumi na hata kiusalama, kama ilivyokuwa kwa Shirika la Ndege *ATC*, ambayo hatukugundua wala kujua chochote hadi ilipoanguka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *TRL* imeshapata mkopo wa jumla ya *USD 77* milioni, bila shaka kwa dhamana na baraka za Serikali yetu yaani kutoka *International Development Agency (IDA)* *USD 33* milioni na kutoka *International Finance Corporation (IFC)* *USD 44* milioni. Bunge lako Tukufu liliwahi kujulishwa kuwa kampuni ya *RITES* itajenga kilomita 645 za reli wakati wa mkataba wake. Hata hivyo, nyaraka zilizoko, zinaonyesha kuwa *TRC* kabla haijakodishwa kwa *RITES* ilikuwa

imeomba kutoka *IDA* na *IFC USD 77* kwa ajili ya ukarabati wa reli kilomita 645, ukarabati wa injini na mabehewa ya abiria na mizigo kama ifuatavyo:-

Injini 90 za kukarabatiwa, behewa za abiria 100 na behewa za mizigo 1,280 hizo zilizokuwa mali ya *TRC*. Kampuni ya *TRC/TRL(?)* wangetoa *USD 34* milioni kufikia *USD 121* milioni zilizokuwa zinahitajika kwa kazi zilizotajwa. Mpango huo ulikuwa umeandaliwa na *TRC* na fedha zilikuwa zimeombwa kwa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, kama taarifa hii ni sahihi, *RITES* wanaelekea kutekeleza tu mpango uliokuwa umeandaliwa na *TRC* na fedha zenyewe zimeombwa na *TRC*. Je, Serikali inalieleza nini Bunge hili kuhusu nafasi ya *RITES* ambayo dhahiri wamedandia mpango uliokuwepo bila wao wanyewe kuleta chochote, wala si fedha, wala si teknolojia, wala vifaa? Je watanzania watakosea wakisema kuwa hapa kuna jambo limejificha na huenda wametapeliwa? *RITES* ni dhahiri anatekeleza mpango uliokuwepo na siyo kwamba anajenga reli kutokana na mtaji wake. Bunge lako Tukufu ni lazima lipate majibu ya kina na sahihi kabisa kuhusu maswali haya mazito na magumu ya Watanzania. *TRC* na sasa *TRL* ni mali ya Watanzania na Serikali haiwezi kamwe kuhodhi na kuficha taarifa muhimu kama hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, zipo kauli zinazopingana kati ya wafanyakazi na wawekezaji (Uongozi) kuhusu vipuri vilivyohamishwa toka Tanzania kupelekwa India. Bunge lako Tukufu, linahitaji kuthibitishiwa uhakika wa taarifa hizi na kama ni za kweli ni vifaa gani vilipelekwa India, vyenye thamani gani na kwa lengo gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na maumbile ya sura ya nchi yetu na kutokana na taarifa za kitaalamu kutoka kwa wataalamu mbalimbali, injini za muundo wa “88 Class” na “89 Class” zilionekana bora na zenye kufaa nchini kwetu. Kampuni ya *TRL* inafahamu vyema ubora huo. Taarifa zinasema kuwa kati ya injini zilizokuwepo 15 baadhi ya injini hizo zimepelekwa nje ya nchi kwa matengenezo. Kwa muda mrefu *TRC* ilikuwa imeandaa wataalam wake yaani mafundi wa kutengeneza injini, karakana bora na ya kisasa iliyoko Morogoro, jambo ambalo linawahakikishia vijana wetu wa Kitanzania ajira. Ni kwa nini injini hizo zimetolewa nje ya nchi badala ya kuzitengeneza hapa hapa nchini, ambapo kama tatizo ni spea na vifaa vingegizwa na kama utaalamu usingetosha, basi wataalamu wachache wangeliletwa kuzitengeneza hapa hapa nchini jambo ambalo lingepunguza gharama, lingesaidia kuongeza ujuzi wa mafundi wa Kitanzania na hata kutoa ajira kwa mafundi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, isitoshe, *TRL* hivi sasa imekodisha injini za muundo wa “73 Class” toka India ambazo ni “*Reconditioned*” pamoja na kuwa ubora wake ni wa maeneo ya tambarare zaidi jambo ambalo halihimili milima na jografia ya maeneo mengi ya nchi yetu. Swali linalotakiwa kujibiwa na Serikali ni je, injini hizo za kukodisha tena za kiwango cha chini, zitaleta tija inayokusudiwa au ni hila, mbinu na hujuma kwa Taifa letu?

Wananchi wanaendelea kudai kwamba injini zilizokodishwa ni za zamani na ni mbovu ambazo zinahitaji matengenezo ya mara kwa mara kama hizi zilizopo nchini zilizokuwa mali ya TRC. Serikali inatakiwa kuondoa hofu hizi za wananchi kwa kutoa taarifa sahihi za kilichotokea hadi kuletewa injini mbovu kama ni kweli tumeletewa injini mbovu. Kama ni kweli, kwa nini hazikukarabatiwa hizi za kwetu badala ya kukodi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa kuwa Wizara ya Miundombinu, Waziri wa Miundo mbinu amesema kwenye Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuwa mkataba utaangaliwa upya (*review*) baada ya miaka mitano, huu ni muda mrefu sana kwa kampuni ambayo imeanza kufanya kazi wakati Watanzania hawafahamu hata mtaji wake tena imeanza kazi ikiwa na matatizo mengi.

Mheshimiwa Spika, ili utata huu uweze kuondoka, ni dhahiri kuna haja ya kupitia mkataba wenyewe uliokodisha TRC kwa TRL/RITES. Lakini si mkataba tu, kuna haja ya kupitia nyaraka mbalimbali kama vile mikataba yote inayohusika na fedha zilizokopwa kutoka IDA, IFC na masharti yake, kuangalia mchakato wa zabuni, kupata kumbukumbu mbalimbali za vikao vilivyohusika kuidhinisha taratibu mbalimbali zilizotumika, mambo ambayo kwa utaratibu wa kawaida, si rahisi kupatikana isipokuwa kwa kutumia mamlaka ya Bunge yanayotolewa kwa Kamati Teule ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, baada ya kuyasema haya yote, ni dhahiri kabisa kuwa Serikali ndiyo iliyohusika na mchakato mzima wa mkataba kati yake na Kampuni ya RITES na kwa kuwa mkataba huo umezalisha maswali mengi yenye utata na kwa kuwa hakuna mtu anayeweza kujichunguza na kujihukumu mwenyewe, kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge, Kifungu cha 117(1), Toleo la 2007, Bunge lako Tukufu sasa likubali kuunda Kamati Teule kuchunguza utata uliojitokeza katika mchakato mzima unaohusisha suala hili kabla Taifa halijatumbukia katika tatizo kubwa zaidi kutokana na mkataba tata na unaoonekana dhahiri kutokuwa na maslahi kwa Taifa letu tofauti na Serikali inavyotaka Watanzania tuamini.

Jambo hili linaathiri sehemu kubwa ya Watanzania wanaotumia njia ya Reli ya Kati kuanzia Dar-Es-Salaam hadi Kigoma, Tabora – Mwanza na Tabora- Mpanda. Lakini hata Watanzania wasiotumia njia hii, huathirika vile vile kwa vile fedha zinazotumika ni mali yao na wanachangia katika kila kitu kuihudumia reli hii, ikiwa ni pamoja na kulipa mikopo ya Benki ya Dunia ambayo TRL imekopa kwa niaba yao, japo hata wao wenyewe hawakujulishwa na wala wawakilishi wao yaani Wabunge hawakupewa taarifa ya kuridhisha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninarudia kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa kunipa nafasi hii ya kutoa hoja yangu hii. Ninatoa pia shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kukubali kunisikiliza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, sasa naomba nisome azimio, chini ya Kanuni ya 54(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007.

**KWA KUWA** Shirika la Reli Tanzania (*TRC*) lilikodishwa kwa Kampuni ya *RITES* ya India mwaka 2007 na kuanzisha Kampuni ya *TRL*;

**NA KWA KUWA** ukodishaji huo mpaka sasa haujaonyesha ufanisi zaidi ya huduma kuzorota hivyo kusababisha adha kwa watumiaji wa reli hiyo na pia kuwepo malalamiko mengi ya wafanyakazi kuhusu shirika hilo linavyoendeshwa hata kufikia kufanya migogo ya mara kwa mara;

**NA KWA KUWA** kitendo cha Serikali kutoa fedha za kulipa mishahara ya wafanyakazi wa Shirika hilo kumewafanya Watanzania wajiulize ni kwa nini mzigo wa kuliendesha shirika hilo unarudi tena kwenye Serikali na fedha ya walipa kodi zinaendelea kutumika wakati lengo la kulikodisha lilikuwa ni kuwaondolea walipa kodi wa nchi hii mzigo huo;

**NA KWA KUWA** kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya (63)(2) ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Sura ya Pili, Toleo la 2002, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo chombo kikuu chenye madaraka kwa niaba ya wananchi ya kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake;

**KWA HIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba Serikali lifanye yafuatayo na kutoa taarifa ya utekelezaji kwenye Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge.

(i) Kuangalia mkataba wa ukodishaji wa Shirika la Reli kwa Kampuni ya *RITES* ili kuondoa dosari zote zilizopo kwa maslahi ya Taifa.

(ii) Kwa kuwa Serikali inahisa 49 na Kampuni ya *RITES* ina hisa 51, Menejimenti ya Shirika hilo iwe na uwiano sawia kati ya Watanzania na wakodishaji hao na kwa kuwa Stesheni na magenge mengi yamefungwa, zichukuliwe hatua madhubuti za kuhakikisha usalama wa reli na vyombo vyake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Arfi. Kwanza, napenda kukuhakikishia kwamba hotuba yako yote, ile hoja, itaingia kwenye *Hansard* kwa jinsi ulivyoitayarisha, sio huo muhutasari uliutoa hivi sasa.

Waheshimiwa Wabunge, nimepata wachangiaji watano katika hoja hii na kama kwa ile ya kwanza, kama wataweza kufupisha itakuwa bora ili baadaye Naibu Waziri wa Miundombinu aingie na kuchangia kuhusu hoja hii.

Sasa nilionao hapa ni Mheshimiwa Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Tatu Ntimizi kwa mpangilio huo.

Sasa ninayo nafasi ya mchangiaji wa kwanza kuanza, kwa hiyo namwita Mheshimiwa Juma Kaboyonga.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwaza ya kuchangia hoja binafsi ya Mheshimiwa Arfi kuhusu uendeshaji wa kampuni ya Reli, *Tanzania Railways Limited (TRL)*.

Mheshimiwa Spika, wakati anaitoa hoja yake nimekuwa nikimfuatilia wala sina nakala ya hoja yake na kwa maana hiyo sitaweza kuzijibu kwa mtiririko kama alivyozitola lakini mchango wangu nataka uwe wa ujumla.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijaendelea, napenda niseme dhahiri na wazi kabisa kwamba mimi ni Mkurugenzi katika Shirika la Reli la Tanzania nikiwakilisha Serikali ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kwamba Serikali imekodisha miundombinu ya reli kwa Kampuni ya *Tanzania Railways Limited* ambayo wadau wake ni Serikali ya Tanzania kwa hisa 49 na *RITES* ya India kwa hisa asilimia 51. Huyu *RITES* ndiyo mwekezaji kiongozi yaani *Strategic Investor*. Aliyoyasema mtoa hoja mengine yamekosa mwelekeo mzuri kwa maana anasema kampuni hii imekodishwa toka mwaka 2007 lini? Maana leo ni Aprili 2008, angesema imekodishwa 2007 lini.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa uhakika ili kuziba hilo pengo ni kwamba Kampuni ya *TRL* imeanza kufanya kazi na kukodishwa miundombinu ya reli tarehe 1 Octoba, 2007. Kwa maana hiyo, mpaka kufikia leo hii tunapozungumzia hoja hii, tuna miezi sita tu ya ukodishwaji. Ni kipindi kifupi sana kwa *standard* zozote kutoa lawama kwamba hakuna *performance*.

Mheshimiwa Spika, kilichofanyika ni nini? Kwa kifupi ni kwamba Serikali wakati inataka kukodisha miundombinu ya reli, iliunda kampuni inayoitwa *RAHCO, Rail Asset Holding Company*, ikaipa majukumu ya kuwa ndiyo mdhibiti na msimamizi wa mali zote za Shirika la Reli kwa maana ya reli hizi ambazo ni injini na mabehewa yanayotembea juu yake na mali zote zikawekwa chini ya kampuni inayoitwa *Rail Asset Holding Company* ambayo kwa asilimia 100 ni mali ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kilichokodishwa ni kutumia reli kuendesha biashara ya usafirishaji mizigo pamoja na abiria. Lakini mkataba ulitoa nafasi kwa kampuni inayokodishwa kutumia vifaa vilivyokuwa vya Shirika la Reli kwa maana ya injini, mabehewa na baadhi ya wafanyakazi watakaokuwepo. Sasa vifaa hivi kwa maana ya mabehewa na injini ambavyo vimepewa kampuni hii ya *TRL* kuvitumia ili kufanya kazi ya kusafirisha mizigo na abiria vingi vyao, ni vibovu. Vilikutwa vibovu tena vibovu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kazi ya awali ya kampuni hii iliyokodishwa ni kuanza kutengeneza mabehewa na injini na ndiyo maana mtoa hoja anasema kuna mikopo kutoka *World Bank, IDA, Dollar 33*, milioni na *IFC- International Finance Company Dollar 44* milioni, ni kweli. Lakini *Dollar 33* zinakuja kwa ajili ya kutengeneza

reli na kwa maana hiyo zitatumika kwa ajili ya kuboresha reli yetu. *Dollar* 44 milioni zinakuja kwa ajili ya kutengeneza vitendea kazi vikiwemo injini, mabehewa yote ya mizigo na ya abiria. Sasa kazi hii ndiyo imeanza kwa maana ya kutoa *tender*, kufanya *assessment* ya *repairs* zinazotakiwa kufanya na kuagiza vipuri.

Mheshimiwa Spika, *time lead* ya kuagiza vipuri na kuvipata haiwezi kuwa miezi sita tu. Viko vipuri vitachukua miezi tisa mpaka mwaka mmoja kupatikana. Sababu ni nini? Sababu kubwa ni kwamba reli yetu ni ya kizamani, reli hii upana wake ni mita moja. Katika dunia ya uendeshaji wa reli, reli yetu hii ni moja ya reli zilizo kongwe ambazo si sehemu nyingi duniani zipo. Kwa hiyo vifaa vyake vinavyotumika kwa maana ya mabehewa na injini zake kwa leo hii huwezi kuvipata dukani. Huwezi kwenda *workshop* ukamwambia nipe injini hiyo nipeleke Tanzania au ukawaambia nipe behewa lile nipeleke Tanzania, hakuna *workshop* zinazotengeneza injini pamoja na mabehewa yanayoendana na upana wa reli yetu kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kinachofanyika sasa ni nini? Ukitaka kitu kipya inabidi utoe *order* na unapotoa *order* kule kwenye *workshop* si wewe peke yako unayetoa *order* wapo na wengine wanaokutangulia. Kwa hiyo, ukitaka injini mpya si chini ya miaka miwili kuipata na mabehewa hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa tunafanya nini? Uamuzi uliopo ni kuvikarabati vilivyopo. Mtoa hoja amesema injini nzuri ni zile za *class* ya 88 na 89, ni kweli. Lakini aende Morogoro akaangalie ni injini ngapi za *class* ya 88 na 89 zinafanya kazi na ziko katika hali gani? Ziko katika hali mbaya sana na ili ziweze kufanya kazi, ndiyo maana huu mkopo wa *IFC* umetafutwa na leo hii haujapatikana kwa maana ya kuwa *disbursed* kwa sababu *conditional precedent* ya ku-*disbursed* ule mkopo, hazijakuwa tayari. Ndiyo maana nikamuuliza anasema mwaka jana ndiyo reli imekodishwa mpaka leo utendaji mbaya, atafute sababu ni nini? Sababu ni kwamba vile vitendea kazi havijatengemaa ili kuweza kufanya kazi kama ilivyokusudiwa. Taratibu zinafanywa kuvitengeneza.

Mheshimiwa Spika, ninachomwomba mtoa hoja awe na subira mipango ipo mbioni kutengeneza hizo injini za *class* ya 89 pamoja na kutengeneza mabehewa lakini inachukua muda, si jambo la kupewa juzi, leo kila kitu kiwe tayari, haiwezekani. Ni *over simplification*. Hoja hii ame-*over simplify* sana, ina mwelekeo mzuri wa kutaka kuleta changamoto kwamba tufanye kazi kwa haraka kwa sababu reli tunaihitaji, ni kweli na mimi nasema tunaihitaji sana tena sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana Serikali ikaamua kuikodisha kwa sababu yenyewe kama Serikali haikuwa na uwezo, nirudi nyuma. *PSRC* ambayo ndiyo ilisimamia ukodishwaji wa Shirika letu la reli ilikaa na Shirika la Reli ikitafuta mwekezaji kwa takribani miaka kumi likingojea kubinafsishwa. Muda wote huu hakuna uwekezaji wa namna yoyote uliowekwa ndani ya Shirika la Reli.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa mtoa hoja anasema Serikali imeisaidia kampuni kulipa mishahara, kwa upande wa Serikali hii si hoja ngeni. Kabla ya kukodishwa, Serikali ilikuwa inapeleka pesa za kulipa mishahara lakini leo kwa mishahara ule wa



shilingi 80,000 kwa kima cha chini ambao ulikuwepo na ndiyo mwekezaji alikuwa akijua kima cha chini cha mshahara ni Sh.80,000 mpaka 87,000 alishaumudu huo na hakuhitaji msaada wa Serikali. Serikali imekuja kuingia kwa sababu ilipobadilisha kima cha chini cha mshahara kutoka Sh.80,000 mpaka 200,000 ika-*throw out of gear* mipango yote ya kampuni hii kwa sababu wao walikuja wakijua mshahara wa kima cha chini ni Sh.80,000.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakati kampuni inarekebisha na kuangalia tutapata wapi fedha za ziada na kwa kuwa haikuwezekana kuzipata fedha za ziada haraka kama zilivyotakiwa, ndiyo maana Serikali kama mbia akaingia kusaidia kuziba pengo lililojitokeza la upandaji wa mishahara wa haraka kutoka Sh.80,000 mpaka Sh.200,000, ndiyo sababu hiyo lakini kadri siku zinavyokwenda na mazungumzo yanaendelea kufanywa baina ya kampuni na Serikali, tunafanya nini juu ya huu mshahara mpya wakati uwezo wetu sisi ni mdogo. Basi huko mbele tutaona na Serikali kutoa msaada katika kampuni si ajabu kwa sababu yeye yenyewe ni mbia, haiwezi ikaacha kampuni yake inaanguka ati kwa sababu *RITES* yupo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitarejea yale ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu aliyosema juu ya *Air Tanzania* kwamba kuna habari nyingine, alitumia neno umbea kwa sababu maneno haya yanayozungumzwa hayafanyiwi utafiti wa kutosha. Sasa kwa sababu hayafanyiwi utafiti wa kutosha, linakuja jambo kwamba vipuri vimechukuliwa, vimepelekwa India thamani yake hazijulikani, sijui vitakuaje.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba *RITES* ina mahusiano makubwa na *Indian Railways* ya India. *Indian Railway* ina *workshop* kubwa sana kuliko mnavyoweza kufikiria. Wana uwezo mkubwa sana. Sasa kama sisi wenyewe hatuwezi kuzitengeneza hizo *spares* hapa Morogoro na Dar es Salaam na kwa kuwa yeye ni mshirika katika kampuni hii, inawezekana kabisa kwamba zipo aina fulani ya *spares* zinapohitajika kutengenezwa basi zinapelekwa *Indian Railways workshop* ili zitengenezwe na baadaye zirudishwe. Sasa kuna tatizo gani katika hilo kama taratibu za kupeleka na kurudisha zimefuatwa sawasawa.

Mheshimiwa Spika, Shirika linakodisha injini za *73 class* ambazo hazina nguvu. Ni kweli hizi injini hazina nguvu kama injini za *88 na 89 class* lakini sababu ni kwamba hatuna injini kabisa. Sasa tunafanya nini? Tusimame tu, tutangojea mpaka lini? Kwa kuwa huyu mbia ana mahusiano na *Indian Railways* na kule zipo injini *in fact* zimeletwa kwa utaratibu wa ku-*lease*, hatujanunua hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zitakapomaliza muda wake za kuwa *leased*, kitu unapoki-*lease* sio lazima kiwe kipya ili mradi kina kuwa *reconditioned* kuja kufanya kazi iliyokusudiwa kufanyika na mkataba umetoa maelekezo kwamba kama hiyo injini ikiwa hapa, itakapokuwa *off duty* kwa sababu zimeharibika, kipindi kile hakichajiwi na hizi zinakuja zikiwa na mafundi na *spares* za uhakika ambazo zinakuwa *consumed on regular basis*, hizo zipo kabisa, wameshakuja nazo na wao ikiharibika wanatengeneza hapo hapo. Katika maeneo ambayo injini hizi haziwezi kwenda peke yake kwa sababu ya *ingredient*, utaratibu unafanywa wa kuzifunga mbilimbili na kama haina budi hata tatu ili mradi mzigo uende wakati tunasubiri zile injini kubwa kutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, mipango ya baadaye, ni pamoja na kununua injini kubwa ya class 2,300 kutokana na mipango hiyo, hizo injini kubwa zikija mambo yatakuwa mazuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia hauniwezeshi kumwita mchangiaji mwingine. Niseme tu kwamba huyu mchangiaji aliyemaliza sasa hivi, ningejua kwamba mchango wake ni wa kujibu hoja, ningemsogeza baadaye kidogo kwa sababu ingekuwa ni vizuri zaidi tusikie wale ambao hawahusiki moja kwa moja kimaslahi na *TRL* lakini si kitu.

Wachangiaji waliosalia, niwatamke ili saa kumi na moja wajiandae, nao ni Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Mheshimiwa Susan Lyimo. Kwa hiyo, saa kumi na moja jioni tutakwenda kwa mpangilio huo hapo.

Kwa sasa kwa kuwa muda wa kusitisha shughuli za Bunge umefika, nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

*(Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotangaza tulipositisha shughuli pale saa 7.00 mchana, wachangiaji wangu ni watatu. Ninawaomba sana waokoe muda. Nisingependa baadhi ya hoja hizi, zishindikane kuwasilishwa Bungeni, ikajenga hisia kwamba, labda hoja husika imepigwa chenga. Kwa hiyo, ninae Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Mheshimiwa Susan Lyimo. Tutaanza na Mheshimiwa Ponsiano Nyami.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze na mimi kutoa mchango kidogo. Kwanza kabisa, lengo la kukodisha reli yetu ni kuboresha zaidi katika kutoa huduma kwa wananchi. Hilo ndilo lilikuwa lengo, lakini vilevile kuhakikisha kwamba, tunakuza uchumi wetu na hasa kuboresha reli yenyewe katika suala zima la usafirishaji wa bidhaa zetu. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuhakikisha kwamba, Mkataba ambao upo, uwe ni mkataba ambao unaweza kutekelezeka na kama ulikuwa na upungufu wa hapa na pale, basi upungufu huo uweze kurekebishwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, mkataba huo, ninaomba sana usiwe unabagua. Mkataba ambao kama tunavyoona, una asilimia 51 za huyo mwekezaji na asilimia 49 za Serikali, kwa hiyo, bado ni mali ya wananchi. Katika mkataba huo lipo eneo linalozungumzia reli yenyewe, lakini mwekezaji amepewa eneo fulani. Ningeomba usiwe wa kibaguzi kwa sababu kama hautaweza kutengeneza maeneo mengine ni vizuri tukajua ni maeneo yepi

ambayo amepewa. Tutajikuta watu wa Mkoa wa Rukwa ambao tunategemea reli zaidi kutuunganisha na Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Tabora, tutakwama. Kwa hiyo, kama eneo hilo hajapewa mwekezaji kulishughulikia ni vizuri Serikali iweze kulishughulikia kikamilifu. Vilevile maeneo kama vile kutoka Manyoni hadi Singida, nayo yanaweza yakasahaulika.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna fununu ninaomba nizifahamu na hasa atakapokuwa anajibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu kwamba, reli ile ya kwenda Mpanda kutoka Kaliua na ile ya kutoka Manyoni kwenda Singida, zitaweza kusimamishwa kufanya kazi au pengine hata kung'olewa. Hili likoje? Ninaomba mtuweke wazi mapema. Pia utengenezaji wa injini zetu na mabehewa usiwe tu ule wa kupeleka India wakati wote, karakana zetu zile zilizoko Morogoro, Dar es Salaam na Tabora, ziweze kuimarishwa kikamilifu ili ziweze kufanya kazi kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo; ni wazi matatizo ya kazi huwa yako kila mahali. Hivi karibuni tunaona kwa mfano, watumishi wale wa reli waligoma. Mimi nilikuwa ninajaribu kuwaasa wajaribu kuona ukweli uliopo katika shirika lao, kule walikotoka na pale walipo leo. Wakati anakuja huyu mbia, wao kama watumishi wazalendo Watanzania, walikuwa wamelifikisha wapi; je, walikuwa wamefanya vizuri au wamefanya vibaya hadi wakati mkataba unasainiwa? Walimkabidhi huyu mbia na ile hisa iliyobakia ya Serikali shirika likiwa katika hali gani kuanzia mabehewa yale ya kusafirisha watu, pamoja na yale ya mizigo na vichwa vya kusafirisha mabehewa hayo, vilikuwa katika hali gani? Wao ndio walikuwa na dhamana ya kusimamia kama wazalendo mali yao wenyewe; walikuwa wameendesha vizuri si suala la kulalamika tu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia wajaribu kutazama, kuna hujuma zilizokuwa zinafanyika na nani? Kwa mfano, ile ajali ya mwaka 2003, ambayo iliua watu wengi sana na wengi wakazikwa hapa Dodoma. Je hujuma kama zile zinafaa? Wasiwasi wangu ni kwamba, kwa sasa hivi wanapokuwa wamefunga baadhi ya magenge na baadhi ya stesheni, kutakuwa na umbali mrefu sana wa treni kutembea bila kuwa na stesheni wala magenge yale ya kuhudumia reli. Inawezekana kabisa hujuma zikaongezeka, nalo hilo kiusalama ni la kulitazama. Suala la usumbufu kwa wananchi, nalo hili litazamwe ili wananchi wasipate usumbufu zaidi; je, lipo kwenye mkataba kwa kufunga vitu kama hivyo?

Mheshimiwa Spika, umetuambia tuongee kwa kifupi sana, nimeongea kwa dakika nne. Ninaomba niache kuongea ili na wengine waweze kuongea. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ninakushukuru Mheshimiwa Ponsiano Nyami. Sasa ninamwita Mheshimiwa Josephine Genzabuke, atafuata Mheshimiwa Susan Lyimo, baadaye Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia fursa hii nami niweze kuungana na wenzangu katika kujadili hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi ya kwangu ni machache. Tangu Shirika la Reli lilipobinafsishwa, likakodishwa akachukua huyu ambaye sasa hivi ndiye analiendesha, yametokea matatizo mengi sana. Mimi nitazungumzia matatizo wanayoyapata wananchi baada ya Shirika hili kuchukuliwa na huyo ambaye analiendesha hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanapata shida sana. Kilichonifanya nisimame jioni hii ni huruma inayonifanya mimi kama mwanamke, kuwaona wanawake wanalala stesheni na watoto kila wakati na mpaka sasa hivi ufumbuji hakuna. Treni ilikuwa inafanya kazi mara nne kwa wiki, sasa hivi ni mara mbili. Ukiangalia mazingira ya sasa baada ya kuwa treni inafanya kazi mara mbili kwa wiki, behewa linalobeba watu 80, linabeba watu 150. Kiti kile kimoja, utakuta wamezidisha watu mara mbili, yaani watu wamekaa mpaka migongoni, ukiweka mguu, hakuna kutoa. Kule chooni ndiko abiria wanakoenda; ni nani anayependa kusafiri akiwa chooni? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukienda mahali pale kuangalia, machozi yanatutoka! Chakula cha shida; mtu amepanga safari yake, ametoka maeneo ya vijiji vya mbali, labda anatoka Wilaya moja kwenda nyingine, ambako ndiko treni inakoanzia safari; treni haianzi safari siku hiyo, wanasema kwamba treni itaanza safari kesho yake au kesho kutwa, wanalazimika kulala stesheni, hawana chakula, hawana maji, wanaugua na dawa hawana. Ninashauri Serikali ilianganalie hili kwa sababu wale wanaoteseka ni Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia mazingira yenyewe ambayo treni inapita sasa hivi, kutokana na wafanyakazi tuseme labda walikuwa tisa, lakini wamepunguzwa, wanabakia watatu, wanashindwa kufanya kazi zile ambazo watu tisa walikuwa wakizifanya, wanabakia watatu. Wanashindwa hata kuwashikia nyundo wenzao wakati reli inapokuwa imeharibika. Vilevile majani unakuta yamefungana, njia ile ambayo treni inapita. Tulianganalie hilo, wanashindwa kuendesha huduma zile za njiani, sasa treni itakuwa inapitaje wakati majani yamefungana njiani? Si hilo tu, kuna wananchi wanaoishi njiani wanapata shida. Siku hizi ukienda hapo stesheni, hakuna mizigo kwa sababu watu hawana uhakika na treni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili nalo tulianganalie, huduma ya watu wale wanaoishi njiani, siku hizi hakuna. Hakuna asiyefahamu watu wa Reli ya Kati, kwa maana ya Ukanda wa Ziwa na Magharibi kwamba, sisi njia yetu kubwa ni usafiri wa reli. Kitu hicho hakuna na si kwamba, Serikali haioni, inaona. Pamoja na ufinyu wa hali yenyewe ya kipesa, lakini wajaribu kutupia macho waanganalie, tuwahurumie wale watu wanaoishi mazingira ya namna ile.

Mheshimiwa Spika, nitaenda haraka haraka. Kuhusu usafiri wa mizigo, sasa hivi kutokana na jinsi mtu mwenyewe aliyechukua reli hiyo, ninaweza kusema kwamba, siyo mkweli. Mwaka 2007 mwezi Novemba, nilisimama hapa kuuliza swali kwamba ni kitu gani kilichosababisha kusitisha treni kuanzia Dar es Salaam mpaka Dodoma, badala take ikaanzia Dodoma mpaka kwenda Mikoa ya Mwanza, Kigoma na Rukwa?

Mheshimiwa Naibu Waziri alinjibu kwamba, kufikia mwezi Machi, tatizo hilo litakuwa limekwisha, watakuwa wamerekebisha njia ya reli na watakuwa wameongeza mabehewa. Kwa hiyo, hakuna tatizo lolote litakalokuwa linajitokeza, kila kitu kitakuwa tayari. Tangu mwezi wa tatu, leo tunaingia mwezi wa tano, zaidi ya miezi miwili, hakuna lolote.

Mheshimiwa Spika, mabehewa ya kubebea mizigo imekuwa tatizo. Utakuta wale wafanyabiashara sasa hivi wamekwishaachana na njia ya reli kabisa, wanaenda kwa njia ya barabara. Si kwamba wanapenda, wangependa kutumia njia ya reli, lakini kwa sababu mabehewa hayapo, ndiyo maana wanalazimika kusafirisha mizigo yao kwa kutumia magari. Vilevile ucheleweshaji wa mizigo yao, ndiyo sababu ya wao kulazimika kutumia malori.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaishi Mkoa wa Kigoma, kutokana na tatizo hili la ukosefu wa mabehewa, mwezi wa kwanza na wa pili, bei ya mafuta Kigoma Mjini, Kasulu na Kibondo, lita moja ilikuwa shilingi 3,000, kwa sababu mabehewa yalishindwa kusafirisha mafuta kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma. Sasa ninauliza, huyu mwekezaji atatufikisha wapi?

Mheshimiwa Spika, si hilo tu, Mheshimiwa Nyami amesema, lakini na mimi ninalazimika kusema tena kuwa, uchumi wa nchi hii unaathirika kutokana na ukosefu wa mabehewa na miundombinu ya reli. Sasa hivi watu wa *DRC*, hawapitishi tena mizigo yao huku kwetu, wanapitishia Kenya.

Pamoja na matatizo yaliyoko Kenya, wanapitishia huko, inaingia Rwanda, ikiingia Rwanda, inafika *DRC* wakati mwingine inaenda mpaka Zambia. Sasa hatuoni kama sisi wenyewe tunajinyima haki zetu? Uchumi wetu sisi tunaacha kuuboresha, tunaenda kuboresha wa nchi jirani!

Mheshimiwa Spika, niombe kuikumbusha Serikali, matatizo haya yanayojitokeza, waende kuyaangalia ili wananchi wasinung'unike kwa sababu ya ukosefu wa huduma hii.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Waziri alipoteuliwa, Mkoa wa Rukwa walifurahi na ninaomba nimwambie kwamba, hata Kigoma walifurahi, walisema sasa na sisi tutaponea hapo hapo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakuomba na ninajua ninapozungumza hapa na wewe ninakusemea kule Mpanda. Tunaomba kabisa suala hili la reli liangaliwe upya; ile mikataba kama haipo vizuri, iletwe tena iangaliwe upya, ndiyo ushauri wangu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitolee mfano mdogo tu wa Vituo hivi vya njiani. Mimi huwa ninasafiri kwa treni kutoka Kigoma mpaka Dar es Salaam. Kuanzia Dodoma mpaka Morogoro hapa kati kati kuna Vituo; Kilosa na Kimamba. Hawa wananchi wa maeneo haya, wamekuwa wakifanya biashara kati ya watu wa Morogoro na watu wa Dodoma. Watu wa Dodoma wanapeleka bidhaa zao Morogoro au kwenye vijiji vile vilivyopo katikati. Hivi sasa kwa sababu huduma hiyo ya reli imekuwa ni ya kusuasua, mawasiliano yamekatika. Tuwahurumie ndugu zetu wale, ambao wapo

pembeni ya reli ili na wao waweze kunufaika, waweze kuendesha biashara zao kwa kupitia njia ya reli.

Mheshimiwa Spika, sisi watu wa Kigoma reli ni kilio chetu kikubwa sana, kwa sababu bila reli hatuna njia nyingine ya usafiri. Daraja la Malagarasi halipo, miundombinu ambayo ni mizuri ambayo tunaweza tukasafiri kwa kutumia barabara nayo hakuna. Sasa kwa nini sisi tunaachwa kisiwani; hatuwezi kuhama kwa sababu kule mipakani si mnajua, watu tunaishi lazima tulinde mpaka? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali ilianganalie upya jambo hili ili iweze kumaliza matatizo ya wananchi. Baada ya kusema hayo, ninaomba kukushukuru na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuwa msemaji wa mwisho katika hoja hii iliyoletwa na Mheshimiwa Arfi, kuhusu uwekezaji katika shirika letu la reli na kampuni ya *RITES* ya kutoka India.

Mheshimiwa Spika, ninaamini sote tunaelewa umuhimu wa reli na tunajua kwamba, katika nchi zote zilizoendelea ulimwenguni, wametumia zaidi reli katika maendeleo yao, hususan katika kusafirisha mizigo. Ni jambo la kusikitisha kuona kwamba, hapa Tanzania reli haitumiki, imeharibika na ndiyo sababu imekuwa sasa hivi makontena yetu mengi yanatumika katika nji ya barabara na hivyo kuleta uharibifu mkubwa sana katika barabara, hasa tukiangalia katika Mto Ruvu na katika sehemu nyingi za barabara zetu, zinaharibika kwa sababu zinabeba mizigo mizito ambayo ingepaswa kubebwa na reli.

Mheshimiwa Spika, suala la uwekezaji au ubinafsishaji, linakuja kwa lengo la kuboresha huduma. Kwa hili la *RITES*, ninaomba nitofautiane kabisa na msemaji wa kwanza hasa kwa yale aliyoyazungumza. Tukiangalia reli ya Kaskazini kutoka Dar es salaam - Tanga - Arusha, madhumuni yake makubwa yalikuwa ni kubeba mazao mbalimbali, ikiwa ni pamoja na saruji kutoka Tanga, lakini pia na mbolea kutoka Arusha, kwenye kile kiwanda cha Minjingu. Si hivyo tu, tukichukulia suala la Reli ya Dar es Salaam - Tanga, utagundua kwamba, Tanga kuna Bandari na ile Bandari ni muhimu sana na kwa hiyo, ile reli ingesaidia sana kupunguza tatizo la makontena Dar es Salaam, mengine yangeweza kubebwa kutoka Tanga.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli ulio wazi kwamba, hili shirika pamoja na kwamba, hii kampuni mpya imekwishalichukua miezi sita, bado hatujaona utendaji wake. Tanzania ni nchi ambayo imebarikiwa sana kuwa imezungukwa na nchi sita ambazo ni *landlocked*. Kwa maana hiyo, kuwa kwetu kati ya nchi hizi sita, kungetusaidia sana katika kuboresha uchumi wetu na hivyo kuwa na maendeleo makubwa sana katika Afrika. Hakuna nchi nyingine ya Afrika, ambayo imeweza kuzungukwa na *landlocked countries* sita. Utaona kwamba, kwa sababu nchi hizi nyingi pia zinatumia Bandari ya Mombasa, pamoja na kwamba, Kenya ilikuwa kwenye matatizo makubwa wakati wa uchaguzi wa mwezi Desemba mpaka mwezi Machi, bado Tanzania tumeshindwa kabisa

kutumia fursa hiyo na kwa hiyo, tukaachia Kenya waendeleo kusafirisha mizigo ya nchi hizi ambazo zimeizunguka Tanzania.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninataka kulizungumzia ni kwamba, pamoja na kufunga njia ile ya reli kutoka Dar es Salaam - Tanga, sasa hivi hakuna watu wanaoangalia zile reli na matokeo yake, mataruma yale ya reli yameng'olewa na wiki iliyopita, tumeona kwenye vyombo vya habari, jinsi gani wafanyabiashara wa vyuma chakavu wameweza kutumia mataruma yale kufilisi au kuhujumu uchumi wa nchi hii. Kwa hiyo, ninaamini kabisa, kama mwekezaji huyu angekuwa makini ni wazi kwamba, huduma zingeborehwa na siyo zingelitishwa kama ilivyo sasa hivi kwamba, reli hizo hazifanyi kazi na kama zinafanya kazi basi ni kwa kiwango duni sana.

Ndiyo sababu Mheshimiwa Josephine Genzabuke ameongezea kwamba, ilikuwa reli hii ya kati ambayo ninaamini wananchi wa Ukanda huu wa Kati wanaitegemea sana kwa asilimia 90, kwa sababu miundombinu ya barabara ya kawaida ni mibovu. Kwa hiyo, nilikuwa ninategemea kabisa reli hii kwa wakati huu imechukuliwa na mwekezaji, basi ingekuwa nzuri zaidi ili wananchi wa ukanda huo, waweze kufaidi safari zao na vilevile mazao yao.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye suala la mazao, utaona kwamba, Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini; Mikoa ya Rukwa, Ruvuma na Mbeya ni Mikoa ambayo tunaiita *The Big Three*, kwa maana ya kwamba, inazalisha kwa kiasi kikubwa sana. Ni ukweli ulio wazi kwamba, lazima Tanzania tuweze kuondoa umaskini na njia mojawapo ya kuondoa umaskini ni kumsadia mkulima. Wakulima wa Tanzania wamejitahidi sana kulima na wanavuna mazao mengi, lakini kutokana na tatizo kubwa la usafiri, hususan Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini, unakuta wafanyabiashara wanatoka Dar es Salaam kwenda kuchukua mazao hayo kwa wakulima. Kule wanachukua gunia moja kwa mfano la mahindi kwa shilingi 5,000 hadi 10,000, wanalifikisha Dar es Salaam, wanaliuza kuanzia shilingi 50,000.

Vilevile kwa mazao kama maharage na mchele, kwa hiyo, unakuta wakulima wetu kwa kweli wanajitahidi vya kutosha, lakini kutokana na miundombinu mibovu ya reli, wameshindwa kusafirisha mazao yao na hivyo, wafanyabiashara wakubwa wamekuwa wakiwanyonya. Kwa hiyo, ninadhani ni muhimu sana kama mkataba huu una matatizo yoyote, basi uboreshwe ili reli ya kati iweze kufanya kazi kama ilivyokuwa inafanya siku za nyuma na Wananchi wa Tanzania, hususan wa upande huo, waweze kusafiri kama ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, kuna suala hili ambalo limeongelewa sana na Mheshimiwa Arfi, hasa suala zima la vipuri. Ni jambo la kusikitisha kuona kwamba, vipuri vinatolewa Tanzania kupelekwa India. Msemaji wa kwanza ali-*support* hilo. Sisi tunajiuliza, *value for money* iko wapi? Inawezekanaje vipuri vya tani nyingi, vipolekwe nje wakati tunaweza kabisa kuwasafirisha hawa wataalam waje wafanye kazi hizo hapa? Tuna karakana kubwa pale Morogoro na tunaamini hiyo ingekuwa njia moja ya kupunguza tatizo la ajira kwa vijana. Kwa hiyo, suala la kupeleka vipuri vyetu kule kwenda

kutengenezwa na watu wa India, ninadhani tunawakosesha haki ya ajira wananchi wetu wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna suala lilijitokeza wiki kama tatu zilizopita, suala zima la marupurupu au mishahara ya wafanyakazi. Limezungumwa kwa kirefu na sote tuliona, lakini pia nimeshangaa kusikia kwamba, kwa kuwa Shirika hilo ni la Watanzania, basi Serikali ilikuwa na wajibu wa kuwalipa mishahara. Mimi sikubaliani na hilo kwa sababu sasa shirika hilo limebinafsishwa, kwa hiyo, lilikuwa ni jukumu la hao wawekezaji, kuona ni jinsi gani watawalipa, kwa sababu naamini katika ule mkataba toka mwanzo waliposaini kulikuwa na makubaliano ya jinsi gani watawalipa mishahara na jinsi gani wataliendesha hili shirika. Haiwezekani Serikali iendelee kuwalipa wafanyakazi, wakati tayari shirika hilo limebinafsishwa. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Naibu Waziri, anapokuja kujibu atueleze ni kwa kiasi gani, Serikali imelipa hizo pesa na zimetoka wapi wakati sisi tunajua Bungeni hapa hatujapitisha? Kwa hiyo, tunaomba kujua Serikali inapata wapi hela za kuwalipa mishahara wafanyakazi hao, wakati tunajua shirika hilo limebinafsishwa?

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, ninapenda kujua suala zima la kusitishwa kwa huduma za reli na ni jinsi gani wananchi wetu wameweza kupata matatizo. Lingine la mwisho ambalo ninataka kulizungumzia ni suala zima la Wabunge kuwa katika Bodi za *Directors*. Hapa ninataka niongelee suala ambalo mchangiaji wa kwanza ameliliezea.

Mheshimiwa Spika, mimi ninavyojua, Wabunge ni wawakilishi wa wananchi, lakini inapokuwa tena Mbunge anaitetea Serikali, inanipa matatizo kidogo na ndiyo sababu hata kwenye Ripoti ya *CAG*, imeeleza wazi kabisa sababu gani Wabunge hawapo kwenye Bodi za Mashirika ya Umma ili waweze kutekeleza kazi zao za Uwakilishi hapa Bungeni. Kwa hiyo, ninaomba pia hilo litolewe ufafanuzi. Ninashukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Susan Lyimo.

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Said Amour Arfi, kwa hoja yake aliyoileta Bungeni, kama Hoja Binafsi. Ninaunga mkono hoja hii kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, mkataba wenyewe umekwishaanza kuonyesha upungufu katika kipindi kifupi sana cha uendeshaji wa Kampuni ya *RITES* ya India. Baadhi ya vifaa zikiwemo injini na mabehewa yaliyoleta utata, kumekuwepo matatizo ya wafanyakazi na dalili za migomo inayoashiria tatizo katika kuendesha shirika hili. Hatua ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuingilia kati matatizo hayo ni dalili tosha kuwa, kuna haja ya Serikali kuwa karibu sana katika kuendesha kampuni/shirika hili, ambalo pamoja na mikopo waliyopewa, bado kuna wasiwasi kuwa baadhi ya reli kama ya Kaliua - Mpanda haitapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, tungependa Serikali ituhakikishie kuwa, reli hii ya Mpanda haitasahaulika katika mipango yao.



Je, Serikali inatambua kuwa Mkoa wa Rukwa na hasa Wilaya ya Mpanda, haina barabara wala reli ya uhakika kwa kusafirisha mizigo yao?

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja, lakini ninapenda yafuatayo yaangaliwe hivi sasa: Mkataba upitiwe upya ili kuona kama unatekeleza matarajio ya wananchi; Uongozi wa *TRL* kwa haraka iwezekanavyo, uwe wa uwiano kwa pande zote mbili; na Mikataba ya Hiyari kati ya *TRL* na wafanyakazi ili kwa pamoja kila upande ujue majukumu yake, marupurupu yao na namna ya kuyarekebisha matatizo ya mara kwa mara, kwa kuzingatia pia sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, tungependa kujua kwa undani, jinsi mpangilio wa matumizi ya fedha za ndani na za wahisani mbalimbali, ili vipaumbele vijulikane waziwazi.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa mchango wangu kwa njia ya maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninaionba Serikali ilifuatilie Shirika hili la *RITES* kwa karibu sana, kwani huduma inayotolewa sio nzuri kwa maeneo kadhaa.

Idadi ya abiria haiendi sambamba na viti vilivyomo ndani ya mabehewa na kusababisha msongamano; mabehewa yamechakaa sana na ni ya zamani sana, hata madirisha madogo na yapo juu; husababisha joto na ni rahisi kuambukizana maradhi; na injini ni kuu sana kiasi kwamba, treni huchoka na kusimama njiani au kuhitaji injini ya ziada.

Mheshimiwa Spika, vilevile lipo tatizo la mishahara kwani wafanyakazi wa kutoka nje hulipwa zaidi na wafanyakazi wa kwetu hulipwa mishahara midogo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali ifuatilie mambo haya hasa treni ya kati na ya Singida.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la mabehewa ya mizigo na kusababisha mizigo na mifugo kusafiri kwa barabara na kuharibu barabara zetu. Tuweke mabehewa ya mizigo kwenye treni ya Singida.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu, sasa nitamke kuwa, ninaunga mkono hoja hii na ninaomba mchango wangu upate majibu.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, baada ya Shirika la Reli kukabidhiwa kwa *RITES*, njia ya reli za Tanga, Moshi, Arusha na Tanga na Dar es Salaam zimefungwa, pamoja na *stations* zake na mali zote, pamoja na njia kuachwa bila ulinzi kabisa.

Vifaa hivyo ni mali ya Watanzania na njia hiyo ya Tanga - Dar es Salaam - Moshi - Arusha ni muhimu kwa uchumi wa Tanzania, kwa kuwa Tanga kuna bandari nzuri tu na viwanda vingi kikiwepo cha *cement*.

Mheshimiwa Spika, ninashauri Serikali iangize *TRL*, isifunge njia hizo maana itakuwa gharama kubwa kuja kujenga njia nyingine ya reli. Pili, njia za reli zimebaki ni za Serikali, kwa hiyo basi, Serikali imewekeza *TRL shares* asilimia 49, pamoja na njia. Kwa hiyo, Serikali ina hisa zaidi ya asilimia 49, kama ukiweka gharama ya njia. Kwa hiyo basi, lazima ishiriki kwenye maamuzi makubwa ya *TRL*.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, *RITES* mara baada ya kukabidhiwa uendeshaji wa Shirila la Reli Tanzania, walianza kwa kufunga huduma badala ya kuboresha huduma. Wamefunga Reli ya Ruvu - Mnyuzi - Tanga - Moshi - Arusha - Manyoni - Singida na Kaliua - Mpanda

Uamuzi huu ni wa Mkodishaji (*RITES*), bila kushauriana na Viongozi wa Wananchi na Serikali yao (zao), kuhusu usitishaji wa huduma. Aidha, pamoja na kusitisha huduma, pia watumishi wameondolewa kutoka maeneo hayo.

Matokeo yake, Mtandao wa Reli hizo umeachwa uanze kuhujumiwa na watafuta vyuma chakavu. Kusitisha kwa huduma za Reli ya Tanga, kumechangia katika kuidumaza Bandari ya Tanga. Kusitishwa kwa huduma za Reli na kudumaa kwa Bandari ya Tanga, kumesababisha wananchi wengi kukosa ajira kutokana na miundombinu (Reli na Bandari) kuhujumiwa.

Huu ni uhaini na wote waliojijhusisha na maamuzi haya machafu, wachukuliwe hatua za kisheria. Serikali itakiwe kuhakikisha kuwa, huduma za usafiri wa Reli na Bandari ya Tanga zinarejeshwa mara moja.

**SPIKA:** Ninamwita sasa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu, kwa kuzingatia kwamba, mchangiaji wa kwanza alijitahidi kujibu baadhi ya hoja, basi pengine dakika hizo 15 zitakuwa zinakutosha.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii na mimi kukushukuru kwa kunipa nafasi, niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Nianze tu kwa kusema kwamba na mimi kwa niaba ya Serikali, ninaunga mkono hoja hii na maagizo ambayo ukiangalia Azimio lile la mwisho, sina tatizo nalo.

Tatizo dogo ambalo ninaliona kama ambavyo Mheshimiwa Kaboyonga alisema, kampuni hii imeanza karibuni na Bunge la Bajeti ambalo tunatakiwa tuelele ripoti ni miezi miwili/mitatu kuanzia sasa.

Tutaleta, lakini ninachosema, ule muda utakuwa haujatoa fursa nzuri ya kuona ile picha vizuri. Sisi tutajiandaa, kwa maana ya kuleta hiyo ripoti kama ambavyo Azimio la mwisho limesema.

Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema, Mheshimiwa Kaboyonga, amenisaidia sana na mimi ninataka nimshukuru. Ninataka nianze kwa kusema kwamba, kweli umuhimu wa reli kama alivyosema ni muhimu sana.

Sisi kama Chama cha Mapinduzi, katika Ilani yetu tumezungumzia kuboresha miundombinu, ikiwemo suala la reli na tumetaja kabisa pale.

Ni kweli kabisa kwamba, Reli yetu ya Kati, kama ambavyo imeelezwa, ilikuwa katika hali mbaya sana na kwa muda mrefu sana tuliangalia namna gani tunaweza kuiboresha.

Tulifika mahali hali ya reli ilikuwa mbaya sana na ilibidi tufike mahali Serikali iamue kuikodisha reli hii. Vilevile amesema kwamba, mchakato wa kuweza kupata mkodishaji au mbia katika reli hii umechukua miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, ninataka nije kwenye mchakato, kwa sababu suala ambalo limeulizwa hapa la kumpata huyu mkodishwaji, kwa kuwa Serikali ilikuwa haina uwezo wa kibajeti wa kuwekeza na kurudisha reli yetu katika hali nzuri, ilibidi tuangalie vyanzo vya nje.

Tunajua bila kuweka hii *PPP* ambayo tunaizungumza, kwanza, hata ukitaka kupata mikopo kwa sasa hivi kutoka nchi za nje na mashirika mengine ni vigumu sana.

Kwa hiyo, mchakato ule tumendelea nao, lakini ninataka nimweleze mtoa hoja kwamba, huu mchakato haukuwa na mizengwe, kama ambavyo labda amejaribu kusema; ulikuwa ni mchakato wa wazi na ulifuata sheria.

Niseme tu kwamba ni kweli ulichukua muda mrefu kidogo na kuna wengine walijiondoa wakabaki wawili, yule kutoka Afrika Kusini akawa na malalamiko yake kutokana na yeye kushindwa kukidhi baadhi ya vigezo, hata akajaribu kwenda kwenye vyombo vya sheria.

Alipoona kwamba, hawezi kushinda ile kesi, akajiondoa akasema basi ninaachia. Kwa hiyo, akabaki *RITES* na huu ni utaratibu wa kawaida, kwenda mpaka unabaki labda na mkandarasi mmoja, inatokea mara nyingi kama wale wengine ama wanashindwa vigezo au wanajiondoa.

Mchakato haukuwa na matatizo na baada ya kufanya pale *due diligence*, watu wetu walikwenda India na Msumbiji, ambako wamekuwa waki-*operate* na baadaye ilichukua muda kidogo kuangalia. Tunavyo vipengele kwamba, baada ya kumpata huyo mbia, kuna *negotiation* kwamba, unanza kwa kujadili naye baadhi ya vipengele na hii ilifanyika kwa umakini sana. Niwajulishe kwamba, hata ile asilimia 49 haikuwa hivyo,

lakini kutokana na baadhi ya majadiliano, Serikali iliona ni lazima kuwe na *stock* kubwa, ndiyo tukakubaliana naye tukaweza kupata hiyo asilimia 49. Lilikuwa ni jambo muhimu sana kwa Serikali yetu na kwa manufaa yetu kwamba, tuwe na *stock* kubwa.

Mheshimiwa Spika, tarehe moja tukampata *RITES*, imekwishaelezwa ni muda mfupi na tukaanza kuji-*mobilise*, miezi mitano, kwenda mwezi wa sita na mkataba si mbaya. Huu si mkataba ambao unaweza kusema mwangalie vipengele ni utekelezaji wake, ninadhani ndiyo tunataka tuusisitize. Utekelezaji wake unatakiwa kuangalia maeneo ambayo tunaona kwamba, hayatekelezwi vizuri na hapo ndipo mnapotutuma sasa na ndilo tutakalolifanya.

Mheshimiwa Spika, nimeulizwa hapa nieleze kwamba, anatulipa nini kwenye mkataba huu? Katika mkataba huu, huyu anatakiwa atulipe *fixed concession fee* ya dola milioni sita anapoanza na baada ya hapo, anatakiwa atoe *valuable concession fee* inayotokana na biashara. Kwanza, mwaka wa kwanza mpaka mwaka wa tano, asilimia tano ya *gross revenue* na kuanzia mwaka wa sita mpaka wa 25, atoe asilimia saba na nusu ya *gross revenue*. Licha ya kuwa kuna *performance bond*, ambayo anatakiwa atoe dola milioni mbili kila mwaka, mwaka wa 1- 5 na mwaka 6 - 10 atoe dola milioni moja na nusu, mwaka 11-15 atoe milioni moja kila mwaka na mwaka 16 - 25 atoe dola nusu milioni kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, alipofika matatizo aliyoyaona katika miundombinu na kuna mambo mengine ambayo tuliyaona, wakati anafanya *due diligence* kulikuwa na injini 85, alipokuja tulimkabidhi kama injini 57; 28 zilikuwa zimekwisha haribiwa na ndizo tulizokuwa tunazizungumza hapa kwamba, hata sisi wenyewe kama wafanyakazi wa reli na Watanzania, tumechangia katika ku-*vandalise* ile reli, kwa hiyo, akawa na matatizo mengi.

Mheshimiwa Spika, mbia huyu alisema kwamba, kwa namna ninavyoanza nitashindwa mwanzoni kuwalipa, kwanza kwa mwaka huu kulipa hiyo *fixed concession fee* haitawezekana na vilevile *performance bond* muipeleke mpaka mwakani. Tukaangalia na tukakubaliana naye aanze kutulipa mwaka ujao, kwa sababu ya matatizo tuliyoyaona aliyoanza nayo.

Mheshimiwa Spika, ukiacha malipo yake hayo, suala la mtaji kwa miaka mitano ya mwanzo limeangaliwa, tukaona kwamba, sisi na yeye tunahitaji dola milioni 87 kwa ajili ya kazi za kuboresha miundombinu na hizo *rolling stock* na tukasema katika hizi, nusu tutoe sisi wanahisa milioni 43. Wanahisa kwa maana ya Tanzania na yeye; sisi tutoe milioni 16 lakini kutoka kwenye biashara yake hiyo hiyo atoe milioni 27, itakuwa ni milioni 43. Katika hii ya kutolewa na wanahisa, sisi tumetoa zote dola milioni 7.84 na yeye ametoa zile za kwake dola milioni 9.44 kufikisha dola milioni 16, sasa anazoendelea kutoa ni zile ambazo zinatokana na biashara ili zifikie milioni 43 na 44, ndiyo mkopo kutoka *IFC*.

Mheshimiwa Spika, zile zilizotajwa, dola milioni 33, ambazo tulikuwa tukope kutoka Benki ya Dunia, hazimo kwenye hesabu hii kwa sababu hii ni ya Serikali ya

Tanzania kwa ajili ya reli yenyewe lakini zitakuja kuboresha. Ndizo hizo njia ambazo tunasema kwamba, katika asilimia zake za mkopo, ashughulikie zile kilomita 645, sisi tutakapopata mkopo ule kutoka Benki ya Dunia, tutaendelea kuboresha maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, mkopo umechelewa na yeye katika ile biashara amechelewa kutokana na matatizo ambayo nimeyaeleza. Kwenye mkopo ule wa *IFC*, ilitakiwa tufungue akaunti ya dola milioni tano, lakini dola milioni mbili tutoe mara moja halafu milioni tatu tutoe baadaye. Imechukua muda kidogo, lakini Serikali yetu kupitia Hazina, wametoa hizo fedha, tumefungua akaunti na tukamaliza.

Mheshimiwa Spika, vilevile maoni ya *AG*, pamoja na kuteua *process service agent*, ambaye atakaa *London*, hiyo *process* imekwisha na jana tumepata uthibitisho kwamba, tumekamilisha hilo na sasa *IFC* watakuwa hawana matatizo ya kutoa hizo hela. Bado wanaulizia migomo na ndiyo maana ninawaambia wafanyakazi kwamba, tutoe ushirikiano hata hizi hela ionekane kwamba, tunaweza tukazipata.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa *TRL* umekuwa na matatizo na nitaeleza. Ukiona hata sisi kama nilivyoeleza hapo mwanzo kufungua ile akaunti ilichukua muda kidogo lakini pia hizo injini nilizoeleza, hakuzipata kama alivyozikuta wakati wa *due diligence*, imecheleweshwa kidogo, lakini kuna mambo ambayo na yeye amefanya.

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia zile injini tisa za *class 73*, ambazo zimekodishwa; tisa zimekwishaingia na 14 zinakuja na mabehewa 23, ukarabati katika zile *class 88* ambazo ndizo zina nguvu kama ilivyosemwa, alishapeleka saba kule. Tukasema kwa nini hutumii, akasema sisi hatuingii kwenye *PPA*, kwa sababu asilimia kubwa ni ya kwetu, lakini tukasema angalau muwe na *procurement regulations* ili wafanye mambo yao inavyoeleweka. Tumewaambia wapeleke hizo saba zilizotangulia, lakini zile nane tuje tufuate utaratibu wa *International Tenders*. Wameagiza mafuta na vilainishi dola karibu milioni 20, vipuri wameshaandaa *procurement* ya dola milioni kumi na wameanza kukarabati maeneo kutoka Itigi kwenda Kitaraka, kilomita kama 15 na vifaa kadhaa.

Mheshimiwa Spika, bado tunasema, kama ambavyo wadau wengi wanavyosema na sisi tunaona utendaji bado haujaridhisha, ingawa tunakubali muda ni mfupi, lakini huo muda mfupi ilitakiwa tuone basi maandalizi ya kutekeleza mkataba vizuri. Kwa mfano, kutokana na matatizo hayo, tunaona kwamba amepunguza hata ile *performance*. Oktoba, abiria 50,000 walikuwa wanasafiri kila mwezi, lakini kufikia Februari mwaka huu walikuwa wanasafiri abiria 26,327 na hata mizigo ikawa imeshuka kutoka tani 41,000 Oktoba kufikia tani 39,000 Februari.

Mheshimiwa Spika, hizo reli ambazo hata Mheshimiwa Suzan Lyimo amezungumzia; Ruvu, Tanga, Moshi na Arusha, hili tumemkatalia na tunasisitiza ni lazima azirudishe, akawa amesema pia Manyoni, Singida, Kaliua na alikuwa na nia, tumemkatalia kabisa.

Mheshimiwa Spika, uharibifu kwenye magenge, unatokana na hiyo ya kufuta magenge mengine, imeleta matatizo, vifaa vile asivyovihitaji vinaibwa na kadhalika. Tuna matatizo ya muundo pale limesemwa ni Wahindi watupu kwenye *top management*. Sasa hili tumesema arekebishe, vifaa bado vinaonekana vichache, halafu hii ya kukodisha ni kweli matatizo bado anayo lakini ajiandae kununua isiwe ni kukodisha tu na kukarabati na hilo tunamsisitiza katika mazungumzo hayo ambayo tumedhamiria kuyafanya na ambayo mmetuagiza.

Mheshimiwa Spika, hii dhana ya kupunguza wafanyakazi nayo iangalie mkataba; yeye aliposema anataka wafanyakazi fulani alisema angeleta *flying games*, teknolojia ambayo angefanya *severance* kwa haraka zaidi, kwa kutumia mbinu hii. Sasa haijafanywa na anapunguza wafanyakazi, tunambana katika hilo. Katika utekelezaji wa Mradi wa Maendeleo, kuwe na *investment plan* inayoeleweka; mfumo mzuri na *procurement plan* ambayo inaonekana tuone *procurement regulation*, siyo unaamua tu kwamba, unapeleka tu *RITES* India bila kuwa na ushindani fulani, hata kama *PPA* hutumii, lakini Bodi ni lazima msisitize *procurement regulations* angalau za kwao ambazo zinakubalika, hata kama kuna vipengele vinatofautiana na vya kwetu.

Mheshimiwa Spika, mambo yote haya tunayachukua na yale ambayo Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Mheshimiwa Diana Chilolo wameyasema ya injini na matatizo ya abiria wanayopata ni baada ya hizi hela zitakazokuwa zimepatikana na ameboresha tunategemea yatakuwa yamefikia mahali pazuri.

Mheshimiwa Spika, mwekezaji huyu tutambana na tunashukuru kwamba, mmetuongezea nguvu, tulishaanza mazungumzo haya na tutamuweka chini ili tuweze kukamilisha.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa ufafanuzi wako. Sasa ni zamu ya mtoa hoja, Mheshimiwa Said Arfi, ninadhani dakika hizi zisizozidi 20 zitakutosha kwa sababu hakuna aliyeipinga hoja yako.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda nirudie tena kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa mara nyingine ili niweze kuhitimisha hoja ambayo niliiwasilisha mapema leo.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha, ninapenda niwatambue wale ambao wamechangia hoja hii kwa kuzungumza ama kwa maandishi. Ninapenda niwatambue Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Suzan A. J. Lyimo na Mheshimiwa Dr. Milton M. Mahanga - Naibu Waziri wa Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niwashukuru kwa michango yao na sehemu kubwa wameunga mkono hoja, ambayo nilikuwa nimeiwasilisha, lakini ninayo mambo machache ambayo ningependa kuongezea katika haya ambayo wenzangu wamechangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninaomba nizungumzie mchangiaji wa kwanza, ndugu yangu na jirani yangu, kwa sababu siwezi kufika Mpanda bila kupita Tabora kwa Mheshimiwa Kaboyonga. Ninaomba niungane na Mheshimiwa Suzan A. J. Lyimo katika yale ambayo alikuwa ameeleza kwamba ni dhahiri sasa ule wasiwasi aliokuwa nao CAG, kama alivyoainisha katika taarifa yake hii kifungu cha 7.3 ukurasa wa 127, juu ya nafasi ya Wabunge kuwa Wajumbe wa Bodi, ninaomba kunukuu: *“I have noted incidences where political leaders are vested with roles of public entity oversight, this can be reflected in some Members of Parliament being Members of the Board of Directors or Chairpersons of some Boards of Directors of Public Entities, this is considered as departure from the best practices as far as good governance is concerned.”*

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wa CAG umejidhihirisha wazi ni namna gani Mheshimiwa Kaboyonga, alivyosahau majukumu yake kama mwakilishi wa wananchi na akachukua nafasi hiyo kuwa msemaji wa RITES. Anayo haki kama Mbunge, kwa sababu alikuwa anayajua hayo, lakini kwa bahati mbaya sana, Mheshimiwa Kaboyonga hili jambo amelipandia katikati tu, amekuwa na mashaka na hoja yangu kwamba, nimezungumzia kuanzishwa kwa TRL mwaka 2007 lakini sikutaja mwezi, akasahihisha akasema kwamba, imeanza mwezi wa Oktoba. Ninakubaliana naye kabisa na ninakubali kuwa uhai wa TRL ni miezi mitano au sita kama alivyosema.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kumpata RITES ni wa muda mrefu, tangu mwaka 2004 alipokuwa amekubaliwa kukodisha miundombinu ya reli. Sheria au ratiba iliyokuwa imetolewa na PSRC juu ya mchakato wa kumpata mwendeshaji wa kampuni ya reli ulikuwa umeweka *timeframe*, toka siku wana-*award* hadi siku ya kutengeneza hiyo kampuni ya ku-*mobilise* vifaa na kuanza, iliwekewa kikomo cha muda. Muda ulipokwisha, mwekezaji huyu alishindwa kuanza kwa sababu alikuwa na matatizo ya kifedha na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa za kutafuta mwekezaji mwingine. Hapo ndipo tumekuwa na mashaka na kusema tuangalie mchakato mzima; kwa nini ulisuasua na kwa nini yalitokea hayo yaliyotokea na hatimaye akapewa kampuni hiyo kuiendesha kwa ubia na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, bado yapo mashaka juu ya uwezo wa Kampuni hii ya RITES pamoja na maelezo mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu, lakini Kampuni hii ya RITES ilipewa fedha za kuweza kuja kuweka mchango wake katika kuanzisha kampuni hii kutoka kwenye Serikali ya India, kama ilivyokuwa imeidhinishwa na Baraza la Mawaziri wa India. Wameidhinisha hilo kwa sababu *Internal Rate of Return (IRR)* itakuwa ni asilimia 43, wameshaona ni kiasi gani cha faida watakazotengeneza kwa kutumia miundombinu yetu, ndiyo maana Serikali ya India ikakubali kui-*support* Kampuni ya RITES na kutoa kiasi cha milioni nane ili waje watoe *equity* yao kwa kuanzisha kampuni hii.

Mheshimiwa Spika, lakini pia zipo habari ambazo zilikuwa zinaelezwa kabla hata ya kuletwa kwa kampuni hii; aliyekuwa Waziri wa Mipango na Uwezeshaji Mheshimiwa Juma Ngasongwa alinukuliwa wakati fulani akisema kwamba, kabla tu ya kuanza kazi itaingiza mtaji wa dola milioni 43. Hii ilikuwa inaleta matumaini na matarajio makubwa sana kwa Watanzania kwamba, kampuni hii itanza kwa nguvu kubwa sana na dosari zote zilizokuwepo wakati wa kuiendesha *TRC* zitaondoka.

Mheshimiwa Spika, matarajio ya Watanzania na hususani wakazi wa Jimbo langu la Mpanda na Wilaya ya Mpanda ambao hawana njia nyingine yeyote ya usafiri wa uhakika kuliko reli yalikuwa ni makubwa sana kwa kampuni ya *RITES*, matokeo yake ndiyo kumekuwa na matatizo ya hapa na pale na ufanisi hauna matumaini kabisa katika siku chache zijazo, ndiyo maana makusudio kwa nia safi kabisa kuitaka Serikali iweze kuwasukuma hawa kuona matarajio ya Watanzania yanafikiwa, lakini bado pia iko haja ya makusudi kabisa kuupitia mkataba kama nilivyoomba katika azimio la Bunge, kwamba je Mkataba huu unatoa fursa ya kukatisha Mkataba wakati wowote itakapokuwa imebidi kukatisha Mkataba?

Mheshimiwa Spika, hakuna mtu anayefahamu, ndiyo maana tukasema kwamba, ipo sababu ya msingi kabisa ya kupitia mkataba kama unatoa fursa hiyo ya kuwepo kipengele hicho kama wawekezaji hao wameshindwa waweze kuachia ngazi. Suala hili si jipya kwa sababu pia liliwahi kuulizwa na Mheshimiwa Adam Malima, Mbunge wa Mkuranga, wakati akichangia Hotuba ya Bajeti ya Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2007/2008, kuhusu Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Malima, aliomba kupewa maelezo hayo lakini mpaka sasa hivi, Serikali haijatoa maelezo kwamba, kipo kipengele cha kuweza kuukatisha Mkataba huu kama tunaona hauna maslahi kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hoja nyingi ambazo zimetolewa na upungufu mwingine wa wazi ambao umeongezwa hapa, hata heria zetu zimepuuzwa kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, Sheria ya *PPRA* haikutazamwa na kusimamiwa na hii yote ni kinyume na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika kwamba, sote kwa pamoja tunakubaliana na umuhimu wa reli, faida zake na namna gani itakavyoweza kusaidia uchumi wa nchi yetu. Ni vyema basi katika hayo, Serikali ambayo itayasimamia na kuyafanya, wakahakikisha kwamba, wawekezaji hawa wameongeza mabehewa ambayo yatakuwa maalumu kwa ajili ya kubeba makontena. Mabehewa mengi ambayo tunayo yaliyokuwa mali ya *TRC*, yaliyokuwa yamefungwa ama mabehewa ya kubeba mifugo ambayo hayawezi kubeba makontena.

Mheshimiwa Spika, kuna msongamano mkubwa sana wa makontena katika Bandari ya Dar es Salaam na limekuwa ni tatizo kubwa sana, ambalo linatusumbua. Kwa hiyo ni lazima waone wataweka nguvu kiasi gani ili kuweza kupunguza msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam ili kuweza kuongeza tija na ufanisi wa Bandari na uchumi wa taifa kwa ujumla wake.



Mheshimiwa Spika, aidha, nikubaliane na kauli ya Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na kuwa na mashaka kuhusu njia hizi ambazo ni *branch line*, ambazo kampuni hii inafikiri kwamba, si muhimu sana, wanachotazama ni faida watakatengeneza kusafirisha mizigo kwa kupitia Reli ya Kati na hawaoni umuhimu kabisa wa reli ya kutoka Ruvu kwenda Tanga - Moshi - Arusha na Manyoni - Singida - Kaliua - Mpanda.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika kwamba, Serikali imeshatoa kauli kwamba, watahakikisha reli hizi hazifungwi, lakini kwa taarifa zilizopo reli ya kutoka Ruvu kwenda Tanga, Moshi hadi Arusha sasa hivi haifanyi kazi. Wafanyakazi wote katika vituo vya reli wameshaondolewa, nyasi zimeota katika njia nzima ya Reli ya Tanga, mali yetu Watanzania imetelekezwa, hakuna anayeisimamia inaharibiwa, inaibiwa na hii ni fedha ya wananchi maskini wa nchi hii, ambao waliwekeza katika miundombinu ya reli.

Mheshimiwa Spika, tunaitaka tena Serikali katika eneo hili, waangalie kwa haraka iwezekanavyo, katika mchango wa Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi amesema, tendo hili ni uhaini na wanastahili kuchukuliwa hatua za kisheria. Ninakubaliana naye kabisa, huu ni uhaini na ni hujuma kwa nchi yetu na uchumi wa Taifa letu, lazima tuangalie ni namna gani sasa tunaweza tukaisimamia vizuri reli hii ya Tanga.

Mheshimiwa Spika, wapiga kura wa Jimbo la Mpanda Kati hawawezi kunielewa kama sintoizungumzia reli ya Mpanda, pamoja na matatizo mengi yanayoigusa reli ya Mpanda lakini hali inazidi kuwa mbaya sana baada ya kampuni hii kusimamia huduma katika njia ya kutoka Tabora, Kaliua – Mpanda.

Mheshimiwa Spika, idadi ya mabehewa imepungua kwa kiasi kikubwa sana na hakuna maelezo yoyote yanayotolewa, wasafiri kama alivyosema Mheshimiwa Genzabuke, wanasafiri katika hali ngumu sana, mahali walipokuwa wakichukuliwa kwa mabehewa matano sasa wanasafirishwa katika mabehewa mawili.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tufikiri kwamba, watu hawa wanasafiri katika hali gani; hawa ni wale Watanzania maskini, wanyonge na wasiokuwa na uwezo wa kumudu usafiri mwingine wowote. Kutoka Mpanda mpaka Dar es Salaam kwa njia ya barabara ni shilingi 53,000 na unalazimika kulala Sumbawanga na Mbeya; gharama yote ya safari inakaribia shilingi 70,000 mpaka laki moja. Kusafiri kwa kupitia njia ya reli ni chini ya shilingi 20,000 ni usafiri ambao maskini wanauweza, watu ambao hatuwafikirii kuweza kuimarisha na kuwahakikishia kwamba wanapata usafiri wa uhakika wakati wote.

Mheshimiwa Spika, tupo tayari kuwekeza katika usafiri wa anga, ambao unatumiwa na watu wachache na usafiri ambao unatumiwa na wapiga kura wetu wengi tunaupuuza. Ipo haja ya makusudi sasa, Serikali kama inaweza kuwekeza na kununua ndege inaweza pia ikawekeza na kununua injini za treni.

Mheshimiwa Spika, lazima tuangalie usafiri huu wa reli na tuupe uzito unaostahili. Matumaini yangu ni kuwa ahadi iliyotolewa na Serikali, kupitia Bunge hili

kwamba watatekeleza, wataisimamia, wataisukuma Kampuni ya *RITES* itimize wajibu wake itatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, wafanyakazi ambao sasa hivi wapo katika Kampuni ya *TRL* nao watoe mchango wao kama inavyostahili na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokwenda kuongea nao mara ya mwisho ili kuzima mgomo ambao umewasumbua sana Watanzania wengi.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa kwa maneno yale aliyoyasema Mheshimiwa Waziri Mkuu, basi wafanyakazi wa reli watatimiza wajibu wao na pia mikataba kati ya wafanyakazi na Kampuni ya Reli ni lazima iheshimiwe na kila upande ujue jukumu lake, wajibu wake na haki ili waweze kutekeleza ipasavyo kwa maslahi na faida ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, Watanzania wametusia, wanatutazama na wanangoja kusikia maamuzi ya Bunge hili, kama lilivyopewa mamlaka na wananchi hao ili waweze kuisimamia Serikali, wataamua nini kuhusu hoja niliyowasilisha leo mapema.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Said Arfi, kwa ufasaha wa kuiwasilisha hoja. Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyopo mbele yetu, hitimisho lake lipo katika ukurasa wa pili wa Azimio lililoandaliwa. Kwa maana hiyo, Bunge linaombwa sasa kuitaka Serikali kuangalia Mkataba wa Ukodishaji wa Shirika la Reli; sura ya menejimenti; na iangalie uboreshaji wa huduma katika eneo hilo, hoja imetolewa na imeungwa mkono sasa nitawahoji.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja Binafsi ya Uendeshaji Usioridhisha wa Shirika la Reli Tanzania ilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Tunaendelea, leo ni siku ya Hoja Binafsi tu. Katika hatua hii, ninaomba nitoe tangazo kwamba, nimekaa na wataalam wangu, tumepiga hesabu ili tuzimalize itabidi tuchukue na saa moja ya kesho asubuhi.

Nisingependa Hoja Binafsi hizi zikatugawa, kwa sababu ikiahirishwa itabidi iwe hadi mwezi wa nane, kwa sababu Mkutano wa Kumi na Mbili ni wa Bajeti na huwezi kuwa na shughuli binafsi mpaka hatua za mwisho mwisho mwezi wa nane, huko ni mbali sana tujitahidi tuzimalize kesho asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, bahati njema, kesho kama mnavyofahamu, ratiba yetu ina Miswada ya Kusomwa Mara ya Kwanza. Kwa hiyo, hakuna mjadala kuna Maazimio mawili tu mepesi. Kwa hiyo, ninadhani tunaweza kumaliza kama tulivyopanga. Sasa nitamwita mtoa hoja wa hoja inayofuata ambayo inahusu utendaji usioridhisha wa

Kampuni ya *Tanzania International Container Terminal Services*, Mheshimiwa Godfrey Zambi.

## **USIORIDHISHA WA KAMPUNI YA TANZANIA INTERNATIONAL CONTAINER TERMINAL SERVICES (TICTS)**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha hoja inayohusu utendaji wa kazi usioridhisha wa kitengo cha makasha pale Bandari ya Dar es Salaam (*Tanzania International Container Services (TICTS)*).

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 54(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2007, ninaomba kuwasilisha maelezo yangu binafsi kuhusu utendaji kazi usioridhisha wa kitengo hicho ambacho kinajihusisha na upakuaji wa makasha pale bandarini.

Kufuatia utendaji huo usioridhisha, ni naomba Bunge lako Tukufu liagize Serikali, isitishe nyongeza ya pili ya mkataba wa miaka 15, ambao Kampuni ya *TICTS* iliongezewa, kwa sababu mkataba huo uliongezwa bila kuzingatia Sheria Namba 21 ya mwaka 2004, inayosimamia manunuzi Serikalini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia nichukue nafasi hii, kukushukuru wewe mwenyewe, Naibu Spika, pamoja na Kamati yote ya Uongozi ya Bunge, kwa kukubali hoja yangu isikilizwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Kuhudumia Makasha katika Bandari ya Dar es Salaam, kilikodishwa kwa mwekezaji binafsi mwaka 2000. Mkataba wa uendeshaji wa Kitengo hicho, ulitiwa saina tarehe 05 Mei, 2005 kati ya Serikali na Kampuni ya *International Container Terminal Limited* ya nchini Manila. Mkataba huo ulikuwa wa miaka kumi na ulikuwa umalizike mwaka 2010. Kampuni ya *ICTL*, haikudumu sana na hivyo, iliamua kuuza hisa zake zote kwa Kampuni ya *TICTS*.

Kampuni ya *TICTS* inamilikiwa kwa pamoja kati ya Kampuni ya *Hutchison Port Holdings (HPH)* ya *Hong Kong* na Kampuni ya Kitanzania inayoitwa *Harbours Investment Limited*. Kampuni ya *HPH* ya *Hong Kong*, inamiliki hisa asilimia 70, wakati ile ya Kitanzania inamiliki hisa asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 30 Desemba, 2005, Serikali iliamua kuiiongezea *TICTS*, mkataba wa miaka mingine 15 na kufanya mkataba huo kuwa wa miaka 25.

Mheshimiwa Spika, madhumuni makubwa ya ukodishaji wa Kitengo cha Kontena ilikuwa ni kuongeza ufanisi zaidi wa kitengo, kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi. Ilitegemewa kwamba, bandari ingeweza kuendeshwa kwa tija kubwa zaidi, hasa kwa mkodishaji kuleta vifaa vyenye teknolojia ya juu zaidi, ikilinganishwa na vilivyokuwepo

kabla ya ukodishaji. Kwa ujumla, ilitegemewa kwamba, mkodishaji angeweza kukabiliana na ushindani wa bandari za nchi jirani kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya awali, *TICTS* ilionekana kufanya vizuri, hata hivyo, kuanzia mwaka 2005, utendaji wake wa kazi ulianza kushuka. Hiki kilikuwa ni kiashiria tosha kabisa, ambacho kingeifanya Serikali isiiongezee *TICTS* mkataba mwingine wa miaka 15. Kwa ujumla, kushuka kwa ufanisi hakukuendana na matarajio au makusudi ya kukodisha Kitengo cha Kontena. Suala la utendaji mbaya wa *TICTS*, nitaliezea kwa kirefu katika kipengele kinachofuata hapa chini.

Mheshimiwa Spika, mambo ambayo mkodishaji alipaswa kufanya kwa mujibu wa mkataba; kama nilivyoieleza hapo juu, madhumuni makubwa ya ukodishaji wa Kitengo hicho yalikuwa ni kuongeza ufanisi. Hivyo, chini ya mkataba huo, vigezo ambavyo mwekezaji alitakiwa kuvitimize ili kufikia azma hiyo ni kama ifuatavyo:-

Moja, kuongeza kiwango cha shehena inayohudumiwa na kitengo. Pili, kuongeza ufanisi katika kuhudumia makasha. Tatu, kufanya matengenezo ya vifaa ambavyo alikodishwa na mamlaka. Nne, kununua vifaa vingine endapo ipo haja ya kufanya hivyo. Tano, kulipa kodi ya pango na mrabaha (*royalty*), kama ilivyoainishwa kwenye mkataba.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia utekelezaji wa mkataba huo na hususan vigezo vilivyotajwa hapo juu, yafuatayo yamejitokeza:-

Kigezo cha kwanza, katika kupitia nyaraka mbalimbali kutoka Kampuni ya *TICTS* na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*), inaonekana kwamba, shehena ya makontena imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 14.9 kila mwaka. Katika kipindi cha mwaka 2007, jumla ya *TEUs* 343,130 zilihudumiwa na kitengo. Inakisiwa kuwa, idadi ya *TEUs* milioni moja zitahudumiwa na kitengo ifikapo mwaka 2016. Ongezeko hilo ni kubwa sana na ni dhahiri kwamba, eneo lililopo sasa halitaweza kubeba ongezeko la *TEUs* 650,000 ifikapo mwaka 2010, kulingana na mkataba. Aidha, mkataba uliopo, hauna kipengele chochote kinachomtaka mwendeshaji, kukodisha eneo lingine au kununua eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, mkataba unaonyesha kwamba, mwekezaji mwingine ataruhusiwa kuomba kufanya biashara ya aina hiyo, pale tu Kampuni ya *TICTS* itakapokuwa imefikisha kuhudumia makontena 650,000. Kipengele hiki ni cha kushangaza, hasa katika ulimwengu wa leo wa biashara ya ushindani. Kuna jedwali pale chini, ambalo limeonyesha *trend* yake ilivyokuwa inafanywa pale ilipoanza mpaka mwaka 2007.

Kigezo cha pili, mwekezaji alitakiwa kuongeza ufanisi katika kuhudumia makontena. Moja ya kigezo kinachotumika katika kupima ufanisi wa kupakuwa na kupakia makontena kwenye meli ni mzunguko wa *crane* kwa saa. Ukiiondoa mwaka 2003 na 2004, *TICTS* haijawahi kufikisha lengo kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba, kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali la pili, ambalo lipo pale chini. Mwaka 2007, ufanisi ulishuka kwa asilimia karibu 26.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zinaonyesha kuwa, ongezeko la shehena halikwenda sambamba na ufanisi, yaani uhudumiaji wa makontena.

Aidha, takwimu hizi zinaonyesha kwamba, mwendeshaji hakuwa na vifaa vya kutosha vya kumwezesha kuhudumia meli na mizigo kwa ufanisi; suala hili nitalizungumzia baadaye kidogo.

Katika kuthitibisha zaidi kwamba, kigezo cha ufanisi kimeshuka, mambo yafuatayo yamejitokeza:-

Moja, muda wa meli kusubiri kuingia bandarini umeongezeka kutoka wastani wa siku 0.2 mwaka 2001 hadi kufikia siku 4.8 mwaka 2007. Kiwango kinachokubalika Kimataifa ni siku 0.2.

Mbili, wastani wa muda wa mzunguko wa meli (*Ship Turn Round*), umeongezeka kutoka siku 1.0 mwaka 2001 hadi siku 6.2 mwaka 2007. Kiwango kinachokubalika Kimataifa ni siku 2.0.

Tatu, wastani wa makontena yanayokuwepo ndani ya kitengo kwa wakati mmoja (*Holding Capacity*), umekuwa zaidi ya *TEUs* 9000, ukilinganisha na uwezo wa Kitengo wa *TEUs* 6,500.

Nne, muda wa makontena ya *imports* kukaa bandarini umeongezeka kutoka siku 16.7 mwaka 2004 hadi kufikia siku 18.3 mwezi Agosti, 2007.

Tano, msongamano wa meli zinazosubiri kuingia bandarini umeongezeka sana. Kwa mwezi Agosti, 2007 ilifikia asilimia 84.9, kiwango hicho ni cha juu sana. Kiwango kinachokubalika Kimataifa ni kati ya asilimia 50 hadi 60 kwa gati za makontena. Kiwango hicho, kadri ya wataalam ni kwamba hakiruhusu hata matengenezo ya gati kuweza kufanyika.

Sita, wastani wa makontena yanayoshushwa (*imports*), kukaa bandarini ulishuka hadi kufikia siku 10.6 mwezi Julai, 2001. Baada ya hapo, wastani umekuwa ukiongezeka hadi kufikia siku 23 mwezi Desemba, 2007. Kigezo kilichotumika kubainisha uwezo wa Kitengo (*Terminal Capacity*) ni wastani wa siku 12. Kwa ujumla, *TICTS* imeshindwa kabisa kufikia kiwango cha wastani wa siku 12, kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 3, ambalo lipo hapo chini. Hata hivyo, ikichukuliwa kesi moja moja, kontena hukaa bandarini kwa zaidi ya siku 60.

Kigezo cha tatu, mkodishaji anapaswa pia kufanyia matengenezo vifaa alivyokodishwa na *TPA*. Kutokana na taarifa nilizonazo ni kweli kuwa, *TICTS* hufanya matengenezo ya vifaa hivyo. Hata hivyo, vifaa vingi ni vichakavu sana, kwani vingi vilinunuliwa na *TPA* kati ya mwaka 1987 na 2000, kama inavyoonyeshwa kwenye taarifa ya utendaji kazi ya *TPA*, ambayo Waheshimiwa Wabunge nimeambatanisha. Kiwango cha kuharibika vifaa hivyo ni kikubwa na hivyo kuathiri sana utendaji kazi wa *TICTS*.

Kigezo cha nne, mkodishaji anatakiwa kununua vifaa vingine endapo ipo haja ya kufanya hivyo. Kwanza ni vizuri Bunge lako Tukufu, likafahamu kwamba, mkodishaji hakuja na vifaa vyovyote alipoanza kazi; alikodishwa ardhi, pamoja na vifaa vilivyokuwepo. Hivyo, inashangaza pale ambapo mkataba unasema mkodishaji atanunua vifaa vingine, endapo ipo haja ya kufanya hivyo. Inashangaza kwamba, umuhimu na ulazima wa mkodishaji kununua vifaa vya kisasa zaidi haukuonekana, kiasi cha kumruhusu afanye hivyo kwa hiari yake, kama ataona ipo haja ya kufanya hivyo. Maana ni kwa kufanya hivyo, ndipo kazi ingefanyika vizuri zaidi na kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nachelea kusema kwamba, *TICTS* waliutumia mwanya huo na hivyo kutonunua vifaa vingi na vya kisasa, ambavyo vingewawezesha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Kwa mfano, wakati *TICTS* wanaanza kufanya kazi, makontena yalikuwa yanapangwa hadi tatu kwenda juu, maana uwezo wa vifaa vilivyokuwepo ulikuwa unawezesha makontena kupangwa si zaidi ya matatu kwenda juu. Hata hivyo, katika kukabiliana na tatizo la nafasi, *TICTS* ilianza kupanga makontena hadi sita kwenda juu. Kutokana na ukweli kwamba, vifaa vilivyokuwepo vilikuwa na uwezo mdogo, huchukua muda mrefu katika kupanga makontena na hivyo kusababisha ucheleweshaji mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa yake kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, hapo tarehe 23 Januari, 2008, taarifa hiyo nimewaambatanishia Viongozi wa *TICTS*, waliieleza Kamati kwamba, wanatambua umuhimu wa kuwepo kwa vifaa katika uendeshaji wa Kitengo cha Kontena. Aidha, waliieleza Kamati kwamba, hadi kipindi walichokuwa wanatoa taarifa kwa Kamati, walikuwa wamewekeza zaidi ya dola za Kimarekani milioni sita kwenye wa vifaa. Taarifa hii pia imeambatanishwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na taarifa hiyo ya *TICTS*, bado kiwango cha uwekezaji katika ununuzi wa vifaa ni kidogo sana. Kulingana na Mkataba *TICTS*, ilitakiwa iwe imewekeza jumla ya dola za Kimarekani milioni 10.389 hadi mwaka 2007. Hii ni tofauti ya takribani dola za Kimarekani milioni nne. Hali hiyo, haionyeshi kama kweli *TICTS* inayo dhamira ya kweli katika uwekezaji, wala suala la vifaa.

Kwa maoni yangu, ninadhani Uongozi wa *TICTS*, ulitaka kuionyesha Kamati kwamba, inayo dhamira na bila shaka ulidhani kwamba, Wajumbe wa Kamati, hawajui chochote kilichopo kwenye Mkataba.

Mheshimiwa Spika, tarehe 23 Januari, 2008, *TICTS* iliieleza Kamati kwamba, imewekeza dola milioni sita za Kimarekani kwenye ununuzi wa vifaa. Tarehe 15 Aprili, 2008, tulikutana nao hapa Dodoma walitueleza kwamba, wamewekeza dola milioni 15 za Kimarekani kwenye ununuzi wa vifaa. Dhahiri, mtu anaweza kuona kwamba, huu ni uongo, kwa sababu kusingikuwa na tofauti ya shilingi milioni tisa katika kipindi cha miezi mitatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika taarifa yake kwa Kamati, Uongozi wa *TICTS* ulieleza kwamba, mmoja wa wamiliki wa Kampuni ya *TICTS* ni Kampuni ya *Hutchison Port Holdings (HPH)* ya *Hong Kong*. Kamati ilielezwa kwamba, *HPH* ni kampuni inayoongoza katika kuwekeza katika bandari, ikiwa ni pamoja na kujenga na kuendesha

jumla ya gati 292 katika bandari 46 za nchi 23 huko Asia, Mashariki ya Kati, Afrika, Ulaya na Bara la Amerika. Pia Kamati ilielezwa kwamba, makasha zaidi ya milioni 59 TEUs, huhudumiwa kwa mwaka. Bila shaka hii ni kampuni kubwa sana na yenye mtaji mkubwa sana na yenye uzoefu wa kufanya biashara ya aina hiyo duniani. Inashangaza na wala haiingii akilini kabisa, kuona jinsi kampuni kubwa namna hiyo, yenye uwezo mkubwa hivyo duniani na inavyomiliki asilimia 70 ya hisa za TICTS, imeshindwa kuwekeza katika ununuzi wa vifaa, kama makubaliano yalivyokuwa kwenye mkataba. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kigezo cha tatu, moja ya masuala muhimu ambayo mkodishaji anatakiwa kufanya ni pamoja na kulipa kodi ya pango na mrabaha kama ilivyoainishwa kwenye Mkataba. Kitengo hiki, kimekuwa kikipata faida kubwa sana tangu kianzishwe. Hata hivyo, kiasi cha fedha kinachowekezwa ni kidogo sana. Kwa mfano, faida iliyopatikana mwaka 2006 ni takribani shilingi bilioni 33,664, sawa na dola za Kimarekani milioni 28, zilitolewa kama gawio kwa wanahisa wa kampuni katika kipindi cha miaka miwili ya 2005 na 2006. Kiwango cha uwekezaji katika kipindi cha miaka 2007 na 2008, kilikuwa ni takribani dola Kimarekani milioni 24.4. Inashangaza kwa sababu wanapiga hesabu na mwaka ambao pengine hatujafika hata nusu yake! Mapato halisi na matumizi ya TICTS, kuanzia mwaka 2001 ni kama inavyoonyeshwa hapo kwenye jedwali, ambayo mmeambatanishwa. Matumizi yanaonekana katika jedwali namba tano na pale ndiyo mnapoweza kuona hata kiwango ambacho Serikali inaambulia kutoka mapato yote ambayo TICTS inayapata, takriban dola milioni 43.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba, kitengo cha TICTS, kimekuwa kikipata faida kubwa sana, ikilinganishwa na uwekezaji kwenye maeneo mbalimbali, hususan ununuzi wa vifaa. Aidha, ukiangalia kwenye jedwali namba tano, utaona kwamba, kiwango cha mrabaha kinacholipwa Serikalini ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, ninakwenda haraka haraka, kwa sababu mengine ninatumaini Waheshimiwa Wabunge, watakuwa wameshayasoma.

Kipengele cha nne, utaratibu uliotumika katika kuiongeza TICTS Mkataba wa miaka mingine 15, kwa maoni yangu ulikuwa na kasoro kubwa kama zifuatazo:-

- Sheria Na. 21 ya mwaka 2004 ya Manunuzi ya Umma ilikiukwa. Kwa mjibu wa Sheria hiyo Mkataba wa aina hiyo, ukishawekwa sahihi na pande zinazohusika, hautabadilishwa kwa namna yoyote ile, ila tu kama kufanya hivyo ni kwa manufaa ya Serikali na si vinginevyo. Kama ambavyo nimeshaeleza huko nyuma, Mkataba huu haukubadilishwa kwa manufaa ya Serikali, kwa sababu kama tulivyoona, Mkataba ulibadilishwa kwa kutiwa saina wakati utendaji wa TICTS umeanza kushuka chini.

- Nyongeza ya Mkataba wa miaka 15, ilikiuka pia makubaliano ambayo yapo kwenye Mkataba wenyewe. Kifungu cha 9.1 kinasomeka hivi, kwa ruhusa yako ninaomba kukinukuu: *“This lease including the schedules and appendixes, shall not be amended except by an instrument in writing agreed to and signed on behalf of each parties or their assignees, hereto after due consultation with all the parties who may be affected by such an amendment. Amendments of the term shall not be permitted.”*

Mheshimiwa Spika, wale wote waliohusika na kubadilisha mkataba huu, walijipa madaraka makubwa kupita kiasi. Kwa vyovyote vile, walifanya kwa makusudi na kwa maslahi yao, jambo ambalo ni ukiukwaji wa zana nzima ya Utawala Bora, lakini pia ni kinyume na kaulimbiu ya wakati huo “uwazi na ukweli.”

Mheshimiwa Spika, katika Taarifa yake ya Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma, kwa mwaka ulioishia 30 Juni, 2007, Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, pia amebaini upungufu mkubwa sana kwa upande wa *TICTS*. Ametaja pia kukiukwa kwa Sheria ya Manunuzi Serikalini; na kukiukwa kwa Mkataba wenyewe wa *TICTS* na Serikali. Kwa ujumla, CAG amesema nyongeza hiyo ya Mkataba ni batili.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, nyongeza ya pili ya Mkataba wa miaka 15, ilifanywa kupitia barua Na. TYC/R/160/32 ya tarehe 6 Septemba, 2005, iliyoandikwa na kutiwa saini na Mheshimiwa Basil P. Mramba, wakati huo akiwa Waziri wa Fedha. Barua hiyo, pamoja na mambo mengine, ilimtaka Kamishna wa Mapato Tanzania (*TRA*), ahakikishe kuwa, muda wa Mkataba unaongezwa kuwa wa miaka 25; nakala ya barua hiyo imeambatanishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kufuatia nyongeza hiyo ya Mkataba kwa Kampuni ya *TICTS*, mambo yafuatayo yamejitokeza:-

Moja, hakukuwa na sababu yoyote kwa Serikali kuiongezea *TICTS* nyongeza ya mkataba, kwa sababu utendaji wake ulikuwa umeanza kushuka mwaka 2005. Aidha, walishindwa kununua vifaa kulingana na mkataba.

Mbili, kitendo cha kuiongezea *TICTS* muda, kinyume na makubaliano ya awali ilikuwa ni kukiuka wazi wazi Sheria ya Manunuzi Serikalini, kama nilivyotaja hapo juu.

Tatu, hakukuwa na dharura yoyote ya kulifanya suala hilo zito na nyeti kwa uchumi wa nchi katika mazingira ambayo Bunge na Baraza la Mawaziri, vilikuwa vimevunjwa na waliokuwa Mawaziri walikuwa wamekasimu kazi zao kwa Makatibu Wakuu wa Wizara walizokuwa wanaziongoza, ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Basil P. Mramba, aliyeandika barua akiagiza kuongezwa kwa Mkataba huo.

Nne, kulikuwa bado kuna malalamiko mengi kutoka kwa wafanyabiashara na wadau mbalimbali, wakilalamikia utendaji mbaya wa *TICTS*.

Tano, kuna upungufu mkubwa uliopo kwenye Mkataba kati ya Serikali na *TICTS*, kwa mfano, kuwepo kwa kipengele cha *exclusivity*, malipo ya mrabaha ambayo hayaendani na ukuaji wa biashara na mkodishaji kutokuwa na mpango wa uwekezaji hasa ununuzi wa vifaa vipya.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, mambo yote hapo juu yanaonyesha upungufu mkubwa uliopo Serikalini na hususan katika suala hili. Hivyo ni wajibu wa Bunge lako



Tukufu, kuisimamia Serikali kikamilifu ili isiendeleo kuvunja kwa makusudi, sheria, kanuni na taratibu mbalimbali ambazo zipo kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba nisome Maazimio.

**KWA KUWA** Kampuni ya *TICTS* imeshindwa kabisa kutekeleza matakwa na masharti ya Mkataba wa kuhudumia makasha katika Bandari ya Dar es Salaam, hususan kuwekeza kwenye ununuzi wa vifaa na mitambo mipya inayohitajika kwa ajili ya kuhudumia makasha hayo bandarini;

**NA KWA KUWA** kumekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wadau mbalimbali, wakiwemo wafanyabiashara na Wabunge kuhusu utendaji usioridhisha wa Kampuni ya *TICTS*;

**NA KWA KUWA** kutokana na utendaji mbovu na usio na tija wa Kampuni ya *TICTS*, masharika mengi ya meli yamelazimika kupunguza safari zinazopitia Bandari ya Dar es Salaam kwa kuhofia meli zao kukaa kwa muda mrefu bandarini hapo;

**NA KWA KUWA** kitendo hicho kinaifanya Serikali yetu ipate hasara kwa kukosa mapato;

**NA KWA KUWA** kutokana na utendaji kazi mbovu Serikali haikuwa na uhalali wowote wa kuiongezea Kampuni ya *TICTS* muda wa mkataba wa kipindi cha miaka 15 zaidi hata kabla ya muda wa mkataba wa kwanza kumalizika;

**NA KWA KUWA** katika mazingira hayo misingi ya uwazi na Utawala Bora haikuzingatiwa katika kufikia uamuzi wa kuongeza muda wa mkataba na kwa vyovyote vile Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004 ambayo kwenye kifungu cha 69(1)(a) inatamka kwamba, mkataba wa aina hiyo ukishawekwa saina na pande zinazohusika, hautafanyiwa marekebisho kwa namna yoyote ile isipokuwa kwa manufaa ya Serikali na si vinginevyo;

**NA KWA KUWA** nyongeza ya Mkataba ina kasoro nyingi za kisheria kama vile kuweka vifungu ambavyo havina tija kwa uchumi wa taifa, kwa kuzuia wawekezaji wengine na kuweka viwango vya malipo ya mrabaha ambavyo haviendani na ukuaji wa biashara;

**NA KWA KUWA** katika taarifa yake ya ukaguzi wa hesabu za mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2007, Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Fedha za Serikali amebainisha kwamba nyongeza hiyo ya mkataba haifai na kwamba kampuni ya *TICTS* imeshindwa wajibu wake;

**KWA HIYO BASI**, ili kuondoa kasoro zote zilizopo kwenye mkataba wa kuhudumia makasha katika Bandari ya Dar es Salaam, kuleta ufanisi na kuiwezesha Serikali kuongeza mapato yake, Bunge linaazimia kwamba Serikali isitishie nyongeza ya

mkataba na kufanya mapitio ya mkataba wa awali ili vifungu vya mkataba huo ambavyo havina manufaa kwa taifa virekebishwe; na kwamba baada ya muda wa mkataba wa awali wa miaka kumi kumalizika, nyongeza yoyote ya mkataba au mkataba mwingine mpya uzingatie Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya mwaka 2004. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote, ninasema ninaiunga mkono hoja na ingewezekana ningeongeza Azimio lingine lakini nitaishia kwanza hapo.

Mheshimiwa Spika, nianze tu kwa kusema kwamba, nimepitia nyaraka zote, nimezizoma kwa umakini sana, ninaungana kwamba mkataba usitishwe, kwanza, kwa sababu Waraka mmoja ambao mtoa hoja ameuambatanisha ni Waraka kutoka kwenye chombo cha Mamlaka ya Serikali. Mamlaka tunayoiamini ni *TPA*, yaani Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari. Unapokuwa na chombo ambacho ni cha Serikali, kinalinda maslahi ya taifa zima na kinatoa dosari; huna namna nyingine isipokuwa lazima ukubali kwamba hoja ni nzito.

Mamlaka ya Bandari imekaa tarehe 27 Septemba, 2007 kule Tanga na iliainisha kasoro zote ambazo Mheshimiwa Zambzi, amerudia kuziainisha leo. Ameonyesha wakati mkataba unaongezwa takwimu zilionyeshwa kwamba utendaji kazi (*performance*) ya Kampuni ya *TICTS* ulikuwa umeshuka. Kwa vyovyote vile, kwa mtu yeyote makini, asingeweza kuongeza mkataba wakati utendaji kazi unashuka na vipengele vyote vya mkataba vilikuwa vinabana. Kwa dhahiri hii ni hoja ya msingi na wenzetu hawa wakiwa chini ya Mwenyekiti wa Bodi, ninadhani ni Ndugu R. Mollel, sina hakika kama huyu ndiyo Katibu Mkuu aliyeko Wizara fulani hivi sasa. Anaitwa R. Mollel, Mwenyekiti wa Bodi. Ninaomba niikubali hii *document* na nitambue mamlaka hii kwamba, inalinda maslahi ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ambayo nilitaka niizungumzie ni hoja ya kwamba, kweli tumeingiziwa ndani ya Bunge lako Tukufu, Waraka ambao hauna saina. Kwa bahati mbaya, umekwisha kuutolea maamuzi asubuhi leo, sitaki kuyakiuka maamuzi yako. Ninataka nitambue tu kwamba, Waraka ulioingizwa hauna saina, wala kinachoonekana kwamba ni majadiliano yaliyotoka kwenye Kamati ya Bunge, jambo ambalo linalidhalilisha Bunge letu, kuingiziwa Waraka ambao hauna mtu tunayemtambua. Kwa Kanuni zetu, nyaraka zinazolingia Bungeni zinasainiwa, hata *Order Paper* kila siku inasainiwa ili kukiwa na kitu, tuweze kumhoji aliyetoa Waraka huu. (*Makofi*)

Kwenye Waraka huu ambao tumesambaziwa asubuhi pamoja na *Order Paper*, ukitazama ukurasa wa 4, unapingana na ukurasa wa 8; jambo ambalo Mheshimiwa Zamboni amesema tunadanganywa. Sasa huko nje tumedanganywa, Serikali imedanganywa, Bunge linadanganywa; hivi ni wapi nchi hii inapelekwa? Ukisoma ukurasa wa 4, kampuni hiyo inatuambia kwamba, imewekeza takriban milioni 16 dola za Marekani. Kwenye ukurasa wa 8, kampuni hiyo hiyo, kwenye Waraka huo huo inasema, imewekeza dola za Marekani milioni 15.368. Ukirudi na ile nukta 368 wala siyo nusu, ingekuwa nusu ungesema wamekaribia milioni 16, lakini ukirudi kwenye Waraka wa Mheshimiwa Mwenyekiti wa TPA, mwaka jana hadi Septemba, 2007, wenzetu hawa walikuwa wamewekeza milioni 7.9 dola za Marekani. Sasa je, hizi takwimu zinazotofautiana namna hii, tunapoletea kuna *interest* gani ya hawa kuweza kutuletea taarifa ambazo hazina msimamo wowote? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme kitu kingine ambacho kimeshtua zaidi; katika barua ambayo imeandikwa na Mheshimiwa Benjamin Mkapa na Mheshimiwa Basil Mramba, ambayo imesomwa hapa na nimemtaja Mheshimiwa Mkapa, ninafikiri kwa makusudi. Barua iliyoandikwa na Mheshimiwa Basil Mramba ya 6 Septemba, inatumia maneno mazito sana, kwa ajili muda nisome tu vipengele vinavyonihusu hapa. Inasema; muda wa mkataba uongezwe kuwa miaka 25 ni agizo hakuna chombo chochote kinachofanya tathmini.

Ameanzia huko juu anasema, ninakutaarifa kuwa, Mheshimiwa Rais, ameagiza Wizara ya Mawasiliano, hususan Mamlaka ya Bandari, kutekeleza yafuatayo; kwa hiyo, ni agizo. Imeagizwa tarehe 6 Septemba, 2005, tupo katikati ya kampeni ya uchaguzi. Bunge lako lazima lijiulize hapa kuna nini; ni kweli kazi ya Serikali huwa haisimami wakati Bunge limevunjwa wakati tuko kwenye uchaguzi; lakini unapobadilisha mkataba katikati ya kipindi ambacho Serikali haifanyi kazi ni lazima ujiulize kuna nini? Mimi ninathubutu kusema, hapa kuna wingu la rushwa. Kwa vyovyote vile, hakuna atakayeweza kunibishia ushahidi ulioko; *performance* iko chini, utendaji kazi kwa maana ya vitu vilivyotakiwa vifanyike viko chini, kifungu kinachoongezwa ni pamoja na *exclusivity clause*, *royalty* inayotolewa haiwiani na mapato au faida inayopata kampuni.

Tunataka kujua hapa ni kitu gani kimetokea? Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu ameishia kusema mkataba ni batili? Kama Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu anasema mkataba huu umekosea, tunataka kujua na aliyesaini barua hii Mheshimiwa Basil Mramba, ninakumbuka nilisimama ndani ya Bunge lako wakati tunapitisha Sheria ya Manunuzi ya Taifa, nikawa ninajaribu kusema ni mpaka lini taratibu zetu za Serikali zinakiukwa? Mheshimiwa Mramba alisimama hapa akasema, Waheshimiwa Wabunge, mkipitisha sheria hii ndiyo mwisho. Hiyo ni 2004. Mwaka 2005, Mheshimiwa Mramba anasaini amesahau alichokitaja mwaka mmoja uliopita! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge lako ni lazima lipate majibu ya kuridhisha, hatuwezi kuendelea kufanya kazi ya umma na kazi ya taifa katika utaratibu wa namna hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme tu vilevile kwamba, nimeshtushwa na jinsi uwiano huu unavyokwenda, lakini vilevile Agizo la Mheshimiwa Rais, pamoja na Waziri linasema, apewe na eneo lingine. *TICTS* waruhusiwe kutumia geti namba 8 na ardhi ya karibu naye, yaani inatolewa na tuna malalamiko ya muda mrefu. Tulikuwa na malalamiko kuhusu bandari yetu, jinsi wawekezaji walivyopewa bila kufuata utaratibu. Sasa inafika hapa, agizo linatoka kwenye ofisi ya juu ya taifa. Suala hili si suala la kuliona kwa utani, si suala la ushabiki, wala si suala la vyama ni suala la rasilimali ya taifa; ni mabilioni ya fedha yaliyopotea katika suala hili. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge wote, tuwe na uchungu katika suala hili, sizungumzi kwa sababu mimi ni CHADEMA, ninazungumza kwa sababu hapa kuna maslahi ya nchi yetu na taifa. Chombo cha *TPA*, ambacho ni chombo chetu, kinatuthibitishia kwamba maslahi ya taifa yamekiukwa.

Ninaomba katika kumalizia nikubaliane na mtoa hoja kwamba, tumalizie hilo kwa kusitisha mkataba huo mara moja na Serikali tangu ilipopata taarifa ya *CAG*, ilitakiwa kuchukua hatua lakini imechelewa. Sasa mpaka tunafikia hatua hii, maana yake ni kwamba, utendaji kazi wa Serikali unaanza kutiwa doa; kwa nini Bunge liingilie wakati mkaguzi ametoa taarifa? Tutafanya hivi mara ngapi; hoja zipi tuanze kuwa tunazileta ndani ya Bunge wakati *CAG* wetu, chombo tulichowakabidhi kazi wanatufanyia kazi ya namna hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sitaki kuchukua muda zaidi ili wengine nao wapate nafasi ya kuchangia, ninaomba kusema ninaunga mkono hoja na ninasema kwamba, tusitishie mara moja na Serikali ilete ndani ya Bunge hili, taarifa kamili kwa nini kulikuwa na shinikizo kutoka Uongozi wa Juu, ikiwemo Ikulu na Waziri wa Fedha na matatizo haya haya yamejitokeza kwenye mikataba mingine ambayo tutaendelea kuijadili ndani ya Bunge lako Tukufu? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dr. Slaa. Sasa ninamwita Mheshimiwa Nazir Karamagi na wakati huo huo, ajiandae Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka.

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Nami ninashukuru kuchukua nafasi hii, ili niweze kutoa mchango wangu katika hoja ambayo iko mbele yetu. Kwa ruhusa yako, ninaomba nitoe maneno yafuatayo kwamba, ninataka kutangaza *conflicts of interest*; mimi ni mwekezaji katika Kitengo cha Kontena kinachozungumziwa. Ninasema hilo kusudi yale nitakayoyasema, yasiye yakanukuliwa kama ninajitetea kwa kificho. Ninasema hivi mbele ya Bunge hili, ambalo linawatangazia Watanzania wote kwa ujumla ili nao waweze kujua hali ilivyokuwa huko nyuma na ilivyo hisi sasa mpaka Kitengo hicho sasa hivi kinamezewa mate. (*Kicheko*)

Lazima kusema ukweli, Kitengo cha Kontena, Bandari yetu *Tanzania Harbours Corporation*, ilikuwa inakiendesha kwa muda mrefu bila ufanisi ambao haukuiridhisha Serikali, wakaamua kukibinafsisha na wakati wanakibinafsisha ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Karamagi, ninataka nikusomee Kanuni ya 61, hujakamilisha. Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 61 inasema hivi na nitamtaka sasa Mheshimiwa Nazir Karamagi aifuata kauli yake: “Wakati wa majadiliano Bungeni au kwenye Kamati yoyote ya Bunge, Mbunge hataruhusiwa kuzungumzia jambo lolote ambalo yeye mwenyewe ana maslahi binafsi nalo ya kifedha, isipokuwa baada ya kusema jinsi anavyohusika nalo na kutaja kiwango cha maslahi hayo.” Sasa umetaja tu kwamba, wewe unahusika, unatakiwa utaje kiwango cha maslahi ndiyo uendelee. Mheshimiwa Karamagi. (*Makofi*)

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, mimi ndiye mmiliki wa Kampuni ya *Harbours Investment Limited*, ambayo ina asilimia 30 katika Kitengo cha Kontena na ni Mwenyekiti wa Kampuni ya *TICTS*. Vilevile ni mwekezaji mzalendo, ambaye nilishiriki mwanzoni kabisa walipokuwa wanabinafsisha sehemu mbalimbali katika Vitengo vya Tanzania.

**SPIKA:** Sawa, sasa limekaa vizuri endelea.

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunisahihisha hilo. Nilichokuwa ninasema ni kwamba, wakati ule makontena yaliyokuwa Bandari pale kwa mwaka yalikuwa wastani wa chini ya laki moja. Uwezo wa Kitengo cha Kontena cha Dar es Salaam ni 250,000, kwa hiyo, kwa kuwa na kiwango cha chini ya laki moja, Kitengo hicho bila shaka kilikuwa kinafanya chini ya asilimia 50, kwa hiyo, makontena machache yalikuwa yanapita Tanzania ya kwetu, pamoja na nchi jirani. Meli chache zilikuwa zinakuja hapa Tanzania. Kwa hiyo, ilibidi kukibinafsisha kusudi kuhamasisha meli nyingi zije Tanzania na Kitengo kile kianze kuchangia katika uchumi wa Tanzania. Hiyo ndiyo ilikuwa msingi wa kukibinafsisha.

Kilipobinafsishwa kikaanza kazi. Mazingira ya kazi pamekuwepo na hoja muhimu, ambayo inabidi iangaliwe kwamba, Kitengo kile uwezo wake ni makontena laki mbili na nusu. Matarajio wakati kinabinafsishwa kwamba, yule ambaye atakuja angalau kwa miaka kumi, azidishe ufanisi mara mbili ya Kitengo hicho. Makontena ambayo yalikadiriwa mpaka mwaka 2010 ni kufikia laki mbili na thelathini na nne elfu. Limezungumziwa jambo la vifaa wakati wa mahojiano, Bandari ilikuwa na kitu ambacho kinaitwa *Rubber Tire Gantry*, ambazo zinapandisha mizigo kumi na mbili juu mara tatu, ingawa moja ilikuwa mbovu, tunaweza kusema ni kumi na moja. Kwa kutambua kwamba, Kitengo hicho kina uwezo wa makontena laki mbili na nusu, kinatosha kupakia makontena kwa kupandisha mara tatu kwa miaka hiyo kumi. Kwa hiyo, haikutarajiwa, wala siyo kwamba haikutarajiwa kwamba, mwekezaji atakapokuja atawekeza hela nyingi sana, ilikuwa ni kuongoza kile Kitengo na kuweza kutumia umaarufu wa kampuni itakayokuja, kushawishi meli zije hapa na kuleta makontena yetu. Kwa hiyo, makadirio yalikuwa ni kidogo tu.

Hata hivyo, baada ya kuanza kufanya kazi katika kipindi cha miaka minne tu, makontena yalifikia laki mbili na elfu hamsini na tisa. Kwa hiyo, Kitengo cha Kontena Dar es Salaam, mwaka 2004 kikawa kimefikia ukomo wake. Sasa kazi hapo ilikuwa ni moja, ambayo hapa Waheshimiwa Wabunge wanauliza; je, ilipofika 2004 Kitengo

kikafikia ukomo wake; kazi ambayo ilikuwa inategemewa kufikiwa mwaka 2010; palikuwepo na hoja mbili tu kuwaambia kwamba, jamani meli Tanzania sisi tumetosheka, Kitengo chetu kimefikia ukomo wake, acheni tuendelee na laki mbili na nusu zinatutosha.

Serikali haikuona busara kwamba, tukomee pale. Kwa hiyo, mazungumzo ambayo yalifanyika 2005, ingebidi yafanyike 2010, kwa sababu ndipo matarajio yalikuwa yanategemewa kiwango kile kifikie konteina laki mbili karibu na nusu. Kwa hiyo, hayo matatizo ambayo yamejitokeza sasa, tunaweza kusema kwamba, Kitengo cha Kontena ndicho kimesababisha chenyewe, kwa kufanya ufanisi ukawa mkubwa kwa haraka zaidi. Hili ndilo lililotokea, maana yake ingekwenda taratibu kama ilivyo, mwaka 2004 badala ya makontena laki mbili na elfu hamsini na tisa, ilikuwa imetarajiwa yawe laki moja na elfu hamsini na ufanisi ungekuwa mzuri, mlundikano usingekuwepo. Kwa hiyo, Kitengo cha Kontena kingekuwa kinapata sifa kama ilivyokuwa hapo zamani.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kusema hivyo, ninaona nirekebishe kasoro ambazo nimeziona kwenye hoja hii, kusudi Waheshimiwa Wabunge nao wakati wanafanya uamuzi, wafanye uamuzi ulio sahihi.

Mheshimiwa Spika, samahani, ninatafuta karatasi ambayo nilikuwa nimeandika lakini siioni. Nitatumia hii moja kwa moja, ambayo ninayo hapa. Tunaambiwa kwamba, Kitengo cha Kontena kilikuwa kinafanya vizuri mpaka mwaka 2005, ufanisi ukaanza kuteremka. Hii ni kweli na imeoanisha katika karatasi ambayo ilikuwa Miundombinu. Kitengo cha Kontena, kweli kilikuwa kinafanya kazi vizuri mpaka Bandari ilipojaa; ni kama msongamano wa Dar es Salaam. Dar es Salaam ina msongamano wa magari, mpaka zikaanzishwa njia tatu. Sijui unaweza kumlaumu nani kama hutaongeza barabara?

Bandari haifanyi *TICTS* peke yake; kuna meli zinaingia, *GPA*, Mamlaka ya Mapato, watu wanavyopitisha *documentation* zao na kuna *TISCAN*. Kwa hiyo, hawa wote wanahusika namna gani, mzigo pale unaweza ukapita kwa haraka. Kama meli imekuja ikapakua mzigo pale kama inavyopakua hapa, imeonekana hapa mtoa mada ameonyesha *imports* ndiyo zina matatizo. Kweli meli inapokuja inapakuliwa, ikipakuliwa ukaiweka kwenye *Yard*, sasa wenye mizigo wasipoiondoa; *TICTS* unataka waitupe majini au waifanye nini? Inabidi ikae nayo, sasa itafanyaje, maana ingekuwa mizigo haijafikia kiwango kilichotarajiwa sawa sawa, lakini eneo ni finyu; eneo ni dogo, kama barabara Dar es Slaam ni ndogo, magari yamekuwa mengi; sasa unataka magari mengine yapite hewani? Ndiyo ilivyo kama *TICTS*.

Imefanya ufanisi, makontena yakaja mengi Tanzania, bandari ikajaa, sasa lililopo ni kukaa chini, kuangalia tunaweza kurekebisha miundombinu yetu na kubadilisha sera zetu za kutoa makontena. Lakini siyo kumlalamikia yule ambaye amesababisha makontena yaingie mengi. Hapa ndiyo naona kasoro ambayo inabidi nisahihishe. Pili, kuna kasoro ambayo inazungumzia kwamba Kitengo kiliongeza muda wake kwa kuvunja sheria. Haikuvunja sheria. Makontena ambayo inabidi kuingia Dar es Salaam kwa

mujibu wa Kitengo kile ni laki mbili na nusu. Sasa hivi yamefikia laki mbili karibu na sabini na kitu. Mwaka huu yatafikia laki nne.

Nyongeza ya laki moja na nusu, Serikali isingefanya uamuzi huo, tukayakosa hayo. Hasara kiasi gani ingeingia Serikalini? Hiyo ndiyo hasara ambayo ingeipata na ndiyo imelazimu Serikali wafanye hivyo, lakini Serikali watazungumza. Lngine ni kwamba, huu mkataba uliongezwa tu na barua na Mheshimiwa Waziri Mramba, ambaye alipewa maamuzi na Rais, hii si kweli. Baraza la Mawaziri lilikaa na ilikuwa siyo mwezi wa tisa, barua iliandikwa mwezi wa tisa labda, lakini Baraza la Mawaziri lilikaa mapema. Ninafikiri Serikali yenyewe watazungumza kama ni kweli au si kweli, kwa sababu haya mambo ya *documentation* huwezi ukayalazimisha.

Tatu, ni kwamba, uwekezaji ambao anauzungumza umefanyika kweli, anashangaa vifaa vya milioni tisa kuingia katika miezi mitatu. Mwezi wa kumi na mbili, zimeingia *rubber gantry* tano, waliziweka hata kwenye picha, zenye jumla ya shilingi milioni saba. Leo hii tunayozungumza, wanapakua *mobile rubber gantry graize* mbili. Kwa hiyo, vifaa kuingia vya shilingi milioni tisa unakuwa umeviagiza muda mrefu uliopita, kama tulivyozungumza leo asubuhi vile vifaa havipo madukani, unapoviagiza unalipa halafu vinakuja.

Kwa hiyo, tusishangae shilingi milioni tisa, hizo tumekwisha lipo kweli na vifaa vinaingia labda kesho ama keshokutwa, mtaona kwenye magazeti. Kwa hiyo, ninafikiri kwamba, muda umekwenda haraka haraka; sababu za kuongeza mkataba zilikuwepo, Kitengo kilikuwa ukomo umefikia 2004, Sheria ya Manunuzi haikukiukwa. Kulikuwepo na sababu, hasara ingepatikana tusingefanya hivyo. Kitengo kina laki mbili na nusu, mmefikia laki mbili na elfu thelathini na tisa, mwaka huu itakuwa laki nne. Kama huoni udharura hapo, utakuwa na wewe ni wa kushangaza. Nimesema haya kusudi Watanzania watufahamu, si wanajua tuko *Container Terminal* wanatufahamu, tusije tukaamua tu kwa *ku-feel* kwamba, Serikali walikuwa ni wajinga, hawajui wanachokifanya, hapana wanajua wanachokifanya na wao wana maslahi ya Taifa.

Kuna upungufu mkubwa uliopo unatokana siyo na *TICTS*, isipokuwa matatizo yanatokana na ufanisi wa *TICTS*, ambapo vitengo vingine kama miundombinu, walipokaa wakaona kwamba, bandari kumbe inahusisha wote, sio *TICTS* peke yake. Maana yake wengine wanafikiri ni *TICTS*. Wakae wote waangalie miundombinu, kwa mfano, hata hii wanayozungumza kukaa muda wa siku 60, kuna wengine wanatumia bandari kama *store*, hawataki kuchukua makontena yao. Wengine magari yanachukua muda mrefu kwenda nchi za jirani na kurudi zaidi ya siku 60. Ninafikiri haya yote yameandikwa kwenye kiambatanisho ambacho kimetolewa na ninataka kusema kwamba, ili kuiweka katika *Hansard* na kutoa upungufu kwamba, mimi ni Mwenyekiti wa Kitengo cha *Tanzania International Container Terminal*. *Document* iliyotolewa, tunaomba samahani kwa niaba yako kwa sababu ilikuwa iwe kama ilivyokuwa *presented* kwenye Kamati ya Miundombinu, tunaikubali. Kwa hiyo, kwa kosa lolote ambalo lipo kwa kutumia fursa hii ikubalike kwamba, wataikubali hiyo kampuni kama ilivyoandikwa kwenye hiyo *document*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaona Kitengo cha Kontena, kihukumiwe kwa ufanisi wake mzuri uliosababisha Tanzania tuwe na matatizo ya kuangalia, sasa tuanze kuangalia miundombinu ya kuleta makontena zaidi, badala ya kumhukumu yule aliyefanya kazi vizuri kwamba, aondoke sasa tumlete ambaye atarudisha ufanisi chini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kutounga mkono hoja, kusudi yale niliyoyazungunza yarekebishwe. Ambaye alifikiri yapo sahihi; si sahihi, takwimu ambazo anazo humu sasa hivi siyo sahihi, vile vilivyokuwa vimeelezwa awali ni kweli.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutounga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Anna Abdallah.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68(7), ninaomba mwongozo wako, msemaji wa sasa atusaidie. Hakuwa Waziri wakati ule, lakini anathibitisha hapa kwamba, hili jambo liliamuliwa na Baraza la Mawaziri. Mimi kwa uwelewa wangu, jambo likishaamuliwa na Baraza la Mawaziri, mwandishi anakuwa ni Katibu wa Baraza. Sasa pengine hayo anayajua zaidi, kuliko sisi tunavyojua. Pengine ungemtaka pia atufafanulie juu ya jambo hili. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Anna Abdallah. Ninadhani hili la msingi, katika vile viambatanisho ambavyo niliruhusu viingie ndani ya Bunge, ingependeza kama tungekuwa na barua inayonukuu uamuzi wa Baraza la Mawaziri. Sasa kama kweli ulikuwapo uamuzi huo na tunajua maamuzi hayo huwa yanaandikwa rasmi, kama alivyosema Mheshimiwa Anna Abdallah, kwa dokezo la *Chief Secretary*; sasa sijui Mheshimiwa Karamagi kama upo ushahidi huo basi useme na udhihirike; kama haupo basi uondoe maneno kwamba, mkataba huu ulipitishwa na Baraza la Mawaziri?

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Mheshimiwa Spika, mimi nina ushahidi kutokana na maandishi ambayo yalitumika wakati tunafanya majadiliano na *PSRC*, ambapo mbele yao walikuwa na waraka ambao ulikuwa unatoka kwa Baraza la Mawaziri, ambao unaruhusu kuanza kufanya majadiliano na *TICTS*.

**SPIKA:** Basi ninakupa hadi kesho uweze kuwasilisha, vinginevyo, itabidi Kanuni zitumike kuhusiana na kulidanganya Bunge. Kwa hiyo, ninakupa hadi kesho saa 5.00 uweze kunifikishia ushahidi huo. (*Makofi*)

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya *TICTS*. Kama unavyojua, wakati wa Mkutano huu wa Bunge ulipoanza, mimi sikuwepo na nichukue nafasi hii



kukushukuru wewe kwa sababu nilikuwa ninashughulikia maafa ya wapiga kura wangu wa Mererani.

Nichukue nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Serikali, Mawaziri na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, kwa kutuma Kamati mbili za Bunge kuja kushirikiana nasi; Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Ulinzi na Usalama; na Kamati ya Nishati na Madini. Zaidi ninalishukuru Bunge lako, kwa kuchangia maafa ya Mererani. Kwa hiyo, ninakushukuru Mheshimiwa Spika kwa haya yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuja kwenye kikao hiki kwa siku hizi mbili, wakati kuna ndugu zetu 17 ambao bado hawajaopolewa. Sababu kubwa ilikuwa ni kuja kuwashukuru, lakini nimeikuta hoja hii ya *TICTS*, nikaona nisiwe bubu niseme machache.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, ambalo ningependa kuchangia ni kumpongeza Mheshimiwa Zamboni, kwa kuleta hoja hii. Mwandishi mmoja maarufu wa magazeti maarufu tu hapa nchini, aliwahi kusema maneno haya katika moja ya makala zake; ninaomba kunukuu: “Inapofikia hatua Dola kuwa kiziwi na kushindwa kusikia wananchi wanasema nini na Bunge nalo linaziba masikio, kunakuwa na Dola kiziwi na Bunge kiziwi na huo ndio mwanzo wa mparaganyiko katika Taifa hilo na kifo cha Dola hiyo.”

Mheshimiwa Spika, lakini mimi ninaongeza, unapokuwa na Serikali na Bunge sikivu kama Serikali tuliyonayo sasa na Bunge sikivu kama hili unaloliongoza, unakuwa unaijengea dola hiyo na Bunge hilo uhalali wa kuishi katika miyo ya hao milele. Nilitaka kukwambia kwa hatua uliyochukua wewe na Kamati ya Uongozi, kukubali hoja zote zilizoletwa zenye sifa ya kuitwa hoja, zije hapa kwenye Bunge ikiwemo hii ya *TICTS*, inajenga uhalali wa Bunge lako na Serikali yetu kwa umma wa Watanzania, nilitaka nikuhakikishie hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lipo suala ambalo ninapata utata, ambalo huko mbele lazima tuliangalie na hili ni la mgongano wa maslahi. Kwa sababu leo tulikuwa na hoja iliyohusu masuala ya *RITES*, tulikuwa na hoja iliyohusu Vitalu; wamiliki wa vitalu vile hawakuja kwenye Bunge hili kupata nafasi ya kujieleza, kama ambavyo wamiliki wa makampuni mengine kama ya *TICTS*, walivyopata nafasi ya kuja kueleza haya. Hivyo hivyo, wale wa *RITES* hawakuja hapa. Tatizo ninalolipata, ndio ninapokubaliana na Hayati Edward Moringe Sokoine, pale aliposema katika moja ya hotuba zake; ninaomba kunukuu: Hayati Edward Moringe Sokone, alipokuwa akiendesha vita vya uhujumu na walanguzi (*the war of the economy and sabotage and racketeers*) alisema: “Tumeruhusu walanguzi na wahujumu uchumi kuongoza nchi, wananchi wamefikia mahali ambapo wanashindwa kutofautisha kati ya Viongozi wa Chama na Serikali na walanguzi na wahujumu uchumi wa nchi.” (*Makofi*)

Simaanishi kwamba, waliozungumza hapa ni wahujumu uchumi hapana. Ninataka kusema, suala la mgongano wa maslahi na umuhimu wa kumuunga mkono Mheshimiwa Rais Kikwete, katika kutenganisha utumishi wa umma na hasa uongozi huu na biashara. Hapa lipo tatizo. Haya mambo yanahitaji kuangaliwa, kwa sababu

mikataba hii tunayoiingia, inapofikia mahali kwamba wanaoingia mikataba hii kwa niaba ya nchi wamekubali kwa namna moja au nyingine, kujenga ubia na wale wanaoitwa wawekezaji, kwa namna yoyote uchumi wa nchi utawanufaisha wale wanaoitwa wawekezaji na nchi itabaki haina mapato na mfano mzuri ni huu wa *TICTS* wala usiende mbali. (*Makofi*)

Mapato wanayopata ndugu zetu wa *TICTS* na mapato yanayoingia Serikalini, hayana uwiano hata kidogo. Inakuwa mbaya zaidi, kama ambavyo mtoa hoja alivyozungumza, juu ya kuvunjwa kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma, iwe Baraza la Mawaziri limekaa liwe ni agizo la Waziri, liwe ni agizo la nani. Ninataka kusema, katika Sheria ya Manunuzi sioni mahali bwana mkubwa yeyote anapotamkwa hapo. Kwa hiyo, ninataka kusema, Sheria ile imevunjwa wala tusipoteze muda, nyongeza ile ifutwe na itenguliwe na tusihangaika kupoteza muda wa Bunge lako na wenzetu waombe radhi. Kwa hiyo, *in fact*, nilifikiri muungwana yeyote, angesimama awaombe radhi Watanzania na Bunge hili, kwa kuingiwa mikataba ya aina hiyo, tusipoteze muda.

Mheshimiwa Spika, lakini sisi tunatoka kwenye Chama kimoja kinachoitwa CCM, ambacho kinaheshimika sana. Tulisema katika ahadi zetu rushwa ni adui wa haki, sitapokea wala kutoa rushwa. Tukasema cheo ni dhamana, sitatumia cheo changu wala cha mtu mwingine, kwa faida yangu. Unapokuwa na mikataba yenye utata kwa kiwango hiki, unafika mahali unasema hao walioweka sainsi hapa, sitaki kwenda mbele zaidi. Ninasema tunahitaji kutazama mambo haya. Mmoja wa wazungumzaji, alipokuwa akizungumza, sijaona mahali akikanusha, kaka yangu Mheshimiwa Karamagi, sijaona mahali akikanusha au akibainisha ule mkanganyiko uliopo kati ya kiwango cha uwekezaji kilichotajwa na mmoja kati ya Waheshimiwa Wabunge, waliokuwa wamezungumza hapa. (*Makofi*)

Hapa kuna wawekezaji wa bilioni 16, sehemu nyingine kuna bilioni sita, sehemu nyingine kuna kumi na kitu. Ukishafika mahali hapo, tulifikiri tungepata majibu ya mkanganyiko huo wa uwekezaji. Lipo tatizo la msingi, ambalo tunahitaji kuwasaidia Watanzania. Tunahitaji tuwasaidie maana wamechoka kusikia lugha inayoitwa ya ufisadi, lugha ya mikataba mibovu ambayo inapelekea kupotea kwa fedha zetu kwenda nje na kutengeneza matajiri wa dharura ambao wana fedha haramu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utajiri huo wa dharura, unahitaji kutazamwa kwa sababu fedha zinakwenda nje. Namna ya Bunge hili na Serikali hii kuendelea kujenga uhalali ni kufanya kazi moja tu; kushughulikia fedha zetu zilizokwenda katika akaunti za nje ya nchi, zile ambazo zimepatikana kwa njia ya haramu zinarudi ndani ya nchi yetu. Fedha zile ambazo hata kama zipo katika mabenki yetu ya ndani, *NMB*, *CRDB*, iwe benki yoyote, tunazichukua maana ni jasho la Watanzania. Tubainishe tu kwamba, umezipata kwa njia isiyo halali, tuzidai zirudi zivasaidie Watanzania kujenga shule zao. Tusipoteze muda na tusiwaonee haya watu hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama juzi ulikuwa na ng'ombe 50 au 200 tu kama Sendeka, lakini leo una maghorofa na hatukuulizi, ninaogopa kidogo kwamba, tunakokwenda sio kuzuri sana; kwa nini mkubali kupata faida kubwa kama ni wazalendo, upate faida kubwa

na nchi yako inapata kidogo na wale *co-partners* wako waendeleo kuhamisha kupeleka pembeni, sasa kwa nini tusihoji kwamba hata uzalendo huo nao unatiwa mashaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ubia huu kati yetu tulioamua kuingia na hao wanaoitwa wawekezaji wa kutoka nje, una matatizo makubwa na ni lazima tukubali kwamba, kama unajua kabisa kwamba wewe una matatizo ya aina hiyo ni vizuri ukafanya toba sasa, lakini wakati wa mafisadi kufanya toba ili tuendeleo kukaa nao. Wafanye toba ya kweli kwa kurejesha fedha za Watanzania walizozichukua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kazi yangu ilikuwa moja ni kumuunga mkono ndugu yangu, Mheshimiwa Zamboni, kwa hoja yake kwamba, uamuzi wa Serikali na utaratibu uliotumiwa na Serikali katika kuweka nyongeza ya Mkataba utenguliwe ile miaka 15 itenguliwe. Ninaunga mkono itenguliwe na usiwepo mjadala mkubwa kwenye hili. Ila ninachowaomba wenzangu wa Serikali watusaidie; hivi wakati mikataba hii inapowekwa, kama maslahi ya nchi hayakuzingatiwa katika kuangalia kile kinachorudi Serikalini kama mrabaha; hamwoni kwamba upo uwezekano pia wa mikataba hii tutakapotengua, hawa wakaenda Mahakamani maana pengine kuna *provision* iliyokuwa inawalinda; maana juzi tulisikia ile ya *DOWANS*, Mwanasheria mmoja akisema hebu njooni tukutane?

Sasa hawezi kusema hivyo kama kiburi hicho hakiwezi, hakina *provision* inayomlinda kwenye mkataba. Sasa ninaogopa kwamba, hebu wanasheria watuungalizie hii mikataba, maana hapa sisi tumeazimia kwamba, tutatengua hii nyongeza, kwa sababu tumeshawishika na hoja zilizoletwa kwamba, zinakidhi. Mikataba hiyo mingine iangaliwe ili *repercussion* isirudi kuwa mzigo tena kwetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nilisema tu nisimame nikushukuru kwa niaba ya Wananchi wangu wa Simanjiro, lakini niweke na mimi mkono wangu kwenye hoja ya *TICTS*, kwa lugha ya kistaarabu tu kwamba itenguliwe na fedha kama zipo walizozipata ambazo hawakustahili kuzipata wazirejeshe, tufanyie kazi nyingine.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ole-Sendeka. Nilikuwa nao wachangiaji wawili; Mheshimiwa Ahmed Ali Salim na Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa. Kwa kuzingatia pande za Muungano, nitampa nafasi ya mwisho Mheshimiwa Masolwa halafu Naibu Waziri wa Miundombinu.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

**SPIKA:** Samahani sana Mheshimiwa Ahmed Ali Salim, kwa sababu muda hauruhusu kwa sasa.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Nami niungane na wenzangu, kumpa pongezi Mheshimiwa Godfrey Zamboni, kwa kutuletea hoja hii ambayo inazingatia

maslahi ya nchi yetu. Kabla sijaendelea, niseme tu kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, matatizo yaliyo katika Kamati yetu ninayafahamu, *TICS* na mambo mengine. Ningesema tu kwamba, katika maelezo yangu ambayo yatakuwa mafupi sana, nitafanya *reference* kwenye nyaraka hizi *documents* tatu. Kwanza ya mtoa hoja, lakini na hii ya *TICS* ambayo kama alivyosema, Mheshimiwa Dr. Slaa ni kwamba haijasainiwa, lakini pia na hii ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu, ninasema *TICTS* haina mkataba hata mmoja, kwa sababu ukiangalia mkataba ambao wamewekeana na Serikali, ukurasa wa kumi wa taarifa ya mtoa hoja, pamoja na mengine kwamba, watafanya *ammendment* kwenye *schedule* na nini, lakini kile kipengele cha mwisho kabisa wanasema, *ammendment of the term shall not be permitted*.

Mheshimiwa Spika, sasa bahati nzuri kidogo, niliwahi kufanya kazi ya u-*coordinator* katika mradi mmoja pale uwanja wa ndege. Kwa hiyo hizi sheria nilikuwa ninazifuatilia sana na ilifikia *time tuka-terminate contract* na kampuni moja. Sasa ikiwa makubaliano yaliruhusiwa katika mkataba wa kwanza, ukaambiwa mkataba huruhusiwi kufanya *extension of time*, lakini ukafanya, maana yake ume-*breach contract*. *It means* kwamba, *TICTS* kipindi walichosainia ule mkataba wa pili, ilikuwa hata wa kwanza ame-*breach contract*, kwa maoni yangu. Sasa kwa kuwa labda ni huruma na wapo Watanzania wenzetu wamewekeza, tuchukue hii ya pili ambayo nayo ilikuwa batili; na hii imekuwa batili kama tutasoma taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; katika ukurasa wa 108, *CAG* kasema katika mikataba dhaifu na isiyoeleweka, huu wa *TICTS* ndiyo umekuwa namba moja. Huyu ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali yetu hii. Amefanya *reference* hizo hizo; *reference* ya kwanza ule utaratibu wa kifungu cha 69, Sheria ya Manunuzi haikufuatwa, pamoja na kwamba, Waziri alipeleka barua ya kusema kama tulivyoona kwamba, ameagizwa na Ikulu iwe hivyo, lakini hakuna aliye juu ya sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *PPRA* ninafikiri ni Sheria ambayo imepitishwa na Bunge, inastahili kuheshimiwa. Sasa huu mimi ninasema haukuwa mkataba, isipokuwa ilikuwa ni maagizo; maagizo na mkataba ni vitu tofauti. Zaidi, kifungu cha Kanuni ya Manunuzi Namba 117 cha mwaka 2005, kimesisitiza pia kwamba, mara baada ya kusaini mkataba au maandishi ya makubaliano, kwa vyovyote vile hayawezi kubadilishwa au kurekebisha ilimradi mabadiliko au marekebisho hayo, hayaitetei hasara *procuring entity*, lakini yalibadilishwa kinyume na utaratibu. Hiyo nimesema 9.1, amefanya *mistake* hapa ni 91, lakini ni 9.1 ya mkataba wenyewe imeonesha pia ni batili. Ame-*conclude* vizuri kwa kusema, kifungu hiki kinaelezea masharti ya mabadiliko ya mkataba lakini msisitizo ni ule tu wa kutofanya mabadiliko yoyote. Kwa hali hii ongezeko la muda wa mkataba uchukuliwe kuwa ni batili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niunge mkono kabisa kwamba, miaka 15 haikuwa halali na ifutwe, lakini pia ningekuwa mtoa hoja ningesema, hata hii miaka kumi ilikiukwa, mkataba haupo. Tulikuwa tunazungumza hewa, hakukuwa na mkataba, waliposaini waka-*block*. Tuchukuwe hii, hata huyo kaka yetu *CAG* ameiona hiyo ila hakuiona ya mwanzo, tuseme kwamba, miaka 15 isitishwe na kwa hiyo ufuate utaratibu.

Nikiangalia pia maelezo ya *TICTS* katika kuwekeza; Mheshimiwa Dr. Slaa, kidogo alilisema kwa ujumla kwamba, ukurasa wa nne na wa nane, kuna *contradiction*. Hakusema tu kwamba, amesema katika ukurasa wa nne, mwaka 2000/2007 aliwekeza dola za Kimarekani milioni kumi na sita. Sisi Kamati ya Miundombinu, tarehe 23 Januari, 2008, tulipewa ripoti kwamba, amewekeza zaidi ya dola milioni sita. Katika taarifa hii ya leo ukurasa wa nane kwenye jedwali hili, amewekeza jumla ya dola za Kimarekani milioni 15.368. Si unaona pale inakuwa kuna matatizo hapo?

Kwa hiyo, kwa kweli hata hawa ndugu zetu tunawasaidia hii miaka kumi ya mwanzo, ninafikiri hawa hawapo wazi; kwa nini wanaficha? Sasa sioni sababu kwa nini sasa tuwaachie tu iwe miaka miwili, kwa sababu hata ile taarifa inakuwa inaji-*contradict*, tutaamini vipi sasa? Serikali ni vyema tu ikubali kwamba, tulifanya makosa, tuli-*breach contract*, kwa hiyo tuna-*terminate*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, sitachukua muda mrefu kwa sababu sikutaka kutoa ngonjera, nilikuwa ninaingia kwenye *point* tu kwamba, namna gani miaka 15 wasipewe *TICTS*.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa mara nyingine, ahsante. (*Makofi*)

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye hoja hii ya Mkataba wa *TICS*. Kwanza, niseme toka mwanzoni kwamba, sina matatizo na hoja hii na kwamba, ninaikubali. Mwishoni nitakuja kuelezea tu kwamba, *process* sasa ya kutekeleza hoja tunakwendaje, kwa sababu ina *process* zake, lakini kimsingi sina matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, suala la *TICS* limelalamikiwa sana na wadau mbalimbali; Wabunge, Wananchi na sisi Serikali tukaliona. Ninataka niseme hata kule kukubali kwangu kwa haraka, ukweli ni kwamba na sisi tulishaona kwamba, kuna malalamiko hapa. Tumeanza kuchukua hatua ambazo zinaelekea hukohuko kwenye hoja hiyo, sema tu kwa sababu Serikali inapofanya mambo inakuja kutoa matokeo. Hutangazi kwamba, sasa leo nimefanya nini, kesho nitafanya nini; ni pale mwisho ukishatoa maamuzi sasa yanatoka wazi ama *press release* au ukitakiwa kutoa katikati. Unatoa mwishoni, labda ikionekana kwamba, Serikali ilikuwa haijaanza kutekeleza, lakini labda nieleze.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la *TICTS*, imeelezwa sina haja ya kusema jinsi ambavyo ufanisi ulikuwa ni mzuri pale miaka minne, mitano ya mwanzo. Limekuja kuonekana tatizo baada ya kuonekana msongamano mkubwa wa makasha pale Dar es Salaam. Kama ule msongamano usingekuwepo na mambo yangekwenda kama pale mwanzoni, labda hata haya mengine yasingeonekana, kwa sababu makasha yangu yanatoka. Watu wanataka ufanisi; makasha yaende, biashara ifanyike, nchi ipate faida na wananchi wafaidike. Baada ya makasha kuonekana kwamba, kuna msongamano, mambo hayaendi pale, ndio watu wakasema nani anayetoa makasha? Wakasema ni *TICTS*. Basi kuna matatizo, hebu tuangalie mkataba wake, kwa hiyo, ndio watu wakarudi kwenye

mkataba wa *TICTS*, kwa nini kuna msongamano? Hawa ndio wanatakiwa waondoe, wapakue na kupakia makasha, basi tuangalie. Nielezee kwanza hilo la msongamano.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, ufanisi wa *TICTS* umepungua, lakini msongamano pale kwenye bandari sio tatizo la *TICTS* peke yake. Kwa hiyo, tuangalie na ujumla huo kwamba, sasa hivi tunayo matatizo mengi. Hii ni kwa sababu ya neema, biashara imekuwa nzuri, biashara ya *container* ikaongezeka *by 20 percent* sasa hivi na meli zinasafirisha mizigo kwa asilimia 20 ni *containers*, haikuwa hivyo. Sisi tumepata biashara kubwa na ufanisi uliokuwepo pale mwanzoni, tukaanza kupata biashara kubwa. Yale tuliyotegemea kupata kwenye makontena laki mbili na thelathini na nne mwaka 2010, tumeshafika laki mbili na hamsini, tukawa tumefikia. Kwa hiyo, kumbe kuna matatizo mengi.

Sasa matatizo ambayo tumeyaona pale, ukiacha uwezo huo wa kitengo, lakini kumekuwepo na matatizo mengine ya utoaji wa *containers* pale bandarini. Kwa maana hiyo sasa, hata wanaochukuwa makontena yao hawafanyi hivyo. Nafasi za kuweka makontena, *capacity* imekuwa ndogo na *TICTS* hawakuwa na uwezo wa kuongeza maeneo ya makontena. Vilevile na *TISCAN* ambao ni wadau wengine, sasa wanashughulikia makontena machache zaidi, 81 badala ya 200 waliyokuwa wanafanya. Yapo matatizo ambayo yametokea mengi tu, sasa nafasi ile ambayo ni ya makontena 7,500 sasa hivi mpaka makontena 10,000 ua 11,000 yanafika pale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya matatizo yote haya, tukaona kwamba, wadau wanaohusika ni *TICTS*, lakini na wengine. Tukakaa pamoja kama Serikali, *TPA*, *SUMATRA*, *TICTS* wenyewe, *TRA*, Polisi, Uhamishaji, hata *TANROADS*, wale wenyewe wadau akina *TAFSA* na wale wakala wa meli, wenye mabasi, kwa sababu kuna masuala ya reli, uwezo wake, barabara kutoka pale, mambo haya yote tukayaangalia. Kwa hiyo, tukaanza kuchukua hatua kama Serikali. Hatua za muda mfupi tufanye nini? Tukaunda *Task Force*, jamani tuangalie namna gani tufanye.

Kwanza, tukaikabidhi *TRA* waanzishe *Inland Container Depots (ICDs)*. Nazo hizo sita za awali, ambazo zilikuwa zimeshaandikishwa, *capacity* yake imeshajaa. Tukasema tuweke tozo zaidi kwa hawa wanaoshindwa kuondoa makontena, haijasaidia sana. Kila mtu afanye kazi saa 24, tuweke kampeni za watu kuondoa makontena yao na mambo kama yale. Tuongeze na minada, wale ambao wamechelewa tuuze vitu vyao mara mbili kwa wiki, badala labda ya mara moja. Tutafute maeneo mapya na kadha wa kadha. *TICTS* tukawaambia ongezeni sasa kazi ya kazi zenu, ufanisi wenu uongezeke. Tukawaambia *TPA* na hawa jamaa wa *containers*, hizi meli ndogo ndogo tunaweza tukapakua haya makontena yake kwenye eneo lile la *general cargo*, badala ya kwenye eneo lile la makontena na zile *trans-shipment* kwenda Zanzibar na Tanga, basi tuzipe vipaumbele. Yote haya ni katika kujaribu kupunguza.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa ajili ya muda wa kati na muda mrefu, tukawaambia *TICTS* muongeze vifaa zaidi. Vilevile na sisi kama Serikali, tuongeze nafasi zaidi ndani na nje maeneo ya kuweka makontena. Ule mfumo wa teknolojia ya *scud* ulikuwa haujaanza kutumika kwenye geti namba 5 na namba 8, tukasema jamani tuufanye kwa sababu unaharakisha hasa katika *documentation*. Vipi tunaboresha sasa

barabara kutoka kwenye eneo lile na suala la reli ambayo inaunganisha na haya magari ambayo yapo pale; hivi tukiyatoa tukipunguza kwa kuweka *parking* ambayo ni *multi-storey*, ghorofa; tutapunguza eneo ambalo magari mengi yamekaa pale? Hiyo ni ya muda mrefu, lakini lazima tuanze sasa kuangalia kuweka *new container terminal*. Ndio tunazungumzia sasa *batch 13* na *14* pale mbele ya *K.O.G.* na Serikali imejipanga na *TPA* katika mpango wa muda mrefu, kutekeleza hayo. Sasa *Task Force* hiyo niliyoisema ya muda mrefu, inafanya kwa ajili ya shughuli ya muda mfupi, imekuwa ikifanya kazi sana na imepunguza. Kwa sasa hivi hata meli ambazo zilikuwa zinakaa mpaka siku 27 pale bandarini, juzi zilikuwa zinakaa siku 15, imepunguza.

Mheshimiwa Spika, lakini bado hiyo haiondoi ukweli kwamba, tuna tatizo na *TICTS*, kwa maana ya ule mkataba, ambayo sasa ninataka nije kwenye suala hilo. Tumeona kwamba, kuna udhaifu, na tukasema jamani lazima tuzungumze na wenzetu, tuanze kurekebisha huu mkataba. Ndio nilikuwa ninasema katika kutekeleza hata hili azimio, ukishaingia kwenye mkataba ni rahisi kusema kwamba, mkataba ni batili kama upande mmoja peke yake wameamua kuuvunja, unaweza kusema ni batili. Umekwenda amesaini yeye na wewe ukasaini na wewe umejikamata. Kwa hiyo, lazima kuwe na *process*, kwanza, majadiliano yeye aseme hii *signature* yako na amesema Mheshimiwa Ole-Sendeka; je, nikienda Mahakamani?

Kwa hiyo, *process* ile ni ya majadiliano kwanza, halafu mfike mahali muone kwamba, kama amekataa, kwa sababu na yeye anafuata *signature* yako hiyo ya barua kama ni ya Mheshimiwa Mramba, imetoka wapi? Yeye anaangalia umesaini huu mkataba na mimi nimeusaini, sote tulikuwa tunajua. Kama ulikuwa huna akili timamu uniambie. Tulusaini kama Serikali, sasa lazima *process* ile tuifuate kwa maana ya majadiliano kwanza, tukishindana tuangalie sasa *repercussions* za kwenda mbele, kwa maana ya kwenda Mahakamani ili tuweze kufuta na kutekeleza Azimio la Bunge.

Tumeona mambo mengi sisi ukiacha la *exclusivity* na hiyo ya miaka kumi kwenda miaka 25. Kwanza ni *performance* na hapo ndipo tunaanza kwamba, jamani *performance* yako imeshuka. Kulikuwa na vigezo na vilikuwa vichache. Ile ya *crane moves per hour* peke yake. Tunasema tuna mambo mengi *due time* mbona ipo? *Ship time, turn round, track time* na vitu kama hivyo, havipo. Tuondoe *exclusivity*, tuweke vigezo vingine na mrabaha upo chini tuongeze. *Performance bond* yenyewe ndogo na vile vifaa ilikuwa haisemi kwamba, ukishavitumia vile vya *TPA*, ukimaliza uvirudishe. Sasa ni lazima tuweke na *investment plan* yako tuielewe na iwekwe na kwamba, utanunua vifaa gani. Kwa sasa ilikuwa ni kwamba, ukiona inafaa ulete. Hata hizi bilioni unazozitungumzia, aliona inafaa, lakini kwa nini haipo kwenye mkataba? Lazima uweke kwenye *investment plan*.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nimalizie kwa kusema kwamba, baada ya kuona hivyo, tuakaandaa timu ya ku-*negotiate* kutoka Serikalini kwetu na Wataalam, ambao wanatusaidia na tukawaalika. Kitu kizuri, wamekubali na majadiliano tunadhani yanaanza wiki ijayo. Kabla ya hapo, *TPA* nao wamewaandikia kama *performance* ilivyoonyesha kwamba, kwa mujibu wa mkataba uliopo ni kwamba, *performance* yenu imeshuka, mtueleze kwa nini imeshuka na hiyo inaweza kupelekea kuvunja hata ule mkataba kama ulivyo. Acha tu kuendelea mpaka 2010, lakini hata kuuvunja mapema,

kwa sababu kama maelezo yao hayataosheleza. Labda wanaweza kuleta maelezo, lakini kitu muhimu mimi niseme kwamba, vipengele vyote vya mkataba tumeanza kuvipitia na kuna maeneo zaidi ya 15 ambayo tunaona kuna udhaifu.

Mheshimiwa Spika, sasa *process* ya kuendelea nayo ndio hii niliyoieleza. Kwanza ya majadiliano; wewe ulisaini pale ukiwa na akili yako timamu na tulikuwa na akili zetu timamu; huwezi ukasema sasa kuanzia leo hakuna, lazima ujadiliane nae, useme bwana hapa lazima twende kurekebisha. Akigoma kwa sababu *signature* yako ipo pale ndio mnaelekea huko sasa kwenye sheria; uanaangalia hasara ikoje. Tunachosema sisi kikubwa katika hili ni ile *exclusivity clause*; tupanue uwanja, wengine waje.

Ndio maana tunasema hata akimaliza kama tutakubaliana kwamba 2010 tunasitisha na yeye aje 2000 katika kile kipindi kingine na wengine waje na sisi tuwe tayari kuweka waingie kwenye *procurement process* tuone ni nani atakayeweza kufanya vizuri. Hapa hapa, huyu tumgawie huku na yule tumgawie huku ili ufanisi uwepo kutokana na ushindani. Ndio nia yetu kama Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu wiki ijayo tunadhani tutaanza *negotiations*, bahati nzuri na ninyi mmetupa sasa *inputs* na ile nguvu, tunadhani tutalikamilisha hili mapema na tutatekeleza yale ambayo Bunge linataka; tutasikia na yeye anasemaje kwa maana ya vifungu vya sheria au *ata-appeal* wapi, kwa maana ni mkataba ambao umesainiwa na pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa ninamwita mtoa hoja, Mheshimiwa Godfrey Zambi. Kwa kuwa hata Serikali imekuunga mkono, sasa ninadhani hauna haja ya maneno mengi sana ni kuwasilisha Azimio lako ili tuliamue. (*Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja yangu. Kwanza, ninaomba nianze kwa kuwashukuru wachangiaji wote, ambao wamechangia katika hoja hii na Mheshimiwa Karamagi, ambaye pia amegoma kuiunga mkono hoja hii. Ninajua kwa nini hawezi kuunga mkono hoja hii. Ninaomba niwatambue waliochangia kama ifuatavyo: Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa na Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga. Hawa walichangia kwa kuzungumza Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wapo Wabunge waliochangia wa maandishi kama ifuatavyo: Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Severina Mwijage na Mheshimiwa Manju Msambya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba niseme kwamba, ninawashukuru sana wote ambao wamechangia kwenye hoja hii, kwa sababu wengi wameniunga mkono, ukiondoa Mheshimiwa Karamagi.



Mheshimiwa Spika, kwa ufupi sana, ninaomba niseme mambo machache yafuatayo: Niwaombe Waheshimiwa Wabunge walioniunga mkono kwamba, sitazungumza kwa kumuunga mkono mmoja mmoja, lakini nitalisema kwa ujumla kwa sababu ninataka nifupishe kadiri ninavyoweza. Ninataka nizungumze mambo machache yanayotokana na yale ambayo amezungumza Mheshimiwa Karamagi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaomba nikushukuru kwamba, umemwomba Mheshimiwa Karamagi, alete au aonyeshe Waraka wa Baraza la Mawaziri, ambao anasema kwamba, pengine uliridhia uongezwaji wa muda kutoka ule mkataba wa awali. Nami ninadhani nitakuwa nimefarijika sana.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nchi yote inaongozwa na utaratibu wa sheria, hatuwezi kusema kwamba, Baraza la Mawaziri limeridhia, lakini limeenda kinyume na utaratibu basi twende nao hivyo hivyo. Wakati mwingine huwa ninasema, unaweza ukawa Waziri au nichukulie mfano tu wa Mheshimiwa Rais; hawezi kusema kwa sababu mimi ni Rais wa nchi, basi ninakuta nyumba ya mtu huyu ninambomolea tu kwa sababu ni Rais wa nchi. Haiwezekani, lazima kuwe na taratibu zile ambazo zinapaswa kufuatwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Karamagi, ametueleza kwamba, walifikia uwezo mwaka 2004, yaani *capacity* hiyo ya *container* mwaka 2004. Sasa hapa watu wanaweza wakajiuliza; hivi hawa watu hawakuwa na *business plan*, yaani walikuwa wanafanya mambo tu kutoka hewani, kwa sababu kwa vyovyote vile ni lazima walikuwa wanafikiria kwamba hii biashara yao itakwenda namna gani? Sasa anapoweza kuja leo akalieleza Bunge kwamba, mzigo ulikuwa mkubwa katika muda mfupi, *then* tukashindwa cha kufanya, sisi tutamshangaa walikuwa wameamua kufanya biashara namna gani; biashara ya kukisia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia Mheshimiwa Karamagi, anasema kwamba, sheria haikuvunjwa. Nimeshangaa kidogo, lakini pia ninataka Watanzania waelewe kwamba, Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Fedha za Serikali, ambaye nchi hii imemwamini, ambaye Rais amemwamini na Bunge hili limemwamini, amesema wazi kabisa kwamba, sheria hii imekiukwa. Sina sababu ya kurudia ku-*quote* vifungu kwenye kitabu hiki cha CAG, kwa sababu wasemaji waliopita wamelisemea hili. Kwa hiyo, CAG ambaye tumemwamini amethibitisha kwamba, sheria ile au mkataba ule wa pili ni batili. Ameshauri hivyo na kwamba, Serikali ichukue hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la kwamba, makontena yamejaa, kwa hiyo, wakakosa pengine mahali pa kutunza mizigo. Hoja hii na mimi ninaomba sana niseme ninamshukuru sana ndugu yetu CAG, Mheshimiwa Utouh, amefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Ripoti hii ya CAG inaishia tarehe 30 Juni, 2007, kwa hiyo ni *very recent*. Kwenye Ripoti ya CAG, ninaomba niseme mambo machache, ambayo utaona kwamba, yanapingana kabisa na ya Mheshimiwa Karamagi, ambayo anataka Watanzania wayaamini. Moja, kwanza CAG anasema, uhai wa mtambo wa *container terminal* ulikuwa umeisha, yaani muda chakavu, kwa kiasi cha asilimia 66. Kwa hiyo, kiwango cha kufanya kazi kilikuwa chini na hata ufanisi ukarudi chini. Kipengele cha

pili, CAG anasema, vifaa vichache vilivyoununuliwa na mkodishaji havikuwa vipya; vingi muda wa uhai wake ulikuwa umekwisha kabisa. Tatu, anasema, ilibainika kwamba, mkodishaji alijikita zaidi katika vifaa chakavu wakati akifanya matengenezo. Hapa ndio anapozungumzia *cannibalization* ya vifaa vingine ambavyo alikodisha kutoka TPA. Hii ni hatari sana, Mheshimiwa Karamagi, anataka tuamini kwamba, waliwekeza sana katika kununua vifaa wakati ukweli ni kwamba, walikuwa wananunua vifaa ambavyo ni *used*, wakati mwingine wameenda mpaka ku-*canibalize* vifaa vingine ambavyo walikodisha kutoka TPA. Haya ni makosa makubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo CAG amelisema, hawa TICS walipewa muda wa kutosha kabisa kwamba, waende sehemu nyingine ambako wangeweza kuweka makontena. Lakini kwenye taarifa hii ya CAG anasema, hali halisi ya mkodishaji kuwa mzito kukubali kuhamisha makontena kutoka bandarini na kupeleka sehemu iliyokuwa wazi kule *Ubungo Inland Container Depot*. Wao ndio waliokuwa wazito, hapa Mheshimiwa Karamagi anasema kwamba, Serikali inawezekana haikuridhia mapema ili waende kule, lakini CAG ametuambia wao ndio waliokuwa wazito. Ndio hapa ninaposema, pengine hawakuwa na *business plan* ya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, ninataka niwaombe Watanzania, lakini pia zaidi niombe Serikali; ifuate taratibu, sheria na kanuni ambazo sisi wenyewe tumejiwekea. Mheshimiwa Karamagi, anaposema tuwapongeze kwa sababu shehena imeongezeka, mimi ninashindwa kuelewa. Unampongezaje mtu ambaye bandari ile pale kumekuwa na wizi sana wa vifaa vya watu kwa sababu ya *inefficiency* tu ya TICS! Tuwapongeze hawa TICS wakati wao wanapata *share* kwenye mapato wanayozalisha pale, Serikali inapata *just the meagre source* kutoka kwao, tuwapongezaje hawa watu! Tuwapongezeje kwa sababu wao wanapata hela nyingi sana au tuwapongeze kwa sababu wao wanataka wanufaike na mali hii asili ya Tanzania, wakati Watanzania wachache wapo kwenye umasikini? Haiwezekani, ndio hapa tunapoiomba Serikali, ichukue hatua za kuhakikisha kwamba, kasoro zile zinarekebishwa. Ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, ambaye amesema kwamba, Serikali imeliona tatizo hili na imeanza kuchukua hatua. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini ninaomba nieleze Serikali, maana yake hata Mheshimiwa Waziri, amenitia wasiwasi kidogo anaposema kwamba, hili ni suala la kisheria na mimi ninakubali ni suala la kisheria; lakini anaposema ni *process*, inawezekana akakubali, itabidi tuangalie, hapa wanatutia wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Bunge lako Tukufu, liielekeze Serikali kuhakikisha kwamba, mkataba ule unasitishwa na sio vinginevyo. Kama ni gharama tuingie; Serikali yenyewe itakuwa imetuingiza huko, lazima tukubali. Watu wasifanye makosa, baadaye waseme tutaenda kwenye *negotiations* tutawaambia Watanzania kwamba, tukienda mahakamani gharama zitakuwa kubwa sana, hapana. Tufike mahali tuseme makosa yakifanyika yarekebishwe.

Mimi ningependa tu niseme, jamani Serikali kukiri upungufu wala sio kitendo cha kudhalilisha hata kidogo; ni kitendo cha kujiamini na kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, ninatoka CCM, Wananchi wa Tanzania wana imani na CCM. Wanapooona makosa ambayo Mawaziri wa Chama cha Mapinduzi wanayafanya na Wabunge wa CCM tukasaidia kuyakosoa, Watanzania hawa wataendelea kujenga imani kubwa sana na Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, ninaomba nimsihi Mheshimiwa Waziri, hili walifanyie mkakati mkubwa na ninaomba utakapokuwa sasa unalihoji Bunge, tufuate Maazimio yalivyo na Serikali ije iripoti kwenye yale Maazimio kama yalivyopendekezwa kwenye hitimisho langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, sina sababu ya kusema mambo mengi, ninawashukuru waliochangia, wameiunga mkono hoja. Kwa hiyo, ninaliomba Bunge lako sasa liazimie kama vile nilivyosema.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Zambi, umekuwa wazi kabisa. Waheshimiwa Wabunge hoja iliyoko mbele yetu yenye sehemu mbili; iko pale ukurasa wa tatu wa hoja yenyewe. Kwamba, Serikali isitishie nyongeza ya Mkataba na kufanya mapitio ya mkataba wa awali na pili baada ya muda ya mkataba wa awali wa miaka kumi, Sheria yoyote izingatie Sheria ya Manunuzi ya Umma, hilo ndiyo lililoko mbele yetu. Kwa hiyo, sasa muamue hoja hiyo.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja Binafsi ya Utendaji Kazi Usioridhisha wa Tanzania International Container Terminal Services ilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, walioafiki wameshinda na kwa hiyo, Azimio la Bunge ni kama ambavyo liliwasilishwa na mtoa hoja na hilo ndilo agizo la Bunge. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(5) nitaisoma: “Iwapo shughuli zilizopangwa kwa siku hiyo zimemalizika kabla ya saa 1.45, Spika ataliahirisha Bunge bila kuhoji, lakini iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kufikia muda wa kuahirisha kikao na Bunge, na Bunge au Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi bado halijamaliza shughuli zake, Spika anaweza kuongeza muda usiozidi dakika thelathini, bila kulihoji Bunge au Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi ili kukamilisha shughuli zilizobaki.” *(Makofi)*

Sasa ninawaharifu kwamba, ninatumia mamlaka yangu kwa Kanuni hiyo, kuongeza kipindi kisichozidi nusu saa ili kuwezesha shughuli iliyobaki iendeleo na kama nilivyosema, tutahitimisha kesho. Ninatazimia leo mtoa hoja inayofuata, atazungumza kwa kifupi na tunaweza kupata mchangiaji mmoja au wawili. Kwa hiyo, sasa tunaingia katika hoja binafsi ya mwisho, inayohusu uuzwaji wa nyumba za Serikali na ninamwita mtoa hoja, Mheshimiwa Aloyce Kimaro. *(Makofi)*

## UUZWAJI WA NYUMBA ZA SERIKALI

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa hoja yangu, ninaomba nitoe wito kwa Viongozi wote, Wabunge wote, kwa Viongozi wa Dini mbalimbali na kwa wote wanaopenda maendeleo kwa Wananchi wa Tanzania na wanaopenda amani idumu katika nchi yetu; ninawaomba wote kwa moyo mmoja tufichue, tuchukie na tuseme hadharani, uovu wa aina yoyote unaojitokeza katika jamii yetu, bila kujali umetendwa na nani na wakati gani, Mungu ibariki Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa ninaomba niisome hoja yangu. Kwa mujibu wa Kanuni ya 54(1) ya Kanuni za Bunge, ninaomba kuwasilisha maelezo yangu binafsi, kuhusu uuzaji wa nyumba za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ibara ya 8(1)(a) inasema na mimi ninakuu: “Wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yoyote na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii.” (b) inasema: “Lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi. Ibara ya 9(h) inasema kwamba, shughuli za Serikali zitatekelezwa kwa njia ambazo zitahakikisha kwamba, utajiri wa utaifa utaelezwa, unahifadhiwa na unatumiwa kwa manufaa ya wananchi wote kwa ujumla na pia kuzuia mtu kumnyonya mtu mwingine. Kwamba, maendeleo ya uchumi wa Taifa yatakuzwa na kupangwa kwa ulinganifu.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ibara ya 63(2) inasema, kwa kuwa Bunge ndiyo chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano, ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi, kusimamia na kuishauri Serikali ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake. Baada ya maneno hayo ya utangulizi, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu, lijadili hoja nitakayoiwasilisha na kutoa uamuzi wa busara kwa niaba ya Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002, Baraza la Mawaziri liliamua kupitia Waraka Namba 7 wa mwaka 2002 ya kuwa, Nyumba za Serikali wauziwe watumishi, bila kuangalia bei ya soko na bei ya kiwanja. Baada ya maamuzi hayo na kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Naibu Waziri wa Miundombinu, hapa Bungeni mwezi Juni, 2007, alitamka ya kuwa, nyumba 7,921 ziliuzwa na mapato yaliyopatikana ni shilingi bilioni 59.1. Kiasi ambacho kilikuwa kimeshalipwa ni shilingi bilioni 29.1 tu na kwamba, kiasi ambacho kilikuwa hakijalipwa ni shilingi bilioni 30.4, zaidi ya nusu ya mapato yaliyotegemewa. Uamuzi huu ulitolewa na kutekelezwa, bila Serikali kuwa na nyumba nyingine mbadala kwa watumishi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali hapa; je, Serikali hiyo ya Awamu ya Tatu, ilipouza hizo nyumba ilitegemea hapatakuwepo tena Serikali nyingine na Watumishi wa Serikali? Ninachosisitiza zaidi ni kwamba, nyumba hizo zilikuwa ni rasilimali ya taifa na mali ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kweli ilionekana ni busara kuziua ni lazima zingeuzwa kwa faida. Baadhi ya nyumba, zilifanyiwa matengenezo makubwa kabla ya kuuzwa na bei sawasawa na bure. Haiwezekani nyumba ambayo ni rasilimali ya taifa kwa Watanzania wote, mkaamua kuiuza kwa shilingi milioni 15 badala ya shilingi milioni 200, ambayo ni bei ya soko. Pia wakati huo unauza hizo nyumba, unawaambia wale ambao ni mali yao, wachange pesa zikajenge madarasa, nyumba za walimu na zahanati! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mfanyakazi wa Serikali ameuziwa nyumba ya Serikali na kwa kuwa yeye na Serikali wana mkataba unaosema kuwa, kwa mujibu wa cheo chake ni lazima Serikali impe nyumba awapo kazini, kwa hiyo, Serikali inapata hasara ya kuuza nyumba na pia hasara ya pili ya kumpa *allowance* ya kukodisha nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali zote duniani, zina maeneo wanapoishi Viongozi kuanzia Rais, Mawaziri, Makatibu Wakuu, Majaji, Mapolisi, Wanajeshi na Wakuu wengine wa vyombo vya usalama.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya yanapokuwa karibu, inakuwa rahisi kuwapata hawa wanaoishi humo na kuwalinda. Ninaishauri Serikali, nyumba zilizouzwa zirudishwe na kwa kuwa hata Mheshimiwa Rais, alikwishasema nyumba zote nyeti zilizouzwa zirudishwe; nyumba hizo ni kama zile za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Polisi, Magereza, Madaktari na Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali yako, itoe orodha ya nyumba zilizouzwa kwa utaratibu ufuatao, ili wananchi wajue jina la aliyeuziwa, bei yake na eneo ilipo nyumba; tuanze na Wizara, twende kwenye Mikoa na baadaye kwenye Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Serikali itoe orodha ya nyumba ambazo ziliuzwa kinyume na utaratibu, kwa watu ambao hawakuwa Watumishi wa Serikali wa wakati huo. Ninaitaka Serikali kupitia Wizara husika, itoe orodha ya wafanyakazi wanaolipwa *house allowance*, kwa kukosa nyumba badala ya zile za awali kuuzwa. Pia ni kiasi gani cha pesa Serikali inalipa hotelini kwa kuwaweka Watumishi wa Serikali waliokosa nyumba.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi, ninashindwa kuona busara iliyotumika ya kuuza nyumba zilizopo Kilimani hapa Dodoma, kwa mfano, kwa bei sawa na bure na kwenda kujenga kule Kisasa, majengo ambayo kwanza hayavutii, wala sio imara na bei ya ujenzi ni kubwa! Vilevile kuuza nyumba za Msasani kwa bei ya chini na kwenda kujenga Mbezi, haukuwa uamuzi sahihi hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwa kuwa, viongozi waolitoa uamuzi huo walikosea, mtitiriko wa maamuzi haya unaashiria kuwa viongozi walioamua nyumba hizi ziuzwe bila sababu za kutosha, ndiyo waliokuwa wanahitaji nyumba walizokuwa wanaishi.

Hawa wafanyakazi wengine, wamekuwa ni wasindikizaji tu. Ninasema hivyo, kwa kuwa hakuna kumbukumbu zinazoonyesha kuwa, Wafanyakazi wa Wizara mbalimbali walikwishaomba kuuziwa nyumba wanazozitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba kusoma Azimio la Bunge Kuhusu hoja kama ifuatavyo:-

**KWA KUWA** Mwaka 2002 Serikali iliamua kupitia Waraka wa Serikali Namba 7 wa mwaka 2002 kuwa Watumishi wa Serikali wauziwe nyumba za Serikali;

**NA KWA KUWA** uamuzi huo ulitolewa na kutekekelezwa bila ya Serikali kuwa na nyumba nyingine mbadala kwa watumishi wake wapya na hivyo kuisababishia Serikali hasara kwa kulazimika kuwalipia watumishi wake wanaoishi hotelini kutokana na kukosa nyumba za Serikali za kuishi;

**NA KWA KUWA** uamuzi huo wa Serikali unaendelea kulalamikiwa sana na wananchi kuwa umeitia na unaendelea kuitia hasara Serikali;

**NA KWA KUWA** Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, alishatoa agizo kuwa nyumba zote za Serikali zilizouzwa kinyume na taratibu ikiwa ni pamoja na zile zilizouzwa kwa watu wasio wa Serikali zirejeshwe Serikalini;

**NA KWA KUWA** Serikali imekuwa inasuasua katika kufuatilia utekelezaji wa agizo hili la Mheshimiwa Rais;

**NA KWA KUWA** hadi kufikia Juni, 2007 zaidi ya nusu ya fedha za ununuzi wa nyumba hizo zilikuwa hazijalipwa;

**NA KWA KUWA** kwa mujibu wa ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sura Namba 2, Toleo la 2002, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndicho chombo kikuu chenye madaraka kwa niaba ya wananchi ya kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba Serikali ifanye yafuatayo: Itekeleze mara moja bila kusita, Agizo la Rais kurejesha nyumba zilizouzwa kinyume cha utaratibu na kwa watu ambao hawakuwa Watumishi wa Serikali wakati huo na vilevile nyumba ambazo hazikupaswa kuuzwa kama zile zilizopo kwenye maeneo ya Utawala wa Serikali; Irejeshe kwenye umiliki wake nyumba hizo zilizouzwa kinyume na utaratibu; Itoe orodha ya nyumba zake ambazo ziliuzwa kwa watu ambao sio Watumishi wa Serikali kinyume na utaratibu na pia zile ambazo hazikupaswa kuuzwa kutokana na unyeti wa kazi za Watumishi wa Serikali wanaostahili kutumia; na ichukue hatua kwa wale ambao hawajalipia na mikataba yao ya kuuziwa nyumba irejewe kuhakikisha kuwa malipo hayo yanalipwa mara moja ama mikataba yao kufutwa na nyumba kurejeshwa kwenye miliki ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo imetolewa na imeungwa mkono na kwa hiyo, ninaomba muiamue; ninao wachangiaji wanne kama ifuatavyo: Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu na Mheshimiwa Benson M. Mpesya. Ninadhani kwa leo tunaweza kuanza na hao wawili, pengine hata watatu, kama hawatarudia rudia, kwa hiyo, sasa ninamwita Mheshimiwa Maria Hewa.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ili niweze kuchangia hoja binafsi, kuhusu uuzwaji wa Nyumba za Serikali. Hoja hii ninaiunga mkono moja kwa moja. (*Makofi*)

Ninaunga mkono hoja kwa sababu zifuatazo: Watumishi wa Serikali, kwa hivi sasa wana shida kubwa sana hasa wale ambao wanahama kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Tunawaona watumishi hawa kama vile hawana sifa na wala hawana heshima ya uongozi, tunapowanyima nyumba na kuwaweka katika mazingira ya kuwa karibu na kupewa rushwa, tunawaweka katika mazingira ya kuwanyanyasa na tunawaweka katika mazingira hatarishi pia.

Kuna viongozi wengine, maisha yao yanakuwa hatarini kila wakati; unamchukua kwa mfano, kiongozi kama Jaji, unamuweka katika mazingira ya kawaida mtaani; unatarajia nini; anakuwa na maamuzi magumu anapokuwa kazini? Huyu mtu anapoishi katika mazingira ya kawaida au hotelini, hana ulinzi hana chochote, lakini masharti yake ya kazi yanamuweka awe na ulinzi ni hatari kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli katika hili, ninaona wazi kabisa kwamba, Serikali yenyewe ndiyo inasababisha hawa wenye heshima hizi, kuwa katika mazingira kama nilivyosema, kuzingirwa na maeneo ya rushwa, kunyanyaswa na kuwekwa katika maeneo ambayo ni hatari, kwa sababu ya unyeti wa kazi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, maeneo haya ya viongozi mara nyingi huwa yana masharti, wenzetu walipokuwa wanayajenga waliweka kabisa kwamba, yawe yana sifa mbalimbali, kwa mfano, yawe yanazungukwa na ulinzi na muda wao wa kufika nyumbani unaeleweka. Hivi sasa unawakuta wapo huko mtaani na wakati mwingine hata yale mahitaji yao muhimu, wanakosa mahali pa kuweka shughuli zao ambazo wanapaswa kuwa wanastahili zao. Kwa mfano, nyumba ambazo zilijengwa kwa watumishi kama niliowataja, huwa kuna maeneo kama ya *house boy counter* na askari wa kulinda. Mambo haya hayapo kwenye maeneo ambayo watumishi hao wanafikia hivi sasa. Wengine inafika mahali wanakosa hata kuishi na familia zao, kwa sababu maeneo ni finyu. Sasa katika hali hii, hatuwatendei haki wale watu wenye stahili za nyumba zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tunakuja kuwaweka hotelini hawa watumishi; wanatumia fedha za nani? Walio wengi wanatumia fedha za Halmashauri zetu na

Halmashauri zetu inafika wakati tunaziandikia Hati Chafu eti kwa sababu wametumia fedha vibaya, fedha hizo ambazo zingeliweza zikarudi kwenye matumizi mengine kujenga hata visima, zahanati na kufanya shughuli nyingine, matokeo yake wanatumia kumlipia huyu mtu ambaye amefikia hotelini na gharama zinakuwa kubwa kiasi kwamba, fedha hizo zinatumika katika matumizi ambayo si sahihi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunazionea Halmashauri zetu, kuziingiza katika matumizi ambayo wangeluweza kufanya shughuli nyingine badala yake, wanatumia kuwapangishia hawa watumishi ndani ya hoteli ambazo ziko karibu na Halmashauri hizi.

Mheshimiwa Spika, watoto wetu huwa tunawauliza; wewe utakapokua mkubwa unataka kuwa nani? Anasema ninataka kuwa Daktari, Jaji, *IGP* au *Pilot*, sasa anapokuwa na kusoma anajua nikisoma sana ninaweza nikawa na cheo kama hiki. Anajua kwamba ni heshima kuwa na cheo kama hiki. Akikua anajiandalia maisha mazuri, sasa leo anamaliza halafu unamuweka Mtaa wa Mtakuja au Mtaa wa Tupendane; anakuwa analijua taifa lake hivi ndivyo lilivyo kweli?

Ninaomba katika hili, hebu tuliweke taifa letu katika misimamo kabisa ya kujua kwamba, kuna watumishi wa ngazi fulani, ambao wanastahili kupata nyumba hizi. Kwa hiyo, anapohama kwenda mahali pengine, anajua anahama pamoja na heshima yake, ikiwepo na kukuta nyumba mahali anapohamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa vile umeomba tuzungumze kwa kifupi, ninaomba nizungumze kifupi kwamba, sasa ninadhani wakati umefika wa *graph* kufikia kileleni kwa haya tunayoyaona Serikalini. Imepanda vya kutosha *graph* hii, tunapozungumzia matukio ya ajabu, ninadhani sasa ifikie kileleni; tumezungumza vya kutosha, mpaka na hoja tumeingia nazo za kuchambua mambo ya ajabu, sasa *graph* hii ianze kushuka, tuanze kuzungumza mazuri ya nchi hii. (*Makofi*)

Tumechoka kugundua kila siku, acha tugundue lakini ifikie hatima sasa *graph* hii ianze kushuka, tuongeele walau basi maendeleo ya nchi yetu, badala ya kukaa kuongeele masuala ya kukosoana tu. Sasa tujirekebishe, tufike mahali tuzungumzie maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie. Ninamshukuru pia mto hoja, kwa hoja yake ambayo imenipa na mimi nafasi ya kuchangia, lakini ningeliomba sana Bunge hili tuwe waangalifu kidogo.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba ni kwamba, Bunge hili liwe na mtazamo wa kuipokea hoja hii kwa mapana kuliko ilivyokuja. Ninasema hivyo kwanza, nieleze waziwazi kwamba, mimi sina matatizo yoyote makubwa na hiyo dhana ya Serikali ya kuuza hizo nyumba. Sina matatizo, yapo madogo madogo tu ambayo ninaamini



yanazungumzika na yanarekebishika. Kwa ujumla, sina matatizo na dhana hiyo. Kwa hiyo, kwa mtazamo wangu, sehemu kubwa ya zile 7,900, kwa vyovyote vile na kwa mfumo ambao tuliokuwa na hapa nchini wa utunzaji wa zile nyumba, ingefika wakati zingelikuwa *condemned* na *not fit for human habitation*. Ukiachia tu yale machache, ambayo yalishughulikiwa, lazima tukiri, yanaweza yakashughulikiwa katika mada hii; kwa ujumla nyumba zilikuwa zimefika mahali pabaya.

**SPIKA:** Ninaomba utulivu Waheshimiwa Wabunge, tuwe na usikivu. Tumpe nafasi.

**MHE. FELIX C. MREMA:** Nipeni tu na mimi nafasi yangu jamani, niendeleo kusema. Shida yangu na hoja nzima ni kwamba, hawaangalii wale wafanyakazi wengi ambao hawakupata fursa hiyo ya kupata nyumba. Tupoteze wakati kufikiria hao ambao hawakupata bahati, watapata bahati ya namna hiyo kwa namna gani, maana wanahitaji hizo nyumba nao?

Mheshimiwa Spika, pili tuwafikirie pia wale ambao wanakaa kwenye nyumba za umma; kule Arusha ninao wanaokaa *AICC* na ni watu wadogo tu, nao pia wanataka wauziwe zile nyumba. Badala yake, *core business* ya *AICC* ni *conference* na *tourism*; hizi nyumba walizirithi tu na baada ya kurithi usimamizi wake una utata. Hivi juzi, wamepandisha bei ya kodi ya hizi nyumba kuanzia asilimia 60 kwa mkupuo mmoja mpaka 150, wapangaji wanalalamika.

Nimeleta malalamiko yangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, ameyapokea na ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa kuyapokea na wananchi wangu kule wanasikia kwamba, Mheshimiwa Waziri kaniahidi kuwa, anayafanyia kazi. Sasa mimi ninataka wanapoyafanyia kazi, hilo ongezeko la kodi kwa mkupuo mmoja asilimia 150 ni kwa sababu *AICC* yenyewe kazi yake siyo ya kupangisha na kukodisha, bali kazi zake ni *conference* na *tourism*; *i-concentrate* na *conference* na *tourism*, iache haya mambo mengine katika hizi sekta ambazo zinaweza kuendesha kazi hizi za kukodisha nyumba. Sasa ninaomba Mheshimiwa Waziri, hilo ulifanyie kazi lakini unapolifanyia kazi, ufikirie hoja ya kuwauzia hawa *AICC*.

Zipa pia na nyumba nyingine za Manispaa kule Kaloleni, Revolosi na Teni, zina hali mbaya sana. Nipigieni makofi, watu wangu wanataka kusikia hivyo. Zipa katika hali mbaya sana, watu wangu wale wachache tumeuziana nyumba nzuri kule *Corridor Area*, lakini hatukuwafikiria kuwauzia zile nyumba nyingine za Manispaa. Ninasema tuwafikirie wale ambao hawana hizi nyumba, yaani wale ambao wanahitaji hizi nyumba, hawa watu wa kawaida. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kinachonisumbua sana, mimi kwenye hoja hii iliyotolewa ile ya nne kwamba, hawa ambao wameshindwa kulipa wanyang'anywe. Kama mmeshindwa jamani, kwa sababu hawa hawana uwezo mnataka wakaibe? Mnataka watoe rushwa? Kinachotakiwa kufanyika ni kutengeneza utaratibu wa wao kuweza kupata mikopo, ile ile hoja yangu ya *mortgage finance*, jamani waweze kupata hii mikopo ili wakanunue haya majumba, tukamilishe hii *mortgage finance* kwa haraka sana. Watu waelewe mahali gani pa kuweza kupata mikopo ya miaka 20 au 30, ili wanunue

nyumba zinazouzwa, wajenge nyumba wanazotaka kujenga na waboreshe maisha yao. Vinginevyo, tutakuwa tunapoteza muda na vitu hivi vidogovidogo, kama kufuata watu wachache hawa, tulalamika sana na tukahamasika sana, haitupeleki kwenye tatizo la nyumba na makazi katika Tanzania hii. Kuna upungufu wa nyumba Tanzania wa milioni 2.2; hizo milioni 2.2 tutawawezeshaje watu wa Tanzania kuzijenga hizo nyumba na kuondoa upungufu wa makazi katika Tanzania hii? Tuweke nguvu yetu huko.

Kuna nyumba zaidi ya 50,000 ambazo watu wameshindwa kuzimalizia, kwa sababu hawana uwezo. Kwa hiyo, hizo nyumba 50,000 mtaji uliolala ni zaidi ya shilingi bilioni 1.5, mtaji ambao umekaa tu hausaidii kuchangia katika kuinua uchumi wa nchi yetu. Hayo ndiyo yatumize kichwa hapa jamani; ndiyo wakati mzuri wa kufikiria nchi yetu hii tunaiharakisha namna gani kuleta yale maendeleo ambayo wananchi wanayataka?

Mtaji uliolala shilingi bilioni 1.5 katika nchi maskini kama hii; hivi kweli tuna akili? Umelala kwa sababu watu wana hamu ya kumaliza nyumba zao, lakini hakuna utaratibu wa kuwawezesha kupata mikopo ili waweze kumaliza nyumba zao.

Tupeleke nguvu huko zikamilishwe hizo, halafu hayo matatizo mengine madogo tutaona yanajipa tu yenyewe, hatutakuwa tunakasirika sana, maana yake sasa hivi tuna kila sababu ya kukasirika. Tuna kila sababu ya kukasirika, kwa sababu mtu anakazana kujenga nyumba yake ya *cash*, analipa *cash* kujenga nyumba yake ni kazi ngumu sana kujenga nyumba kwa *cash* na duniani haifanyiki hivyo na hakuna mahali pengine inapofanyika hivyo. Kila mahali ni mikopo ya miaka 20 mpaka 30, unalipa taratibu huku umekwishahamia kwenye nyumba yako. Tuweke nguvu yetu kwenye kazi hiyo ya kutengeneza mfumo mzuri wa kuwawezesha wananchi wetu kupata makazi bora, kwa wakati na kwa njia ambayo inafaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ninadhani tujipunguzie kazi ya kesho, kwa hiyo, ninatoa dakika kumi hizo zilizosalia kwa Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba kuunga mkono hoja hii mia kwa mia, hasa kwa yale masuala ambayo ni Agizo la Rais kwamba, nyumba zilizouzwa kinyume na utaratibu na zilizouzwa kwa watu ambao hawahusiki, zirudishwe mara moja Serikalini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala hili la kuuza nyumba za wafanyakazi ambazo zilikuwa chache na kila siku wafanyakazi wanaajiriwa wengi hawatoshi kwenye nyumba, yaani kupewa nyumba za wafanyakazi ilikuwa si sahihi, lakini Waswahili husema maji yakimwagika hayazoleki na vilevile tunajifunza kutokana na makosa. Waingereza wanasema, *we learn through mistakes*. Kwa hiyo, lazima tujifunze, wale ambao walipata

nafasi ya kununua hizi nyumba kwa bei poa, wakiwa wafanyakazi wa Serikali na wanakaa katika hizo nyumba ambazo walikuwa wanakaa kama Wafanyakazi wa Serikali ni lazima wamshukuru Mwenyezi Mungu kama inawezekana, kwa sababu bei iliyonunuliwa nyumba ya Oyster Bay kwa mfano, kwa shilingi milioni 15 ni ndogo sana ni sawa na bei ya kununua kiwanja pale Mbezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa ninafikiria kiubinadamu, kama kweli sisi sote tunalitakia kheri Taifa hili na tunazitaka nyumba zile, yaani watu wanunue zijengwe nyumba nyingine, ninapendekeza kwamba, waongeze bei pale na wale walionunua walipe ile *difference*, yaani tofauti ile waliolipa na bei iliyo katika soko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilipoingia hapa Bungeni mwaka 1995, tulipewa mikopo ya magari haya Mashangini na tukatoa *order* ili yaende yakatolewe Japani. Tuliambiwa kwamba, mkopo wetu ni shilingi milioni 15, lakini magari yale yalipofika hapa wengine walilipa shilingi milioni 18 na wengine shilingi milioni 17, kwa sababu tulipojaza zile fomu ilikuwa shilingi milioni 15, lakini yalipofika hapa ile *Yen* ilikuwa imepanda bei na kwa hiyo, tulilipa zile tofauti.

Mwaka 2000 vilevile magari yamelipwa zaidi na mwaka 2005 ni hivyo hivyo, kwa hiyo, sioni ubaya wale ambao walipata zile nyumba na ile *area* ilivyo thamani ya ardhi, thamani ya nyumba na vilevile kuangalia Serikali imechukua gharama kubwa zaidi, ukichukulia wale wengine hawakuwa na nyumba, wafanyakazi wakapewa tena hela ya kupangisha mitaani. Kwa hiyo, ninapendekeza kwamba, waongeze pesa pale ili angalau iwe inafanana fanana na bei ya nyumba ile na *area* ile.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuna wale wengine wamepewa nyumba wala si wafanyakazi, bila kuchelewa ni wazi hii ni rushwa; utapataje nyumba na wewe si mfanyakazi wa Serikali? Kwa hiyo, ipo namna iliyotengenezwa pale na kama imetengenezwa namna hiyo hiyo, rushwa ni adua wa haki na mtoa rushwa na mpokea rushwa, wote wana makosa. Kwa hiyo, ninaomba Bunge lako Tukufu liseme kama ilivyopitishwa hapa kwenye azimio, nyumba zile zirudi kwenye Serikali. Kwa hiyo, yule ambaye alitoa pesa akaipata ile nyumba katika staili anayojua yeye, ambayo bila kuchelewa ni lazima ametoa rushwa, kulikoni amepata nyumba na yeye si mfanyakazi wa Serikali?

Kwa hiyo, ale hasara, nyumba zirudi mara moja kwenye Serikali na vilevile Serikali ichukue hatua kwa yule aliyeidhinisha kumpa nyumba, mtu ambaye si mfanyakazi. Hapo tukienda, ninafikiri tutakuwa tunaendelea kutoa chuya, ili mwaka 2010 tuwe na mchele safi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimezunguka leo kwenye Baraza au Wakala wa Nyumba ili nipate kwa nini hawa wanashindwa kujenga nyumba, kama kweli watu wote wamelipa, nikaambiwa kuna wengine hawajalipa; hivi ndugu zangu kweli kwa bei poa mliyopewa hiyo mmebebwa na bado mnashindwa kulipa; hivi ni nini? Hambebeki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninakubaliana kabisa na azimio hili, wale ambao wameshindwa kulipa nyumba zile zirudishwe Serikalini, kwa sababu hawa ni watu ambao tumezoea kubebwa, tumezoea kupewa vya bure na bure ni marehemu kwa sasa hivi. Kwa hiyo, wanafikiria kwamba, tukikaa muda mrefu bila kulipa Serikali itasahau au wataingia wengine au mafaili yatapotea; mtu anangojea kunyang'anya, kudhulumu nyumba ya Serikali, jasho la wananchi wa nchi hii na kodi zao zilizojenga nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, ninafikiri na ninaomba niunge mkono mia kwa mia, Agizo la Rais kwamba, nyumba walizoshindwa kulipa zirudishwe Serikalini, hakuna sababu ya kusema kwamba, mishahara kidogo na wala hakuna sababu ya kusema nini wala nini; maana kupanga ni kuchagua, kama wewe unataka kununua nyumba ile ulikuwa na haki ya kuchukua hiyo nyumba ili ukatwe kwenye mishahara au utaratibu wowote uliopewa kwa miaka kumi. Kama ulikuwa huwezi, ulikuwa una haki ya kusema ninaomba mnipe nyumba ya bei nafuu mkabadilishana, maana kuna wengine walikuwa wanakaa kwenye nyumba za bei nafuu na chini zaidi, lakini wana uwezo zaidi, wana mbinu nyingine za biashara, kwa mfano, kwa hiyo ulikuwa tayari, lakini kama unanyamaza wewe unataka kudhulumu. Kwa hiyo, ninafikiri hatuna haja ya kuchelewa, warudishe zile nyumba ili tuweze kuwapa wananchi wengine na wafanyakazi wengine.

Mheshimiwa Spika, lingine nililolipata leo ni kwamba, kuna nyumba, kwa mfano, hizi nyumba 300 za Dodoma hapa Kisasa, kama zingenunuliwa na fedha zikapelekwa kwa Wakala ni shilingi bilioni 13, lakini Serikali imetoa shilingi bilioni nne, bado shilingi bilioni tisa hazijatoka. Tunapomaliza, Serikali tunaitoa katika biashara tunawaachia watu wengine wachukue biashara na kuiendesha; kama hivyo, Serikali imejitoa kwenye ujenzi wa nyumba za bure kwa wafanyakazi wake, wamewapa Wakala.

Sasa Wakala hawa kama hamuwapi pesa ambazo zinatakiwa ziwe kama *revolving fund*, wapate zile pesa ili wajenge nyumba nyingine na zimmufaishe mtu mwingine, kwa kweli, Mradi wa Nyumba ni wa muhimu kwa sababu ukiangalia watu wote, hasa wafanyakazi wa Serikali wa zamani, wakati wa Azimio la Arusha, watu walikuwa hawawezi kujenga nyumba, unapata shilingi 1,150 au 1,165, unasaini Azimio la Arusha; hutakiwi kuwa na nyumba ya kupangisha na vitu kama hivyo. Hawa watu walikuwa waaminifu, hawakwenda kinyume na hakukuwa na ufiisadi wakati ule. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hawa walikuwa waadilifu na waaminifu kwenye nchi yao. Sasa hizi nyumba zimejengwa zinawasaidia, angalau wanapotoka pale wana makazi, kwa hiyo wanakuwa wanahangaikia ugali lakini huwezi kujua kama wanakula ugali na maharage kila siku au na dagaa katika nyumba zao, wapo kwenye nyumba zao. Kwa hiyo, hili ni suala zuri sana, lakini unapoacha kumlipa Wakala ili aweze kuendelea na hilo wazo la kujenga nyumba nyingine na wafanyakazi kila siku wanaongezeka, wanatoka vyuoni na kadhalika, wote wanakuja kutafuta kazi wanapata na wengine wanapanda vyeo inakuwaje?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Ahsante sana na ninaunga mkono hoja.

**SPIKA:** Tutakiuka Kanuni sasa tukipitiliza ile nusu saa ya Spika. Kwa hiyo, niwie radhi, lakini ninadhani uliyoyasema yamesikika.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika wakati wa kuahirisha shughuli kwa leo. Hoja ya Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro tutaihitimisha kesho asubuhi. Niwakumbushe tu kwamba, kesho ndiyo siku yetu ya mwisho kwa Mkutano huu wa Kumi na Moja, kutakuwa na Miswada ya Kusomwa Mara ya Kwanza baada ya kipindi cha maswali, lakini tutamaliza kwanza hoja ya Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, halafu Miswada ya Sheria, yatafuata Maazimio mawili, halafu hoja ya kuahirisha Bunge.

Niwakumbushe pia kwamba, mara baada ya hoja ya kuahirisha Bunge, tutaimba Wimbo wa Taifa. Kwa hiyo, mjikumbushe kumbushe, huwa ninaona wengine mnajiumauma tu. (*Kicheko*)

Ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Philip Sang'ka Marmo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge. Waheshimiwa Wabunge, mtakuwa mmepata barua hii, mimi ninasema huu ndiyo utaratibu mzuri wa kuendesha nchi yetu, pale ambapo Mheshimiwa Waziri, anaona katika jibu lake pengine hakueleweka vizuri, hakuna ubaya kusahihisha. Suala la Itifaki ya Wabunge, hasa Majimboni ni tatizo kubwa sana, kwa sababu hata mimi ambaye ni Spika, nikiwa Urambo Mashariki, mara nyingine unajikuta katika hii misafara ya Wakubwa, uko nyuma kabisa na Mheshimiwa Rais akisimama mahali, wengine na umri huu unakimbia kama uko gari la 17 ni matatizo kwa kweli. Kwa hiyo, ninashukuru sana kwamba, Serikali sasa imesema itaangalia hasa Jimboni, hatuhitaji mbwembwe kwingine lakini Jimboni.

Baada ya kusema hayo, sasa ninaahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 02.16 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 25 Aprili, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*